ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kateuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 9 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Katibu na leo kama kawaida kuna wageni wetu mbali mbali walioko kwenye ukumbi wa juu, ambayo ni sehemu ya wageni.

Wageni wetu wa leo wapo makundi matatu, kuna wageni wa Mhe. Fatma Mbarouk Said wa Jimbo la Amani, wageni hawa wanatoka katika *English Club* ya Zanzibar na Jumuia ya *ODYAZ* Jimbo la Amani na jumla yao wako wanane, nawaomba wasimame, wale pale na karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi jengine la wageni ni wageni wanaotoka *Tanzania Media Fund (TMF),* na jumla yao ni 11 na wanaongozwa na ndugu Ernest Sungura wapo hapa Zanzibar kikazi, nawaomba wageni hao wasimame, wale pale na karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi la tatu ni wageni wa mwenzetu Mhe. Ali Salum Haji wa Jimbo la Kwahani, hawa ni wanamichezo wa Skuli ya Msingi ya Muungano wako 25, na wao ndio Mabingwa wa Soka Wilaya ya Mjini kwa Skuli za Msingi, wanaongozwa na Mwalimu wao Habibu Ali Khamis, nawaomba wanamichezo wasimame, wale pale tena kombe lao wanalo pale na karibuni na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji tunakushukuru sana kwa kuwatengeneza vijana wakabeba Kombe la Wilaya ya Mjini Skuli za Msingi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, hao ndio wageni wetu wa leo. Kwa hivyo, wageni wetu karibuni sana nyote kwa jumla pamoja na wengine ambao mumekuja kwa shughuli zenu za kawaida. Hao ndio wageni wetu na nyote mnakaribishwa sana katika shughuli zetu.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Naomba kuwasilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii, lakini kabla sijawasilisha hati mezani naomba nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kuwapongeza vijana au watoto wetu kwa kupata ushindi wa kishindo, ambao wametokea katika Skuli ya Muungano Jimbo la Kwahani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba sasa uniruhusu kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 36

Kilimo cha Mwani na Uharibifu wa Mazingira

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Kwa kuwa ukataji wa miti ovyo husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Kwa kuwa wananchi wengi wa Zanzibar hususan akinamama wameamua kuwekeza maisha yao katika kilimo cha mwani, ambapo hulazimika kutumia miti katika ufungaji wa kamba zao baharini.

Je, ni lini wizara yako itafikiria utaratibu mbadala wa kufungia kamba zao badala ya kuendelea kutumia miti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusu yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake, naomba nikubaliane naye kwamba ni kweli ukataji wa miti ovyo husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Vile vile naomba nikubaline naye kuwa akinamama wengi wamejiajiri kupitia Kilimo cha Mwani, na hivyo hukata miti kwa wingi ili wajipatie vijiti ambavyo huvitumia kwa kufungia kamba za kuwekea mbegu za mwani.

Hata hivyo, hatua mbali mbali zimekuwa zikichukuliwa na serikali kupitia taasisi zake zikiwemo wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ili hatua kwa hatua kuwachisha wakulima wa mwani kuacha kukata miti ovyo hasa miti ya asili kwa kuwatafutia mbinu mbadala.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya, kwa ruhusu yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na taasisi nilizozitaja, zinaendelea na juhudi za kuelimisha wakulima hao wa mwani, jinsi ya kukata miti hiyo kwa utaratibu mzuri badala ya kuiua miti yenyewe, yaani kuwaelimisha kukata matawi, ambayo yataendelea kuruhusu miti hiyo kuwepo na kukua.

(ii) Kuwahamasisha wakulima wa mwani kupanda miti kwa wingi, ambayo wataweza kuitumia kwa ajili ya kupata vijiti vya kufungia kamba kwa ajili ya uzalishaji wa mwani.

Mhe. Spika, majaribio yamefanyika kwa wakulima wa mwani wa Uzi Ng'ambwa wa kupanda mwani kwa kutumia mawe na mpira, (*rubber band*). Majaribio hayo yameonesha mafanikio makubwa, majaribio hayo yalitekelezwa na Jumuia ya Wakulima wa Mwani na Uzi. Kinachoendelea hivi sasa ni kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kueneza utaalamu huo kwa wakulima wengine, ili waachane au wapunguze kwa kiasi kikubwa ukataji wa miti ovyo.

Mhe. Spika, majaribio mengine yamefanyika katika eneo la Fundo na Chumbe, ambapo Kampuni ya *BIRR* kwa ufadhili wa mradi wa *MACEMP*, walitakiwa kufanya majaribio ya kilimo cha mwani mnene.

Ingawa majaribio hayo yalilenga kutafuta njia ya kukuza uzalishaji wa mwani mnene wenye bei nzuri, pia umeonesha kuwa kilimo hicho kinaweza kufanyika kwa kutumia mianzi na malighafi nyengine za kuelea na hivyo kuachana na kukata miti ovyo. Suala la msingi linalohitajika hapa ni kwa serikali kueneza utaalamu huo kwa wakulima wa mwani nchini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri.

(a) Wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba yamepatikana mafanikio mazuri Uzi Ng'ambwa. Je, Mhe. Waziri umeshawahi kuiona Uzi Ng'ambwa na umewahi kufika, kwa sababu wanachi wale pamoja na maendeleo wanayoyafanya yote, lakini wamekuwa na kilio cha muda mrefu cha kuhangaika kubeba mwani wao na kuja mjini hana njia ya kupitia. Kwa hivyo, kuna mpango gani wa kuwatengenezea barabara ile, ili wananchi wapate miundombinu.

(b) Mwani huo mtawatafutia soko ili wapate ureda kama soko la karafuu kisiwani Pemba.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, swali la (a) naona kama liko nje kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri jibu hili la (b).

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru naomba niendelee kumfahamisha Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, kwamba Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais jukumu lake ni suala zima la kuratibu shughuli za mazingira.

Kwa hivyo, naomba nimuarifu kwamba nimewahi kufika Uzi Ng'ambwa lakini si katika suala zima la kufuatilia kilimo cha mwani. Kwa maana hiyo, kilimo cha mwani na masuala ya uendelezaji wake kinatekelezwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu suala la miundombinu iliopo pale ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, ndiyo yenye jukumu la kushughulikia masuala hayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hali hii ya ukulima wa mwani umeshamiri sana hapa nchini. Vile vile wapo baadhi ya watu ambao tayari wameshapata elimu ya ufungaji wa kamba katika mawe.

Je, Mhe. Waziri utafanya jitihada zaidi za kuwatembelea wananchi ambao hawajapata hii elimu, ili na wao waelimike kufunga kamba kwenye mawe?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli nimejibu kwenye swali langu mama kwamba majaribio yamefanyika katika maeneo ya Uzi Ng'ambwa, na maeneo mengine ya kuweza kutumia *rubber band* na mawe katika ukulima wa mwani badala ya kutumia vijiti, ambapo itaweza kuepusha kwa kiasi kikubwa kukatwa kwa miti hiyo.

Mhe. Spika, naomba nimuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba jitihada za pamoja kati ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na Wizara ya Kilimo na Maliasili zinaendelea katika jitihada za kuwaelimisha wananchi juu ya upandaji mwani kwa njia hiyo, ili kuweza kupata kwanza ule mwani ambao ni bora kwa kuweza kupata bei nzuri pamoja na kuepusha ukataji wa miti.

Nam. 154

Kuwepo kwa Sarafu ya Zanzibar

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Tokea kuvunjika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1966, Zanzibar ambayo ilikuwa ni miongoni mwa nchi nne zilizokuwa zikitumia sarafu ya shilingi ya Afrika Mashariki, iliingizwa katika matumizi ya sarafu mpya ya shilingi ya Tanzania ambayo inaendelea kutumika hadi leo chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*). Sarafu hiyo inaendelea kushuka thamani siku hadi siku kutokana na sababu zinazoihusu zaidi Tanzania Bara kuliko Zanzibar.

(a) Ni athari zipi za kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania zinazoikumba Zanzibar na kuathiri uchumi wake na maisha ya wananchi wake?

(b) Je, iwapo itaamua, Zanzibar inao uwezo wa kiuchumi wa kuanzisha, kuihudumia na kuisimamia sarafu yake wenyewe?

(c) Ni zipi zinaweza kuwa faida kwa Zanzibar kuwa na sarafu yake yenyewe?

(d) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni kwamba wakati umefika wa kuanzisha sarafu yake yenyewe, ili iweze kuusimamia ipasavyo uchumi wake kwa faida na maslahi ya watu wa Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali Nam. 154 la Mhe. Mwakilishi lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kuna athari na faida kwa uchumi na wananchi wa Zanzibar. Athari za kushuka kwa thamani ni kama ifuatavyo:-

(i) Bei za bidhaa zitapanda kwa vile Zanzibar inaagiza bidhaa na hasa za chakula kwa kiwango kikubwa kutoka nje ya nchi.

(ii) Baadhi ya wafanyabiashara wataondoka katika biashara wanazozifanya, kwa sababu mitaji yao itapungua hasa kwa wale wanaonunua fedha za kigeni kwa ajili ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje. Hivyo, kupelekea kuwa na wafanyabiashara wachache.

(iii) Kuna uwezekano mkubwa kwa mapato ya serikali yanayotokana na Kodi ya Forodha kupungua.

Mhe. Spika, kwa upande wa faida ni kama ifuatavyo:-

(i) Wafanyabiashara na wakulima wanaozalisha bidhaa zao kwa wingi na hatimaye kuuza nje ya nchi, watafaidika pale wanapouza fedha zao za kigeni na kupata shilingi za Tanzania.

(ii) Kuna uwezekano mkubwa wa kupata wageni kwa hoteli ambazo zitatoza ada kwa shilingi za Kitanzania.

(b) Mhe. Spika, kiuchumi Zanzibar inao uwezo mzuri wa kuanzisha, kuihudumia na kuisimamia sarafu yake. Hata hivyo, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, suala la sarafu ni la Muungano. Kwa mantiki hiyo Kikatiba hatuwezi kuanzisha hata kama tunao uwezo wa kiuchumi.

(c) Mhe. Spika, faida kubwa itakayopatikana kwa Zanzibar kuwa na sarafu yake ni kuwa na uwezo wa kupanga Sera zake za Fedha, jambo ambalo litasaidia sana katika kuchapisha, kudhibiti, kushuka kwa sarafu pamoja na ujazo wa fedha katika soko.

(d) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu (b) la suala hili, kwamba suala la kuanzisha sarafu ni la Kikatiba. Hata hivyo, Jumuia ya Afrika ya Mashariki nayo inazungumzia suala zima la kuwa na sarafu ya pamoja. Kwa maana hiyo, serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kuanzisha sarafu yake wakati nchi zetu za Afrika ya Mashariki zinajenga uwezo wa kuwa na sarafu ya Pamoja ambayo yenye nguvu zaidi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, niruhusu nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ya swali langu, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa sababu katika majibu yake amekiri kwamba hili ni suala la Kikatiba. Kwa hivyo, uwezo wa Zanzibar kuamua kuanzisha sarafu yake pengine itategemea maamuzi ya wananchi kupitia utaratibu wa sasa kwa mjadala wa Katiba unaendelea katika nchi yetu. Lakini katika majibu yake amesema nchi za Afrika ya Mashariki zinafikiria hivi sasa kuanzisha sarafu ya pamoja.

Swali langu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kwa sababu ya uzoefu wa nchi za wengine kwa mfano Umoja wa Ulaya walioanzisha Sarafu ya *Euro* miongoni mwao wameleta mtikisiko mkubwa kwao na sarafu ile ilipokuwa imeyumba kutokana na uchumi wa nchi dhaifu miongoni mwa nchi hizo hupelekea kuathiri hata zile nchi ambazo chumi zake ni imari.

Je, haoni kwamba suala la kuanzisha Sarafu ya Pamoja Afrika ya Mashariki kipindi hichi, ukizingatia chumi za nchi zetu zilivyo, inaweza kuwa ni hasara zaidi kwa Zanzibar kuliko faida?

(b) Iwapo Zanzibar itaamua hatimae kwa maamuzi ya wananchi kupitia majadala wa Katiba kuanzisha sarafu yake wenyewe. Kwa kuwa kumekuwa na utaratibu kwa baadhi ya nchi kuifungamanisha sarafu yake na baadhi ya sarafu za kigeni ikiwa ndio kiungo cha kupima uzito wake.

Je, iwapo Zanzibar wananchi wataamua kuanzisha sarafu yake katika mjadala huu wa Katiba ni sarafu ipi katika Sarafu kubwa duniani. Kwa mfano, *Pound* ya Kiingereza, *Dollar* ya Kimarekani au *Euro* ambayo Mhe. Waziri nadhani inaweza kuwa nzuri kufungamanisha na itakayokuwa sarafu ya Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka niseme katika swali lake la nyongeza nakubaliana nalo, kwa maana hata ukichunguza mwenendo pamoja na mchakato mzima wa uundwaji wa Sarafu ya Pamoja katika Jumuia ya Afrika Mashariki unakwenda taratibu, hasa kwa kuzingatia athari zinazotokea katika Jumuia ya Ulaya, na hasa kwa kuzingatia kwamba katika nchi zetu tano za Jumuia ya Afrika Mashariki tunazo chumi zinazotafautiana, hili nakubalina nalo kabisa. Vile vile nawaomba sana ndugu zangu wa Afrika Mashariki kwamba twende nalo taratibu mpaka tufikie muafaka.

Swali lake la pili ananiuliza mimi sarafu ipi nzuri, labda niseme tu, kwamba sarafu nzuri ni ile yenye uzito mkubwa sana kuliko sarafu nyengine. Kwa maana hiyo, ningeweza kusema *Dinari* ni bora zaidi ukaifunganisha na sarafu ya Tanzania, kwa sababu *Dinari* ya Kuwait ni nzito kuliko hata *Pound*, lakini *Dinari* sio sarafu inayojulikana sana kimataifa ukilinganisha na sarafu kama *Euro*, *Dollar* na *Pound*. Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, basi naweza kumwambia kwamba tuifunganishe na Sarafu ya *Pound*. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nielimishe kidogo sana kama ifuatavyo. Mhe. Waziri amekiri kwamba *Dinari* ndio sarafu kubwa zaidi katika ulimwengu, lakini sio maarufu katika medali ya fedha, pia amesema kwamba *Pound* na *Dollar* ndizo zinazotamba duniani.

Hivi haoni kwamba kuiachia *Dinari* kutokubalika katika ulimwengu wa fedha wakati ndio kubwa zaidi na huo si utawala mambo leo wa nchi za Magharibi? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, katika kupanga ni sarafu ipi maarufu duniani kuna vyombo vya Kimataifa na hasa Shirika la Fedha za Dunia *IMF*. Kwa kweli mimi sijui kama kutoipa *Dinari* ni kuendeleza hivyo anavyosema.

Lakini nadhani kutokana na hali ilivyo hasa ya kimataita, ndio kwa maana hizi sarafu nyengine. Kwa mfano, Sarafu ya *Dinari*, Sarafu ya *Riyal* ya Oman nazo pia ziko *strong* ukilinganisha na *Pound* na *still* hazitambuliki sana kimataifa kama hizi nyengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kabla ya kuomba kujibiwa swali langu naomba nimshukuru na kumsifu sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa majibu yake jinsi yanavyopandisha hadhi Baraza hili na yalivyokuwa ya ufasaha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo naomba swali langu Nam. 155 lijibiwe kwa ufasaha kama lililopita. Mhe. Spika, ahsante sana.

Nam. 155

Misamaha ya Kodi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

(a) Ni mamlaka ngapi na zipi zimepewa uwezo chini ya Sheria za Zanzibar kutoa misamaha ya kodi na ushuru?

(b) Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ni misamaha mingapi ya kodi na Ushuru imetolewa, ilikuwa na thamani gani na ni nani walionufaika?

(c) Idadi na thamani ya misamaha hiyo ya kodi na ushuru kwa mwaka wa fedha 2011/2012 inalingana na kutofautiana vipi na misamaha kama hiyo kwa mwaka 2010/2011?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza na mimi nipokee shukurani za Mhe. Mwakilishi wangu. *(Makofi)*
Pili nataka nijibu swali lake Nam. 155 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar mamlaka iliyopewa uwezo wa kutoa misamaha ya kodi ya ushuru ni moja tu, nayo ni Wizara inayosimamia masuala ya fedha.

(b) Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya misamaha 234 ya kodi na ushuru imetolewa na ilikuwa na thamani ya shilingi Bilioni 22.01. Walionufaika na misamaha hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Wawekezaji walinufaika kwa asilimia 51.
(ii) Taasisi za Serikali walinufaika kwa asilimia 17.
(iii) Kampuni na watu binafsi walinufaika kwa asilimia 5.
(iv) Miradi ya Washirika wa Maendeleo ilinufaika kwa asilimia 6.
(v) Mashirika ya Umma yalinufaika kwa asilimia 20 na
(vi) Taasisi za Dini zilinufaika kwa asilimia 1.

(c) Mhe. Spika, misamaha ya kodi iliyotolewa mwaka 2010/2011 ilikuwa ni 220 na ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 18.39.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza. Mhe. Spika, nakumbuka Mhe.Waziri aliwahi kutuambia katika kikao cha bajeti cha mwaka jana, kwamba moja ya mamlaka ambazo zimekuwa zikitoa misamaha ya kodi Zanzibar ni Mamlaka ya Kusimamia Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*).

Baadhi ya Wajumbe tulieleza wasi wasi wetu na kutaka hatua zichukuliwe kufanywe marekebisho, ili mamlaka hiyo iondolewe uwezo huo na ubakie kwa Waziri anayesimamia masuala ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tu kwa Zanzibar.

Je, hatua ya kufanyiwa marekebisho sheria hiyo yamefikia wapi, ili kukabidhi mamlaka haya kwa mamlaka moja tu katika Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Sheria ya *ZIPA,* mchakato wa kuirekebisha *the first draft* iko tayari na tunachokisubiri hivi sasa ni kuipeleka kwa Makatibu Wakuu, halafu kuyapeleka marekebisho katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi na hatimae marekebisho hayo kuletwa hapa.

Hata hivyo, tumeona kwamba ile Sheria Mama ya Fedha inampa mamlaka Waziri anayesimamia masuala ya fedha. Kwa hivyo, *ZIPA* haikupaswa kuwa na mamlaka hayo, hivyo mamlaka tumeyarudisha kwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri sana tena ya fasaha ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa moja katika malengo ya kutoa misamaha ya kodi hasa kwa wawekezaji ni kukuza uchumi wetu, ijapokuwa Mhe. Waziri amesema ametumia *almost* 51 *percentage* ya 20 bilioni, nadhani kama itakuwa ni shilingi bilioni 10 na kidogo kwa ajili ya kuwasamehe hawa wawekezaji.

Je, fedha hizo zimezalisha kiasi gani katika mwaka huu, ili kuongeza uchumi wetu?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ni kweli asilimia 51 ya misamaha hiyo imekwenda kwa wawekezaji. Kwa hivyo, anachotaka kujua Mhe. Mjumbe ni takwimu, kilichozalishwa naomba nije nimjibu kwa maandishi, kwa sababu takwimu hizo sina hivi sasa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu swali la msingi amesema kwamba ni Wizara ya Fedha pekee ndio imepewa mamlaka kisheria ya kutoa misamaha ya kodi.

Je, ni kwa nini Wizara inayoshughulika na masuala ya ardhi huwa inatoa misamaha ya kodi ya ardhi na mamlaka hiyo imepewa na sheria ipi?

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, swali la msingi nililoulizwa ni kuhusu kodi na ushuru, Waziri wa Ardhi anasamehe ada za ardhi, tena anasamehe ada kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi na uwezo huo anao.

Hata hivyo, tunayo maelekezo kupitia Baraza lako kwamba hizi kodi, ushuru pamoja na ada zote ziwe zinasamehewa na Mhe. Waziri wa Fedha na hatua hizo tunaanza kuziangalia kupitia hatua mbali mbali. *(Makofi)*

Nam. 110

Utengenezaji wa Barabara ya Kijini na Mbuyutende

Mhe. Abdi Mossi Kombo – Aliuliza:-

Tunampongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kutembelea kijiji cha Kijini na kuona tatizo la barabara. Aidha tunawashukuru viongozi na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu kwa kuitia jasi njia hiyo.

Je, ni lini serikali itafikiria kuiweka kwenye kiwango cha lami.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 110 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, barabara ya Keshange hadi Kijini ni miongoni mwa barabara zitakazofanyiwa upembuzi yakinifu na sadifu *(feasibility study and detailed engineering design)* kwa kiwango cha lami, ambapo jumla ya kilomita 48.7 zimepangwa kufanyiwa upembuzi huo.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba hatua ya mwanzo ya kutafuta Kampuni ya Wahandisi Washauri (*short list*) imekamilika na kuwasilishwa kwa mfadhili wa mradi huo (ADB), na amekubali kuendelea na hatua ya pili ya kumtafuta Muhandisi mshauri mmoja atakayezifanya kazi hizo ambazo zinajumuisha barabara zifuatazo:-

- Barabara ya Matemwe (Kiashange) – Muyuni yenye urefu wa (6.5)
- Barabara ya Njia nne – Umbuji – Uroa yenye urefu wa (11km)
- Barabara ya Mkwajuni - Kijini yenye urefu wa (5.5 km)
- Barabara ya Kichewele – Pangani yenye urefu wa (4km)
- Jozani – Ukongoroni - Charawe hadi Bwejuu yenye urefu wa (15km)
- Barabara ya Fuoni – Kombeni yenye urefu wa (6.7 km)

Ujenzi wa barabara hizo ni kwa kiwango cha lami, na utaanza mara moja baada ya kukamilisha utaratibu tulioueleza na upatikanaji wa fedha kutoka kwa wahisani wetu utakapokamilika.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza.
Kwa vile barabara ya Kijini ni ya muda mrefu sana haijafikiriwa na Serikali, je, utakubaliana na mimi Mhe. Naibu Waziri kwamba kuchelewa kwa barabara hii kwa muda mrefu ndio kuchelewa kwa maendeleo ya watu wa Kijini.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Spika, kwa sehemu moja nakubaliana naye kwamba mimi mwenyewe naamini uwepo wa barabara nzuri ni sehemu ya chachu ya kuhimiza maendeleo. Kwa hivyo kama barabara ilichelewa ilikuwa na ni sehemu ambayo ilidumaza maendeleo. Kwa muda huu naamini kepten

atakubaliana nami kwamba barabara itakuwa katika hatua nzuri. Tayari nimeshaimarisha ile chachu na hamasa ya maendeleo kwa wananchi wa Kijini. Namuomba aendelee kufanya subira na tutahakikisha barabara ile inajengwa kwa kiwango cha lami, ili kuhimiza na kutisha shangwe kwa hao wananchi wanaohitaji hayo maendeleo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.
Katika majibu yake alikuwa anasema kwamba wanatafuta mhandisi mshauri. Mimi nilikuwa nataka kujua hii Wizara ya Miundombinu haina wahandisi wanaweza kufanya hiyo kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inayo wataalamu na wafanyakazi hao wanafanya kazi nyingi. Utaratibu wetu inapokuja miradi mikubwa kama hii huwa tunajaribu kufanya kwa kushauriana na wenzetu hawa wahisani au washirika wa maendeleo kwa kuona kwamba kazi ile inafanywa kwa kutanua wigo na kwa uwazi zaidi. Hivyo tunalazimika kutafuta wakandarasi wengine au wataalamu wengine, ili kufanya kazi hii kiufanisi na kwa uwazi, ili kuwajengea imani wenzetu wale washirika wa maendeleo.

Namuomba Mhe. Mwakilishi atambue tu kwamba tunapofanya kazi hizo kwa kufungua milango ya wahandisi wa nje, haimaanishi kwamba hatuna wahandisi wa ndani. Wahandisi wa ndani tunao na tuna kitengo kizima ambacho na hicho kinakuwa kinashirikiana na wahandisi wengine wa nje. Tunacho kitengo cha KODAK, ambacho ni miongoni mwa hawa ambao wanakuwa wanashirikiana na kufanya tathmini ya kazi za uchambuzi zinazofanywa na hawa wahandisi wa nje.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza niipongeze Wizara ya Miundombinu kwa kuwapelekea kifusi ili kuweza kuwajengea njia ile.

Lakini Mhe. Naibu Waziri, majibu yake bado yanatukatisha tama, ndio kwanza anatujibu kuna watu washauriane miradi. Lakini je, hebu Mhe. Waziri atuhakikishie hasa njia ile katika bajeti hii au mwaka huu mko tayari kuitengeneza njia ile kiwango cha lami. Wahakikishie wananchi wa Kijini na Baraza lako hili tukufu Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia kwamba katika mipango yetu katika Bajeti yetu ya mwaka 2012/2013 Bararaba hii haimo katika ujenzi wa lami. Tutaendelea na utaratibu wetu na mchakato wetu wa kufanya *study*, na pale itakapokamilisha utaratibu huu kwa kupitia wenzetu wa ADB basi tutakuja na taarifa njema.

Nam. 144

Udhamini wa Uhakika wa Zanzibar Heroes

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-
Kwa kuwa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) ina udhamini wa uhakika lakini kwa timu yetu ya Taifa ya Zanzibar *(Zanzibar Heroes)* haina udhamini.

(a) Je, Wizara kwa kushirikiana na BTMZ na ZFA wamechukua hatua gani kupata mdhamini kwa *Zanzibar Heroes.*

(b) Ni sababu gani zinazofanya kukosa udhamini kwa timu yetu ya Zanzibar Heroues
(c) Kukosa kupata udhamini kwa timu yetu hii sio sawa na kuitelekeza na kuiacha ikishiriki mashindano mbali mbali yakiwemo ya Cecafa *(Challenge Cup)* kama watoto yatima.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 144 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli timu ya Taifa ya soka "*Zanzibar Heroes*" haina mdhamini. Kwa hivi sasa, timu hiyo inapokuwa na mashindano ya kimataifa au kupiga kambi hutegemea sana ruzuku kutoka Baraza la Taifa la Michezo na baadhi ya wahisani.

Mhe. Spika, ili kuifanya timu hiyo iwe na wadhamini Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Michezo inaendelea kuwasiliana na Kampuni mbali mbali zilizopo hapa nchini, pamoja na kuandaa maandiko ya mradi (*proposal*) ili kuzishawishi kukubali udhamini. Hata hivyo juhudi hizo bado zinaendelea, lakini harakati bado zinaendelea.

(b) Sababu kubwa zinazopelekea timu yetu kukosa udhamini huenda zinatokana na timu hiyo kutokuwa na mashindano mengi yanayoweza kuitangaza Kampuni inayodhamini kiasi cha kuweza kunufaika na matangazo hayo. Hadi hivi sasa timu yetu ya taifa ni mashindano ya *Challenge* tu ndio inayoshirikishwa kila mwaka, ambapo timu hadi kufikia fainali katika michuano hiyo inapaswa kushiriki si zaidi ya michezo sita (6). Mashindano mengine inayoshiriki ni kombe la *VIVA World Cup* ambalo hushindaniwa kila baada ya miaka minne. Hivyo, Kampuni nyingi huona ni hasara kutumia mamilioni ya fedha kuihudumia timu ambayo inavaa jezi ya kuitangaza kampuni hiyo katika michezo sita (6) kwa mwaka.

Katika kukabiliana na kasoro hiyo, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Michezo, imekusudia kuandaa utaratibu maalum wa kuitafutia timu hiyo michezo mbali mbali ya kirafiki ya kimataifa, kwa lengo la kuipa uzoefu na pia kuwajenga imani wafadhili ili waweze kujitokeza kuifadhili timu hiyo.

(c) Kasoro za kupata udhamini kwa timu yetu hakuna maana hata kidogo kwamba timu hiyo inatelekezwa na kuiacha ishiriki mashindano mbali mbali kama mtoto yatima. Kwani Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo muda wote timu hiyo inapokuwa na mashindano ya kimataifa juhudi huchukuliwa kuisimamia timu hiyo. Jambo muhimu chama kinachosimamia soko kuwa na kalenda inayofahamika mapema, ili kusaidia kuwekewa bajeti maalum ya kuiwezesha timu hiyo kushiriki katika mashindano hayo baada ya kuleta ratiba ya kushtukizia.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b)

Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Waziri amekiri kwamba timu hii ya Taifa ya Zanzibar Heroes, huwa inashiriki shindano moja tu kwa kila mwaka, na ndio sababu kuu ya kukosa udhamini wa kampuni mbali mbali. Lakini hivi juzi tu Mhe. Spika, timu hii ilishiriki katika mashindano ya *VIVA World Cup* na ilifanikiwa kupata nafasi ya tatu.

(a) Kwa kuwa timu hii ni timu ya Wazanzibari wote na Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Sekta ya utalii ni sekta muhimu sana katika kuchangia maendeleo yetu ya mambo mbalimbali. Je, Wizara haioni kwamba kuwashawishi na kuwashajihisha kamapuni za hoteli za Kitalii kuweza kuichangia timu yetu hii ya Taifa katika kuleta maendeleo ya mchezo wa mpira wa miguu hapa Zanzibar.

(b) Ni sababu zipi zinazofanya Kampuni ya Zantel kuondoa udhamini katika maendeleo ya Soka ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru sana Mhe. Spika,

(a) Ni kweli kwamba sekta ya utalii ikishirikishwa vizuri inaweza kuwa ni chanzo muhimu cha kusaidia udhamini katika michezo mbali mbali hapa Zanzibar. Hilo tumelianza na kwa kweli ushauri wake labda alisikia kwamba tumeanza na tunatarajia kupata mafanikio mazuri. Ni kweli tumeanza na tutafanikiwa.

(b) Sababu ambazo walizofanya Zantel wajitoe ni kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri katika jibu mama kwamba kampuni nyingi kwa sababu timu yetu inacheza michezo kidogo haioni muhimu wa kuendelea kutudhamini kwa sababu kwa mwaka tunacheza michezo sita (6) tu. Wao wanafanya vile kibiashara, kwa hiyo wanaona kibiashara hailipi, lakini kwa sababu tuna mipango mingi ya kuifanya timu yetu icheze michezo mingi zaidi ili wananchi na wapenzi wa michezo waweze kuiona. Nadhani kwamba utaratibu huu

mpya ambao tumeuanza utawezesha sasa kuzishawishi tena kampuni kama ya Zantel na nyenginezo kuendelea kutudhamini katika michezo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri sambamba na Waziri wake. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri kakiri kwamba kurudi nyuma kwa wadhamini ni kutokana na uchache wa michezo inayochezwa na timu yetu ya *Zanzibar Heroes* kwa mwaka. Na kwa kuwa siri nyengine ya ushindi wa timu zetu hizi za Taifa ni pamoja na kuwa na benchi la ufundi ambalo linaongozwa na kocha aliyebobea katika mambo ya *International Soccer* pamoja na *physical education*. Kwa kuwa wenzetu Tanzania Bara tu hapo wameajiri Makocha wa kimataifa kusimamia mambo ya Soka akiwemo Maxio Maximo na huyu mwengine aliyekuja juzi.

Je, ni lini Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itaweka mbele kipaumbele cha soka kwa kuweza kutuletea kocha wa kimataifa kama vile Maximo na huyu mwengine.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli nchi nyengine zinaona kwamba kuwaajiri Makocha kutoka nchi zenye majina makubwa ya michezo kama vile Brazil, Argentina na nchi nyengine ndio kuongeza kiwango cha mpira wa miguu katika nchi zao.

Ningemuomba aangalie hizo nchi ambazo zimeajiri makocha hao ni kiwango gani cha ushindi zimerudi katika nchi hizo. Sisi tunaona kwamba Makocha Wazalendo wakipewa mafunzo vizuri sana, basi wanaweza kuzinoa timu za nchi zao na zikaleta ushindi katika nchi. Sisi vijana wa Zanzibar Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waamini sana Wazanzibari kwamba wana uwezo na vipaji vizuri vya kufundisha mpira wa miguu katika nchi yetu na ikaleta tija kubwa. Kwa hivyo bado sisi Wazanzibari wakiwezeshwa wanaweza, na ndio maana vijana wetu, makocha wetu tunawaamini na tutawawezesha ili walete ushindi katika nchi yetu Mhe. Spika.

Nam. 180

Madaktari Wanaoingia Zamu za Usiku Kulala Hospitali

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Madaktari wanaokuwa zamu nyakati za usiku hawalali hospitali, na sababu kubwa inayosemekana ni kutokana na kutolipwa inavyostahiki pamoja na kutowepo kwa mazingira bora ya kulala hospitalini hapo. Kwa kuwa Serikali itaanza kuwalipa Madaktari hao katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Je, Wizara imejipanga vipi katika kukabiliana na suala hilo ili kuepusha Madaktari hao kulala majumbani mwao na kuenda kazini pale wanapohitajika.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 180 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kipindi chote madaktari wanakuwa kazini kuendelea na kazi zao kama kawaida. Kwa kawaida daktari wa mwanzo ambaye kwa lugha yao wanaita (*First on call*) anatakiwa awepo siku zamu yake muda wote wa zamu yake. Katika Idara zetu nne zinazostahiki kuwa na madaktari wa aina hizo, kila idara ina chumba kwa ajili ya daktari wa ina hiyo. Lakini daktari wa mwanzo anaposhindwa hutakiwa kumwita bingwa aliyemzidi ambaye anaitwa *Second on call*. Huyu huitwa na yule wa mwanzo na kuja kutoa huduma inayostahiki na halafu hurudi nyumbani kama kawaida yake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kusikitisha sana ya Mhe. Waziri, Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio hospitali tegemeo kwa wananchi wa Unguja na Pemba. Juzi tarehe 28 nimeshuhudia mimi mwenyewe kwamba hospitali daktari hapana kwa upande wa X-ray na wananchi wakaondoka na mgojwa wao wakampeleka Hospitali ya Al-Rahma.

(a) Je, ni sababu gani ya kutowepo daktari pale.

(b) Ni lini mtaweka usafiri panapotokea dharura daktari akachukuliwe na pawe na gari ya kudumu kwenda kuchukuliwa daktari panapotokea kesi kama hizo hasa wakati wa usiku. Kama hapana uwezo japo vespa iwekwe Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, siku ya tarehe 28 alinipigia simu saa 3:00 za usiku na aliponipigia simu alikuwa yeye na daktari wa zamu pale, akaniuliza kwamba mashine zimeharibika? Nikamwambia nipe simu ya huyo daktari aliyekuwepo. Akasema kweli mashine zimeharibika lakini ni kawaida Mheshimiwa simu kuharibika. Kwa taarifa yake lile dudu kule Muhimbili liko miezi 9 sasa halijatengenea, seuze *X-ray* zetu. Ziliharibika lakini asubuhi zikatengenezwa. Kinachoshangaza kwamba pale tunazo *X-ray* tatu, kuna *X-ray* nyengine ilikuwa nzima kule na ingeweza kutoa huduma.
Kwa hivyo mara nyengine inategemea ni nani yupo kwenye zamu kuliko ile huduma iliyokuwepo. Ingeweza kushughulikiwa huduma hiyo anayosema Mhe. Jaku bila ya matatizo. Maana kuna X-ray nyengine mpya na ilikuwa nzima katika idara nyengine wangeweza wakapata huduma hizo. Mara nyengine hamu ya mwenye kuumiwa hatuwezi kui- *control*.

Usafiri ni kweli kumekuwa na tatizo la usafiri, lakini tunahakikisha daktari akitakiwa anakwenda kuchukuliwa, huenda akichukuliwa kwa chombo cha dharura *ambulance* anatiwa daktari inapigwa king'ora, kwa hivyo dakika tano kumbe amefika hospitali. Kwa hivyo huduma ya daktari kufika hospitali ipo na inakuwa ni ile inayohakikisha daktari anafika.

Hata hivyo kama ni kuwa na gari maalum basi tutalizingatia hilo katika bajeti yetu ya mwakani.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nakushukuru sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Afya yanayokatisha tama, naomba kumuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kuwa hata hiyo *ambulance* ya usiku wananchi wanachangia mafuta pale.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hakuna jibu la kukatisha tama, tunajibu na tunaendelea kuishi kwa sababu ya kutatua matatizo. Gari ambazo huchangia mafuta ni zile zilizokuwepo Vijijini. Hilo ni kutokana na ufinyu wa bajeti na kutokana na masafa ya vijijini mpaka mjini ni mbali. Mnazi Mmoja huhudumiwa na Idara ya Mnazi Mmoja kumchukua daktari. Kama Waziri sijawahi kuambiwa kama inafika hatua mgonjwa wa Mnazi Mmoja anachangia gari ya *ambulance*.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Uzi/Ng'wambwa ni kisiwa, ni mda mrefu hivi sasa hakuna daktari Mkuu wa hospitali hiyo. Ni lini tutapata daktari Mkuu wa hospitali hiyo wa kulala, na nyumba hivi sasa zipo lakini hakuna daktari wa kulala katika sehemu hiyo. Kuna upungufu wa madaktari katika sehemu hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, juzi tumepata vijana wetu wasiopungua 176 waliomaliza Chuo cha Afya, na nina Kamati maalum ambayo nimeunda ninaita *deployment committee* kuhakikisha kwamba ugawaji wa madaktari hawa unategemea na umuhimu wa pale panapotakiwa. Ninachoamini kwamba suala hilo litamalizika karibuni.

Nam. 191

Kukosekana kwa Maji Baadhi ya Shehia za Jimbo la Muyuni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Takriban ni miaka isiyopungua 10 wananchi wa Jimbo la Muyuni zikiwemo baadhi ya Shehia zake kama Muungoni, Muyuni (Kipanga), Pete kuwa na kilimo cha ukosefu wa maji pamoja na wananchi hao kujitolea kwa hali na mali kama Mamlaka ya Maji (ZAWA) wanavyozijua jitihada zao.

(a) Je, Mhe. Waziri tatizo hili la Wananchi wa Pete unalifahamu na ni lini utalipatia ufumbuzi.

(b) Kwa kuwa Wananchi wa maeneo hayo shughuli zao kubwa ni kilimo na uvuvi, huoni kukosekana kwa maji kunarudisha nyuma juhudi zao za uzalishaji kutokana na muda mwingi kuutumia kutafuta maji badala ya kufanya shughuil zao hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 191, lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza naomba nitoe ufafanuzi juu ya hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi wa Jimbo la Muyuni wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia kianzio cha maji kutoka Unguja Ukuu na Pete, hali ambayo miaka ya nyuma huduma hiyo haikuwa nzuri kiasi. Hata hivyo kuanzia mwaka 2010/2011 tayari wananchi hao wanaendelea kupata huduma hiyo.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya maji inaendelea na juhudi mbali mbali za kuwapatia wananchi wa Mijini na Vijijini huduma ya maji safi na salama ikiwemo kijiji cha Pete. Miongoni mwa juhudi hizo ni zile za karibuni zilizofanywa kwa kushirikiana na Mhe. Mwakilishi wa Muyuni za kuyatoa maji kutoka Unguja Ukuu hadi Pete. Huduma hiyo sasa hivi inapatikana kiasi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu aliyojibu Mhe. Naibu Waziri hayafanani na swali la msingi. Je, utakuwa tayari baada ya kumaliza kikao hichi nikenda nikakuonesha maeneo ambayo hayapatikani maji kwa muda mrefu. Na utachukua hatua gani kuwaondolea tatizo hilo wakati wananchi wa jimbo la Muyuni wanatusikiliza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwanza kama kuna kasoro ndogo ndogo hizi ni kasoro za kawaida. Sehemu yoyote ile ambayo tunayopeleka mitandao yetu ya maji basi huwa unatokea ukosefu wa maji siku moja au siku mbili. Lakini niseme huduma hiyo sasa hivi inapatikana kwa kiasi. Kama Naibu Waziri basi niko tayari kushirikiana naye na kwenda naye katika maeneo hayo tukaangalia panapo matatizo hayo na kuyafanyia marekebisho.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri amekuwa akijibu maswali kwamba maeneo mengi ya majimbo ya Unguja na Pemba yana maji. Amewahi kujibu hapa kwamba jimbo la Matemwe halina tatizo la maji na ikasababisha wananchi wa Matemwe wakamlalamikia sana Mwakilishi wao na kumlaumu. Leo unatwambia kwamba jimbo la Muyuni kuna maji maeneo ya Pete, wakati Mwakilishi mwenyewe ndio anajua kwamba hakuna maji.

Hivyo naomba kujua majibu yako unayoyajibu unayafanyia utafiti au unakusudia kuwaondosha njiani wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, mara nyingi sana basi ninapotoa majibu na mimi mwenyewe huwa nafatilia. Ninachokizungumza ni sahihi. Suala la Matemwe la tatizo la maji kama nilivyojibu kwamba tumefunga pampu mpya katika kisima cha Matemwe, na kutofika baadhi ya Vijiji hayo ni matatizo ya kawaida. Lakini mwenyewe huwa nafatilia ipasavyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali alisema kwamba maeneo mengi anahakikisha kwamba yanapata maji. Lakini kuna maeneo ambayo yana matatizo na yalikuwa yakipata maji, kwa mfano kama hoteli tuliyokuwa tunakwenda tukifanya semina Coconut Hotel wana tatizo la maji na ni sehemu ambayo inazalisha katika nchi yetu kwa sababu ni sehemu a kitalii na karibu tunaingia katika season ya kitalii na yule bwana ameshalalamika kwamba maji yake ni ya chumvi lakini alikuwa akipata na hivi sasa hapati. Je, kuna hatua gain itakayochukuliwa ili apate maji?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Mhe. Spika, kwanza nakiri kwamba maeneo aliyozungumza kuwa sasa hivi yana matatizo ya maji, lakini vile vile ningeomba wananchi nao waelewe kwamba linapotokea tatizo hususan kwenye kisima cha maji kama *pump* au chengine basi watupe ripoti, bado hatujakuwa na mitambo ambayo inatuonesha kuwa baada tu ya kutokea lile tokeo na sisi wizara tukapata taarifa isipokuwa taarifa

zitoke kwa wananchi wenyewe. Baadhi ya maeneo kweli yanakuwa na matatizo kama hayo lakini tunakosa kupata taarifa kwa muda muafaka ndio jambo linalosababisha uchelewaji wa kufanyiwa matengenezo ndani ya maeneo hayo.

Kwa hivyo, nimhakikishie Mhe. Mwakilishi suala hilo tutalishughulikia na hapo penye matatizo ya maji tutapopata taarifa basi sisi tutajipanga na tutakwenda kuyashughulikia matatizo hayo ili wananchi watokane na usumbufu huo.

Nam. 105

Ufugaji Wa Samaki Kisiwani Pemba

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Aliuliza:-

Kwa kuwa ufugaji wa samaki katika mabwawa kisiwani Pemba hivi sasa umeshamiri kutokana na wananchi wengi kuitikia wito na kuhamasika katika kujikwamua na umaskini, na kwa vile yapo baadhi ya mabwawa yana uwezo wa kuzalisha samaki wengi, lakini pia yapo baadhi ya mabwawa huhitaji kuongezwa ukubwa na hupelekea kukatwa mikoko kwa ajili hiyo.

Je, Mhe. Waziri kuna elimu yoyote waliyopewa wananchi hawa ili kuepukana na uharibifu wa mazingira.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Nashukuru Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ufugaji wa samaki katika mabwawa kisiwani Pemba hivi sasa umeshamiri kutokana na wananchi wengi kuitikia wito na kuhamasika katika kujikwamua na umasikini. Aidha, ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini ukifanyika kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na wataalam unapelekea ufugaji wenye tija kwa mwananchi bila ya kuharibu mazingira.

Mhe. Spika, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 105 kama ifuatavyo:

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Mazao ya Baharini imekua ikitoa taaluma na inaendelea kutoa taaluma hiyo ya kutosha juu ya uanzishaji na ujengaji wa mabwawa ndani ya maeneo yaliyowazi (majangwa) katika mikoko pamoja na utunzaji au upandaji wa mikoko. Pia idara imeanzisha utaratibu maalum wa ukaguzi kwa maeneo yanayotakiwa kuanzishwa au kuendeleza ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini ili kushauri wananchi jinsi gani ya kuanzisha au kuendeleza ufugaji bila ya kukata mikoko au kufanya uharibifu wowote wa mazingira.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri atakubaliana nami kwamba yapo mabwawa kama vile Shamiani - Mwambe, Chambani, Kiwani, Kangani, Mkoani na Makombeni. Mabwawa haya yote yanahitaji kupatiwa msukumo ili wajiendeleze katika kufanya shughuli zao. Kwa mfano, bwawa la Kangani ambalo limeanzishwa hivi karibuni nalo linahitaji elimu ya ufugaji kwa wakulima hao.

Je, Mhe. Waziri unawaambia nini wananchi hao ili wakae na matumaini kutoka kwako ahsante.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli nakubaliana naye kwamba kunahitajika nguvu za ziada na hilo ndio moja katika lengo letu kuwashajihisha wananchi kuanzisha mabwawa ya kufugia samaki na huwa tunatoa taaluma hizo kupitia kwa maafisa wetu wataalamu katika mawilaya. Lakini vile vile penye uwezo huwa tunatoa vifaa au hata fedha na tumefanya hivyo katika mabwawa kadhaa na hususan kwa mule nilimotembelea kama Wambaa, Pujini na kadhalika. Kwa hivyo, namuahidi kwamba tutapomaliza bajeti tunacho vile vile kifungu cha kujaribu kusaidia wananchi wanaotaka kuanzisha ufugaji wa samaki.

Mhe. Rufai Said Rifai: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa serikali inagharamika kwa kupeleka vijana wengi na baadhi ya watendaji wako nchini China kupata mafunzo ya ufugaji wa samaki.

Kwa hivyo ni hatua gani wizara yako imechukua baada ya vijana hawa kurudi kupata yale mafunzo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, hatua ziko wazi tu kwa sababu vijana hao sasa wamekuwa ndio walimu wanawafunza wenzao namna gani ya kufuga samaki. Sasa wale wanatusaidia sisi kama wizara kwenda kutoa taaluma kwa wale wengine ambao wanahitaji taaluma. Ahsante.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa eneo la Shungi kipo kikundi kinafuga samaki sijui amekiwezesha vipi na kukipa elimu na kwa vile wizara yake inajua.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, labda kwa taarifa yake tu naomba kumwambia kwamba na mimi binafsi nilikuwa mdau wa kikundi hicho na nimetoa fedha ili kuanzisha bwawa hilo.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha Kwa Mwaka 2012/2013 –
Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana,
Wanawake na Watoto

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea bado nimeendelea kupata maombi ya kuchangia inayofanya sasa idadi ya wachangiaji kufikia 14 waliobaki. Tuko nyuma ya ratiba kwa siku moja kamili shughuli hii ilikuwa imalizike Ijumaa juzi lakini kwa bahati mbaya ndio ilianza siku hiyo. Sasa jitihada zifanyike kutoka kwenu Waheshimiwa Wajumbe ili shughuli hii imalizike leo. Basi tupange *point* zetu vizuri, tuchangie bila ya marejeo kwa mujibu wa Kanuni ya 59 kwa hivyo tutumie muda mchache ili tuwapate wengi kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Ustawi wa Jamii. Baada ya hayo basi nimkaribishe Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata muda mfupi na mimi kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Kwanza Mhe. Spika, niungane na Mhe. Waziri kwa kutoa shukurani katika sehemu kadhaa kama ifuatavyo na nakuomba kupata maelezo mafupi kutokana na wakati kuwa ni mdogo sana. Kwanza Mhe. Waziri katika kitabu chake cha Bajeti ukurasa wa pili kifungu nambari tano alitoa pongezi kwa Mhe. Rais, Dr. Ali Mohammed Shein kwa kuondoa ada ya uzazi na kusema kuwa serikali itagharamia gharama ile iliyokuwa ikitolewa ya shilingi 40 elfu kila mtu anapokwenda kujifungua.

Mimi kwa hili napongeza lakini pia ningeliomba kuongeza kuwa na sisi Waheshimiwa Wawakilishi tulikuwa na kilio kikubwa kwa suala hili na tulipigia kelele nyingi kweli kweli lakini kwa bahati mbaya hatukufanikiwa. Hata Mhe. Waziri hakuwa radhi kuendelea na shughuli hii na mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu afya au matibabu yalikuwa bure kabisa, haya ni mambo yalikuja kimazingira tu. Kwa hivyo, ni kusema kwamba Mhe. Waziri kalia kule kule azma ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoa matibabu bure.

La pili kuna pongezi kwa wazee wanaoishi katika Nyumba za Wazee kwa kuongezewa fedha na pia kwa Mhe. Rais kutangaza kuwa kipindi hiki cha mwaka 2012/13 wawe wanapata milo mitatu. Hii pamoja na kuwa Mhe. Waziri kamshukuru sana Mhe. Rais kwa kufanya hivyo, lakini kama ingelikuwa ni wizara yangu ningelisikitika sana. Hawa ni wazee, hawajiwezi, hawana pa kwenda, hawana pa kurudi wamewekwa katika nyumba kumbe wazee hawa ambao walikuwa wanahitaji kula kila wakati wanaohitaji kula wenyewe walikuwa wakiwekwa na njaa. Kwa hivyo, kupewa milo mitatu si kupongezwa ni wajibu wao na mimi nashukuru Mhe. Waziri kwa kuona kuwa mambo yanaharibika kiasi hicho akaamuwa kuwa wapewe hii milo mitatu lakini wizara ijilaumu kwa wakati wote kumbe wazee hawa walikuwa wanaishi na njaa.

Kuna Waheshimiwa wazee wetu ambao pia ni masikini sana kweli kweli wanapewa shilingi 5000 kwa mwezi tunasema wanapata *welfare*, nawaambia kuwa hii pesa ni kidogo wafikiriwe na waongezewe angalau kwa asilimia 150 wapate kutumia angalau shilingi 30 kwa siku.

Jengine Mhe. Spika, tatizo liliopo ni kuwa kuna wazee wasiojiweza hawa na wanapata *welfare*, lakini kulitokea kipindi hivi karibuni wengi wakakatwa majina yao, nikitaka nijue ni kwa sababu gani wazee hawa waliokuwa siku zote wanasaidiwa lakini tena majina yao yakakatwa ni sababu zipi hasa zilizosababisha kuwa hivyo.

Vile vile kwa nini katika baadhi ya familia unawakuta wazee wale wale wa familia moja wanapata misaada wakati kuna wengine wenye hali ngumu kuliko ile hawapati. Kwa hivyo, hili nataka nipate ufafanuzi.

Halafu wizara vile vile imetoa shukurani, imejitahidi sana kwa kutoa shukurani, imetoa shukurani kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa juhudi kubwa aliyoifanya ya kugawa misaada kwa wale waliofikwa na maafa katika kuzama kwa Meli ya *MV. Spice Islander 1*. mimi naungana nao kwa namna serikali ilivyojitahidi kupita kwa kila jumba japo kuwa kwa vikundi wakati mwengine kwa kuwakusanya watu tokea Rais, Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili, Waheshimiwa Mawaziri na kadhalika kwa kupeleka mkono wao wa pole, si Makamu wa Pili peke yake ni wote wamefanya mpaka sisi tulikuwepo na Waheshimiwa wengine hapa walikuweko kwa wingi tu.

Hii pesa iliyotolewa mimi siwezi nikaiita msaada, mtu anapokufa hapewi msaada huwa anapewa ubani, kwa hivyo tusiite msaada hii tuite ubani. Lakini ubani ulikuwa ni kidogo kutokana na pesa zilizochangwa na watu wengi lakini hapakuibiwa kitu, hizo zilizochangwa ndizo zilizotolewa. Mimi ningelifikiri zaidi Serikali iongeze fungu lake pale kutunisha huu Mfuko. Kwa sababu kitendo cha maafa kilikuwa ni kitendo cha maana sana. Katika meli kulikuwa na mali ya watu chungumzima na vielelezo vipo vilivyopotea naona hapakuzungumzwa lolote.

Halafu nimeona katika ukurasa wa 9 kifungu nambari 19 kuwa wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 1985 ili iendane na hali hili ya dhana usawa wa jinsia bila ya kukiuka misingi ya Dini ya Kiislamu. Mimi Mhe. Spika, hili Uisilamu una maelekezo yake na ndio hayo hayo hakuna mengine. Mimi si sheikhe lakini husikiliza sana hotuba za masheikhe sijaona katika Dini hii ya Kislamu kwanza usawa wa kijinsia. Kwa hivyo, kwanza mimi nilitaka nielezwe huu usawa wa kijinsia unachukuliwa vipi, kwa sababu kwa fikira zangu wanawake wana heshima yao katika dini na wanaume wana mambo yao hakuna sawa na kama kuna usawa tusingeambiwa kuwa *"Alrijaal Qawwamuna ala nnisai"*. Kwa hivyo kwanza hapo nataka nielekezwe.

Halafu la pili katiba yetu inasema mtu ana uhuru wa kuabudu dini anayoitaka, hiyo ni katiba sio imani yangu ya Dini. Kwa sababu hayo basi, mimi ushauri wangu ni kuwa kama serikali inafanya dini anayoitaka. Hiyo ni katiba sio imani yangu ya dini, kwa maana hiyo basi, ushauri wangu ni kuwa kama serikali inafanya na ifanye kwa hadhari lakini sidhanii kuwa wataweza kufanya mambo haya bila ya kuingilia misingi ya Dini ya Kiislamu. Imeingiliwa katika mambo chungumzima kwa hivyo, tukiingiza hapa nahisi ni kama kuwa ni tatizo na sitaki twende huko kwa sababu Katiba inatufunga kuwa kila mtu aabudu dini anayoitaka. Lakini mimi nina imani yangu na mwengine ana imani yake, kuna wengine dini ni moja tu kwa hivyo tusiende huko ningeliomba watu hii wasingeitia hawawezi wakafanya kazi bila ya kukiuka hii misingi au kama wanaiona ipo wanaweza wakatueleza itakuwa ni vizuri zaidi.

Kwa sababu ya wakati Mhe. Spika, sasa naomba uniruhusu niende kwenye viambatanisho na nianze kiambatanisho nambari 17 kilioko ukurasa wa 68-69. Mhe. Spika, kiambatisho hiki kinaonesha nchi zilizoshiriki kambi za kimataifa za vijana Unguja na Pemba kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Kwanza haya malengo hasa yaliopo hapa naona mimi siyafahamu nataka nifafanuliwe vizuri. Hiyo ni (a), (b) hawaonekani hapa Wapemba ni wapi wala Waunguja ni wapi, tunaona nchi tu hizi chungunzima.

Halafu (c) kushiriki kwa vijana wetu katika kambi hizi hebu tuelezwe kwa uwazi hawa vijana wetu wanafaidika vipi, wanafaidika vipi kimila, kiutamaduni, kimazingira na halafu kuna kitu kinaitwa UVIKIUTA kinachohusiana na mambo haya. Ningeliomba nipewe maelezo ya undani na kama haileti maslahi kwetu hakuna ulazima wa kujiunga huko.

Halafu nitakwenda kwenye kiambatisho nambari 13 ukurasa wa 57. Mhe. Spika, kwa hiki ni kiambatisho kinachoeleza vikundi vya vijana vilivyopata ruzuku kupitia Mfuko wa *UN Habitat* mwaka 2011/2012 na vikundi hivi ni sita. Ningeliomba kujua hivi vikundi vilikuwa vingapi na kwa nini vikapata sita tu halafu ni utafiti gani uliofanywa na uangalifu gani mpaka vikapatiwa vikundi hivi sita. Mhe. Spika, nakwenda kwa sababu ya wakati. Halafu pesa zenyewe zilikuwa ni US $ nashukuru.

Halafu Mhe. Spika, kuna kiambatisho nambari 14 ukurasa wa 58, kiambatisho hiki kinaonesha vikundi vilivyopatiwa mafunzo ya uendeshaji miradi Unguja na Pemba kwa mwaka 2011/2012. na hivi navyo naona ni tisa

tu, na vikundi vilivyoko ni vingi, nikitaka nipate maelezo ilikuwaje vikatafutwa hivi vikundi tisa tu na wakati viko vingi na vilikuwa vinahitaji mafunzo hayo.

Kwa sababu ya wakati Mhe. Spika, twende kiambatisho nambari 15 ambacho kiko katika ukurasa wa 58-66. Kiambatisho hiki Mhe. Spika, kinaeleza vikundi vya vijana vilivyotembelewa kwa mwaka 2011/2012 Unguja na Pemba na ni vikundi vingi sana kweli kweli, ni vikundi 114. Nashukuru kwa ziara ya matembezi kwa vikundi vyote hivyo vya Unguja na Pemba, lakini mimi nina suala moja najiuliza Mhe. Spika, hivi vikundi vyote 114 kweli ni vya vijana tu, hakuna wazee kule, hakuna vikundi vya walemavu, vikundi vya walioathirika na UKIMWI najua viko, kuna na vikundi kadhaa wa kadhaa kwa nini hivyo vyengine wakaviacha wakati wizara hii inashughulikia wazee, wanawake, watoto pamoja na vijana.

Lapili kuhusu hivi vikundi kabla sijaendelea katika vikungi vyengine, vikundi ni vingi ni 114 na hii Mhe. Spika, ni Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na watoto inashughulikia vikundi katika mafunzo, katika kutoa misaada na kadhalika. Lakini Mhe. Spika, tukitizama sifanyi kwa nini lakini nataka nipate maelekezo, tuna Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika hivi vikundi vyote ukitizama na kwa muundo hivyo ulivyo na shughuli zao ni vyao, wao wana Mfuko wa Kujitegemea, wana Mfumo wa AK na JK na wanafanya kazi kubwa sana katika kila sekta kuona hivi vikundi vinaendelea na wanavishughulikia vilivyo. Lakini na huku kunatolewa pesa, kunatolewa mafunzo na kadhalika kwa vikundi hivyo hivyo, hii ni *confusion* kwa jina jengine sasa ni kubabaishana.

Ushauri wangu Mhe. Spika, wizara ikipungukiwa na kazi huwa inajiimarisha zaidi kwa vyovyote vilivyo ningeliomba hivi vikundi viwe katika zamana ya wizara inayohusika. Kuna hatari siku moja wizara hizi zitawaniana vikundi na si jambo zuri.

Mhe. Spika, nikiendelea kuna kiambatisho nambari 18 hiki kiko kwenye ukurasa wa 70. Kiambatisho hiki kinaeleza malalamiko ya wanawake yaliyowasilishwa wizarani kwa mwaka 2011/2012 kuna wa Unguja na wa Pemba jumla ni 132, lakini Mhe. Spika, tukiangalia katika kiambatisho hiki utaona mfano kubakwa kwa Unguja na Pemba kwa mwaka mzima ni mtoto mmoja tu. Kwa hivyo, kwa sababu ya kielelezo hiki na vyengine mfano kama shambulio la kitisho Unguja nzima na Pemba ni mmoja tu, mimi nafikiri katika kuweka hii takwimu hawakuwa makini, tunajua kuna watu wengi wamebakwa hivi sasa hata katika jimbo langu hawapungui watatu kesi ziko Mahakamani kwa hivyo mtu akinambia ni mtu mmoja tu mimi siamini. Sasa ningeliomba hili suala kifungu hiki mimi sikubaliani nacho wakati takwimu zake ni muhimu sana kwetu kuweza kujua ni kitu gani tunaendelea nacho.

Mwisho Mhe. Spika, kuna kiambatisho cha nambari 19 kilichoko ukurawa wa 71 na kiambatisho hiki kimeeleza vikundi vya wanawake vilivyotembelewa kwa mwaka 2011/2012 Unguja na Pemba. Kwa ufupi naishukuru wizara kwa kufanya ziara hiyo lakini la kusikitisha tukitaka tusitake Unguja ni kubwa kuliko Pemba, Unguja ina wilaya sita Pemba ni nne inanishangaza kwa nini Unguja ikawa ni vikundi 68 tu vya wanawake wakati vingi vipo na Pemba ni 121. Kwa hivyo, ninataka kujua kwa nini kule Pemba kulikokuwa ni kisiwa kidogo na vikundi pengine vikawa vingi vilivyotembelewa kuliko hapa Unguja.

Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kueleza hotuba yangu angalau kwa njia ya *point.* Ahsante.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia na vile vile nampongeza Mhe. Rais wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoendeshwa kwa Mfumo wa Umoja wa Kitaifa kwa kumchagua Mhe. Zainab Omar kuwa waziri wa wizara hii na hakupotea.

Mimi Mhe. Spika, nitachangia sehemu ya ukurasa wa 30 Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, maendeleo ni jambo lenye upana mrefu sana, kwanza kwa kutaka maendeleo serikali kwa kupitia wizara hii ya Mhe. Zainab kwanza kuwaizinisha na kuwapa elimu akinamama pamoja na watoto, hasa elimu ndio msingi wa mwanadamu, elimu ndio chanzo cha maendeleo ya mwanadamu, binadamu bila ya kupata elimu bado hajawa na maendeleo. Ningelimuomba Mhe. Waziri wizara yake ichukue jitihada ya kuwaelimisha akinamama kwa kuwakusanya kwa makusudi ili kuwapa taaluma ndani ya biashara zao kuweza kupata faida nzuri.

La pili, Zanzibar akinamama, akinababa pamoja na watoto wengi wetu ni maskini. Miradi yetu ni midogo, mifupi sana, tija zake ni ndogo. Kwa vile ili kupata maendeleo serikali kwanza iwafikirie wananchi kuwapa huduma na nyenzo za kufanyia kazi ili kupata hayo maendeleo yenyewe.

Kwa sababu watu wa Zanzibar ni watu wenye kuishi katika mazingira magumu. Serikali kama itachukua juhudi ya kuwakopesha wananchi zana za kufanyia kazi badala ya kuwapa pesa mkononi, ninafikiri maendeleo yatakuwa mazuri. Kwa mfano kuna akinamama hivi sasa wanao uwezo wa kuendesha viwanda. Kuna SACCOS ambazo zinafika watu 70, kama serikali inajitahidi kuwaletea viwanda akinamama wale basi ninamini wanaweza wakapata maendeleo.

Kwa mfano sehemu zetu za mashamba akinamama wanalima lakini ukulima wao ni kijembe kongoroka. Sasa wakiwa akinamama, serikali pamoja na wizara watawezeshwa kukopeshwa matrekta, wakaweza kulima hivi vikulima vya mbogamboga, kunde, ninafikiri wanaweza wakajikomboa haraka kuliko kuwapa pesa mikononi.

Kwa mfano akinamama waliokuwa 70 wanapewa shilingi milioni 70. Wakigawa wote wale, kwanza zitafikiriwa kwenda kununuliwa vitambaa vya harusi. Hilo moja, lakini watawezeshwa viwanda, kazi za mikono ninahakikisha akinamama wataendelea upesi upesi.

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri awafikirie akinamama awape viwanda. Akinamama wanakopeshwa shilingi milioni mbili, lakini biashara ya mama yule anakwenda kununua maandazi, akiuza maandazi Manispaa anayachukua yote. Haya sasa mkopo ule mwisho wa mwezi anangojewa alipe shilingi thamanini elfu kwa mwezi na Manispaa ameshayachukua maandazi. Kweli mwanamama huyu ataendelea. Lakini mwanamama kama atawezeshwa trekta aende shamba kule akalime, Manispaa hawezi kwenda kulichukua trekta wakenda kugawana pale.

Kwa hivyo ninaiomba serikali wawezeshwe akinamama kwa zana badala ya kupewa pesa za kuuza maandazi. Maandazi hivi sasa yanachukuliwa na Manispaa wanagawana tu basi. Haya mama huyo ataendelea? Hivyo ninaiomba wizara hii ifanye juhudi iwakopeshe akinamama zana za kufanyia kazi badala ya kupewa pesa mkononi.

Nchi za wenzetu tunakwenda kama China, Marekani, hebu tutizame akinamama wa China wanavyowezeshwa, wanawezeshwa vipi. Hawawezeshwi maandazi akenda akachukua Manispaa, wanawezeshwa zana za viwanda. Viwanda ndivyo ambavyo vitainua uchumi wa nchi, na ndivyo vitakavyoinua akinamama na akinababa.

Mhe. Spika, Majimbo yetu ya Matemwe kule, Chaani, Mkwajuni tunazo ardhi za kulima. Lakini hatuziwezi kwa sababu hatuna zana. Akinamama wanalima sana mpunga, kunde lakini zana hawana. Kwa hivyo serikali ninaiomba kupitia Wizara ya Mama Zainab uwakopeshe akinamama matrekta waliokuwepo mashamba walime.

Waliokuwepo mjini ninamuomba Mama Zainab awezeshe akinamama viwanda. Kuna viwanda vya useremala. Hivi sasa wanawake wote wameshasoma, wanaweza wakiwezeshwa.

Mhe. Spika, nikiendelea hapo hapo maendeleo ya wanawake na watoto. Watoto wetu tunao wengi sana. Lakini jinsi ambavyo hatujawapa elimu ya ujasiri amali, hatimae hivi sasa wanavuta bangi kwa sababu hawana kazi ya kufanya. Hivyo mtoto hivi utamjengea kiwanda atakwenda kuvuta bangi, atakuwa na wakati wa kuvuta bangi. Hebu twendeni katika China kule, Marekani wapo watu hivi sasa wanafanya kazi saa ishirini na nne katika viwanda, wanavuta bangi, hawezi kuvuta bangi.

Ninaiomba serikali tuweze mageuzi ya maendeleo. Tuwawezeshe wananchi kazi za ujasiriamali. Hasa akinamama wamepata Waziri ni mwanamke, hakuna sababu akinamama wasiendelee kwa sababu waziri wao ni mwanamke. Hakujakuwa Waziri mwanamme. Waziri wa akinamama hakuna sababu akinamama wasiendelee. Bi. Zainab ni jina tukufu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nikiendelea kuzungumzia kuhusu maendeleo. Maendeleo kama nilivyosema yana nyanja kubwa sana, yanahitaji elimu. Tunao akinababa na wengi wetu hivi hatuna elimu hata ya biashara, tunakwenda tu. Kwa hivyo vile vile Mama Zainab ninamuomba na sisi akinababa utupe elimu, usiwape akinamama tu na sisi utupe elimu ili tupate kuendelea.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi sichangii sana, nimechangia kidogo kwa kuiomba serikali hivi sasa itubadilishie mfumo, iwatizame akinamama kwa kuwawezesha kwa sababu akinamama wengi hivi sasa ni wajane, wameachwa na watoto watano, sita, hawana vya kuwafanya. Kwa hivyo mama uwaonee huruma akinamama. Uwatafute akinamama makusudi hasa uwaelimishe na kuwawezesha.

Mhe. Spika, akinamama wengi hivi sasa wanazurura. Kwa mfano mjini Mhe. Spika, unaweza ukawawezesha katika kiwanda kimoja cha manukato, kwa sababu haya manukato hivi sasa yamechukua bei sana au tuseme yana soko.

Mhe. Spika, baada ya kuwezeshwa wananchi, serikali iwatafutie soko la kuuza bidhaa zao. Wananchi wengi hivi sasa, wengi wana biashara lakini wanakosa soko. Soko ni kitu muhimu katika biashara.

Mhe. Spika, ninashukuru kwa kunipa ruhusa hii ya kuchangia. Ninamalizia hapa ninaunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri na nitaunga mkono zaidi bajeti pindipo atuoneshe kwamba akinamama viwanda vyao ni hivi. Atuchukue Baraza la Wawakilishi ututembeze katika viwanda vya akinamama. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kwa kuichangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataallah* kwa kunijaalia uzima wa kuweza kusimama hapa na kuweza kuichangia bajeti hii.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi kwa sababu mengi yameshazungumzwa na sitaki kupinga kile kipengele cha kujirudia rudia, lakini nitakuwa ninaunga mkono baadhi ya maeneo ambayo tayari wameshayachangia.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika kipengele cha malengo makuu ya Wizara. Lakini kwa kuwa sitaki kurudia, napenda kuunga mkono maneno ya wenzangu waliosema kwamba katika malengo makuu ya wizara hii kuna mambo mengi yanajirudiarudia kutoka bajeti iliyopita na bajeti hii. Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba aliangalie vizuri suala hili.

Mhe. Spika, kwa kuendelea kuichangia hotuba hii, niende kuhusu benki ya wanawake. Mhe. Spika, pia wachangiaji waliochangia wamechangia sana suala hili, lakini na mimi nieleze tu kidogo kwamba Mhe. Waziri, mimi ninahisi hii benki ya wanawake imekuwa ndoto ya alinacha, kila siku inazungumzwa, inapangiliwa lakini hadi leo bado naona haijakaa vizuri.

Kwa hivyo Mhe. Waziri mimi naomba atakapokuja kutoa majumuisho yake, hebu atueleze ni lini hasa benki hii au kuna mikakati gani ya makusudi ya kuweza kufanikisha suala, ili benki hii iweze kuanzishwa ili wanawake wa Zanzibar waweze kufaidika na kunyanyuka kiuchumi kama wanawake wenzetu katika nchi za wenzetu.

Halafu Mhe. Spika, labda nimesema ni ndoto za alinacha kwa sababu nina sababu moja ya kufikiria hii ni ndoto. Kwa sababu Mhe. Waziri katika wizara yako hapo nyuma kulikuwa kuna huu mradi wa kupunguza ajira za watoto na kuongezea akinamama kipato.

Mradi huu ulikuwa umefadhiliwa na ILO. Mradi huu na mimi katika mkoa wangu nilibahatika katika Shehia ya Chwaka na Uroa kuwa ni Shehia za *pilot area*. Walikuja wafadhili wale wa ILO wakasomesha, wakawasaidia akinamama, wakasaidia fedha za kuendeleza mradi ule kwa kiasi. Sasa baada ya kumalizika mradi huu, wizara yako kwa kushirikana na ILO walitaka kujaribu kuwaunganisha wale akinamama wa Chwaka, Mkokotoni na mjini ili kuweza kuanzisha hii benki ya pamoja kwa hizi SACCOS ambazo zilikuwa zimeingizwa katika mradi huu.

Lakini Mhe. Spika, cha kusikitisha ni kwamba baada ya muunganisho ule lakini kilichoendelea ni kwamba watu wa Chwaka – SACCOS ya *TWENDE SALAMA* ile ilitoa pesa zake nyingi na Mkokotoni kuunganisha ili kutaka kufanya ile benki ya wanawake. Lakini kilichotokea ni kwamba zile pesa zilipotea. Hivi sasa malalamiko yamekuwa mengi. Wanawake walikuwa wanajikhini, wanahangaika, wanakata kuni, wanakwenda mwani, wanachangia ile SACCOS yao ili waweze kujikwamua.

Lakini matokeo yake Mhe. Spika, badala ya kujikwamua wizara hii imewakwamisha zaidi na mpaka leo wanahangaika, kila siku mimi wananijia wanakwenda Wilaya, wakienda kusikiliza, wanaambiwa aah!

Wanagombwa na wafanyakazi wako. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja nataka uje unipe hasa ufafanuzi wa suala hili, jee wanawake wa Chwaka hizi pesa zao ambazo wameziingiza wamezileta huku mjini, maana yake huku mjini kumeonekana kama kuliko na watumiaji, wametolewa kule wameletwa mjini kumeundwa SACCOS ya pamoja ya waridi, lakini waridi limeonekana linachanua mjini tu, kule wanalalamika, wanalia na pesa zao nyingi wamepoteza na nguvu zao wamepoteza. Kwa hivyo Mhe. Waziri utakapokuja unipe maelezo ya kina kuhusu hii waridi imefikia wapi wanawake wa Chwaka pesa zao watazipataje.

Mhe. Spika, kwa kuendelea niende katika Idara ya Ustawi wa Jamii. Mhe. Waziri kwanza nikushukuru sana kwa kuongeza huduma hii ya wazee, kuwaongezea posho wazee wetu na huduma ni suala zuri. Lakini ninaomba kukuuliza hivi umetumia kigezo gani katika hili ongezeko la pesa hizi za wazee. Kwa sababu inaonekana katika kitabu chao kwamba wazee wa Sebleni wametoka shilingi ishirini na tano wamekwenda shilingi elfu arobaini.

Lakini wazee wa Limbani, Gombani wametoka shilingi elfu saba wamekwenda mpaka shilingi elfu kumi tano. Halafu kuna hawa wa Makondeni wanalipwa shilingi elfu ishirini na tano. Hapa hizi kuna tofauti gani baina ya wazee wa Sebleni na hawa wazee wengine. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri unipe ufafanuzi.

Halafu Mhe. Spika, ninataka kuuliza Mhe. Waziri katika mikoa yetu huu mpango wa kuwasaidia wazee ambao wapo katika yale makao ni mzuri, lakini katika mikoa yetu na sehemu nyengine ambazo tunazotoka, kuna wazee ambao ni maskini, wazee ambao hawajiwezi, wana matatizo, wana njaa, wana taabu lakini hawapo katika nyumba zile za kutunzia wazee, wapo kule.

Sasa wale wanalipwa shilingi elfu tano kwa mwezi. Shilingi elfu tano yenyewe inawezekana mwezi huu waipate na mwezi huu wasiipate. Shilingi elfu tano hiyo ataikopea kila duka, husema mimi nikiipata shilingi elfu tano yangu nitakuja kuilipa, wanapata shida. Hebu Mhe. Waziri aniambie wazee hawa ambao wapo vijijini hawapo katika yale makaazi maalum ya serikali, hawa umewapangia mipango gani, akinamama wanapata taabu na kuhangaika. Kwa hivyo utakapokuja unipe ufafanuzi wa suala hili.

Halafu Mhe. Spika, Mhe. Waziri pia ninataka kuna wanawake wamekuwa wakiomba sana hasa katika mji huu wa Zanzibar. Wanawake wanaonekana wengine wana nguvu zao, kama watapatiwa mradi labda au pengine watapatiwa elimu au kukusanywa na wapewe mafunzo labda wanaweza. Sijui hawa wanawake ombaomba wa mjini, asubuhi ikifika wanapanda magari wanakwenda zao mjini, pesa pesa hizo kwa ushahidi wanazozipata wanazoombea pale mjini wengine utaona wanakuwa wanafanyia mambo hasa ya maendeleo.

Wako wengine wanajenga mabanda kwa pesa zile za kuombea pale mjini. Sasa hawa umewaweka au umewapangia mpango gani wanawake wale ombaomba wanaokuwepo kule mjini na kuomba.

Mhe. Spika, kwa kuendelea na mimi nieleze kidogo tu ambapo Mhe. Abdi amenifilisi kwa kiasi fulani kuhusu hii Idara ya Wanawake na Watoto kuwainua wanawake kiuchumi. Kwa sababu yale niliyokuwa ninataka kuyasema yeye mwenzangu ameyasemea sana kuhusu wanawake, badala ya kupewa tu mafunzo na kupewa pesa, waanzishiwe viwanda, labda watafutiwe nyenzo za kufanyia kazi ili kuweza kuwapatia kipato.

Kwa sababu mwanamke ukimpa pesa anaweza akafanyia mengine. Unampa elimu lakini mwanamke ni mtu wa huruma sana. Linaweza likatokezea jambo akashindwa kuidhibiti na kuitumia ile pesa ya biashara akaitoa kwa ajili ya kufanyia mambo mengine ya kijamii ambayo yaliyotokezea. Kwa hivyo mimi ninadhani hili Mhe. Abdi kalizungumza kwa kirefu, naomba hilo niliache niende mbele Mhe. Spika.
Mhe. Spika, mimi ninadhani nimalizie kwa suala la udhalilishaji wa watoto kijinsia. Mhe. Spika, ninadhani kila mmoja suala la watoto ni muhimu sana katika maisha yetu ya kawaida, kwani watoto ni mbegu na raslimali ya taifa la baadae. Watoto hao hao ni vitega uchumi vyetu kwa taifa lolote duniani. Hivyo basi watoto hao wanahitaji kuekewa mazingira mazuri, kusomeshwa vizuri.

Tunashukuru Mhe. Waziri kwamba katika malezi yako umesema kwamba kuna watoto wengi ambao wanaishi katika mazingira magumu umewasaidia kupatiwa sare na mambo mengine. Lakini sasa Mhe. Spika, hili suala la udhalilishaji wa watoto kijinsia limekuwa kubwa mno.

Hizi takwimu ambazo zimo humu inaonekana hazikidhi. Kesi zipo nyingi lakini ufumbuzi wake unakuwa wa utatanishi. Kesi ikikamatwa *ready handed* utaambiwa suala halina ushahidi, sijui limekosa nini, linakwenda lile mpaka baadae mtuhumiwa anaachiwa anakwenda kufanya tena.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri tunataka tujue hii sheria hasa ya udhalilishaji ibadilishwe na iwekwe sheria kali ya kuwafanya hawa wanaume wanaowadhalilisha hawa watoto wapewe sheria kali ili hili suala likomeshwe. Hebu Mhe. Waziri naomba ifanye kazi, kama hii sheria haitoshi basi ibadilishwe, na ifanywe sheria nyengine ambayo itawakomesha hawa wanaofanya masuala hayo.

Mhe. Spika, kwa kweli inauma kama mimi ni mama, na wewe ni mama ambaye upo katika wizara hii, ninadhani suala hili utalichukulia kwa uzito wake. Hii sheria kama haifanyi kazi basi Mhe. Waziri ubadilishe sheria ambayo itawabana hawa kuwakomesha kuwadhalilisha hawa watoto wetu ili tuwe na taifa zuri baadae.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, baada ya kuja kunipa ufafanuzi wa yale ambayo nimeyahitaji. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja, ninaiunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, ninakushukuru na mimi kunipa nafasi hii. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama hapa na kuchangia bajeti ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake. Mimi binafsi Mhe. Spika, nilipomuona Mhe. Zainab anawasilisha hotuba ile nilimshangaa sana kwa sababu alikuwa kama mfano wa mashine ya cherehani iliyofungwa mota. Kutokana na umri wake Mhe. Spika, hiyo ni sifa kubwa.

Mhe. Spika, sasa mimi nianze kwa matatizo yanayowakabili wanawake. Hivi sasa Mhe. Spika, wanawake wengi wamekumbwa na maradhi ya kensa ya matiti. Maradhi haya ni mengi na kila siku yanaongezeka.

Maradhi haya Mhe. Spika, matibabu yake ni ghali na usumbufu mkubwa kupatiwa tiba hasa ukitizama uwezo wa wanawake. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri aniambie ana mpango gani kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuwasaidia wanawake hawa waliofikwa na tatizo hili.

Mhe. Spika, vile vile matatizo ya wanawake hivi sasa kuna mawakala hapa nchini kwetu, na wengine wa nje ya nchi yetu wanapenda kuwachukua wanawake na kuwapeleka nchi za Uarabuni kufanya kazi za ndani.

Mhe. Spika, hata hivyo wanawake hawa wanaokwenda huko hudhalilika kwa kupigwa pamoja na mambo mengine ambayo si vizuri kuyataja katika Baraza hili. Mhe. Spika, Mhe. Waziri sijui ana mpango gani wa kuelimisha jamii ili kuachana na mambo ya kuwapeleka wanawake hao nje katika nchi hizi za Kiarabu, na kulinda heshima ya wanawake wa Kizanzibari.

Mhe. Spika, vile vile nikija kwa upande wa watoto naomba nichangie. Zanzibar kama nchi nyengine za Afrika zinapenda kufuata sheria na sera za nchi za Magharibi. Mhe. Spika, sheria tunazozitekeleza kutoka nchi hizo haziendani na tamaduni zetu.

Mfano mdogo Mhe. Spika, wanafunzi maskulini kuambiwa wasipigwe mikwaju. Hii Mhe. Spika, imepelekea watoto kukosa nidhani kwa walimu wao na hata wazazi wao. Mhe. Spika, utamaduni huu utatuathiri kwa vizazi tulivyonavyo na vijavyo. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri ajue ikiwa serikali ina nia ya kujenga jamii iliyo bora, basi izitazame vizuri sheria hizi za Magharibi.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kidogo niende ukurasa wa 34. Mhe. Spika, mimi binafsi nimefarijika kwa kuona pana ujumbe kwa mwaka huu unaosema, “Haki za Watoto wenye Ulemavu ni jukumu letu kuzilinda, kuziheshimu, kuziendeleza na kuzitekeleza.

Mhe. Spika, ikiwa hili tutafanikiwa ninaamini tutakuwa tumefanya kazi kubwa, kwa sababu udhalilishaji wa watoto wenye ulemavu umekuwa mkubwa na wala hakuna ufumbuzi unaopatikana, kwa sababu juzi tu katika Baraza hili lililetwa suala la mtoto mlemavu anayeitwa Msimu. Mhe. Spika, inaonesha dhahiri kwamba mtoto yule si rahisi haki

yake kuipata kwa sababu tunaambiwa kusubiriwa kipimo cha DNA na hatujui kitapatikana lini. Pia namuomba Mhe. Waz\iri sijui suala hili atashirikiana na waziri wa Katiba na Sheria, kwa nini hawa walemavu hawawekewi sheria zao, kwa sababu Mhe. Spika
, kuna walemavu wanazungumza kwa ishara, lugha za alama zile. Kweli Mhe. Spika, lugha ile haijaweza kuwa ushahidi ni lazima papatikane kipimo cha DNA.

Mhe. Spika, mfano yule mwanamke aliyebakwa pengine hakubeba ujauzito, ina maana pale kwa kuwa hapana kipimo, yule mtoto hafai kupata haki yake au ule ujauzito wake umetoka kabla ya kufika miezi sita. Kwa kuwa tu kimekosekana kipimo cha DNA, inaonesha kwamba huyu haki yake haitopatikana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakae na kuandaa utaratibu hasa wa kuweka sheria za kuwalinda watoto wenye ulemavu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Chake Chake naunga mkono hotuba hii ya Waziri. *(Makofi).*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Namshukuru Allah kwa kutujaalia uhai, uzima na taufiki ya kuzungumza. Mhe. Spika, ni mara ya pili au ya tatu kuzungumza kwamba wizara hii inapewa bajeti ndogo sana, kutokana na bajeti hiyo ndogo ambayo inapewa, inaelekea baadhi ya mambo ndio yakakosekana.

Mhe. Spika, karibu Wizara zote zinazo watu wa aina hii, wako vijana, wako watoto na wako wanawake na wako wazee, lakini hii imepewa jukumu la wote. Mimi nafikiria kwamba jukumu kubwa la wizara hii ingekuwa ama kufanya utafiti wao wenyewe au kuziunganisha tafiti zinazofanywa na kuziarifu wizara mbali mbali, pamoja na serikali kuu kwa jumla jinsi hali inavyokua kuhusu watoto, wanawake, vijana na wazee.

Mhe. Spika, mimi nataka nitoe mfano, katika kitabu cha Mhe. Waziri kuna malengo ya wizara na kuna malengo ya idara tofauti. Kwa mfano, katika ukurasa wa tano kuna malengo makuu ya wizara, katika ukurasa wa 30 na 31 kuna malengo ya idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Katika ukurasa wa 35 kuna malengo ya Idara hii ya wanawake na watoto kwa mwaka huu wa 2012/2013. Lakini Mhe. Spika, hakuna malengo makhsus yaliyowekwa, malengo yote ni ya jumla jumla.

Mhe. Spika, utafiti uliofanyika kuhusu lishe kwa mama wajawazito na watoto, inaonesha kwamba Zanzibar bado kuna tatizo la ukosefu wa lishe bora kwa mama wajawazito na watoto, na utafiti uliofanywa na ripoti iliyotolewa na UNICEF, inaonesha kwamba siku 1,000 za mwanzo za mtoto, yaani kuanzia anapobeba mimba mama mpaka anatimia miaka miwili, ni siku muhimu sana katika kukua ule mgongo wake na kufanya kazi. Kama katika kipindi hicho hakupata lishe bora, ina maana kuna hatari ya kwamba yeye anaweza akadumaa au akapata matatizo mengine ambayo hayarudishiki tena. Kwa hivyo, katika kitabu hiki sikuona pahali palipotajwa kwamba ushughulikiaji wa lishe bora kwa mama wajawazito na watoto. Sasa hili lingekuwa ni moja kati ya malengo makhsusi la wizara hii, kuona kwamba utafiti ule uliofanywa ulielekezwa kwao na ripoti imetoka ipo ya Tanzania na ipo ya Zanzibar. Sasa pale ndio tungepata kujua kwamba wao wameelekeza vipi.

Kwa hivyo, wao sio watekelezaji peke yao, lakini wao wanaziunganisha zile tafiti zinazofanywa sehemu mbali mbali kuhusu mama wajawazito na watoto na kuzifuatilia katika zile wizara. Kwa mfano kuhusu hii lishe, tunayo sisi sera ya lishe na chakula, *food security and nutrition*. Kwa hivyo, ingetizamwa sera hii imeishia wapi, je imo ndani ya vitabu tu au tayari inamnufaisha mtoto na mama mjamzito kwenye maeneo tofauti. Upatikanaji wa samaki na vitoweo ni tatizo kubwa sana kwa familia nyingi. Kwa hivyo, kunapelekea kwamba mama wajawazito baadhi yao wengi wanapata matatizo ya ukosefu wa damu. Suala hili lingetizamwa katika ule utafiti wao linaelekezwa wapi, ili hii Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Mifugo na Uvuvi zikachangamka kuhusu jambo hili. Lakini ikiwa kila wizara inakwenda kivyake, basi wizara hii itakuwa haijafanya ule wajibu wake wa kumshughulikia mtoto alipo na kumshughulikia mama mjamzito alipo. Kwa hivyo ni lazima wizara hii iwe ni muunganishi wa wizara kutokana na mambo tofauti.

Mhe. Spika, katika Baraza lako tukufu hili, mimi ndio nilikuwa *champion* wa kupiga kelele sana kuhusiana na watoto wetu kukaa chini maskulini. Tunaishukuru serikali kwa kuona haja sasa ya kuwa na *fund* maalum kuhusu ma-*desk.* Lakini ningetegemea kwamba wizara hii inafuatilia nayo kuhusu hawa watoto maskulini wanafanywa vipi. Hata ile kukaa chini ina maana unawapotezea haki zao, kwa sababu kuna watoto wengine wanakaa juu ya viti na meza na kuna wengine wanakaa chini. Ina maana kuna wengine wananyimwa haki zao za kuweza kujisomea. Hapo

tutakapokuja katika sera ya elimu, imetoa utaratibu huu wa kwamba kuwe na usawa katika utoaji wa elimu. Sasa ikiwa watoto wengine wanapewa fursa ya kukaa juu ya viti na meza, lakini watoto wengi hawapati, ina maana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni moja katika inayowanyima haki zao watoto.

Mhe. Spika, mara nyingi tunasema kwamba pawe na malengo, haiwezekani sisi Zanzibar kuendelea ikiwa watoto wengine wanakaa chini na watoto wengine wanakaa juu ya viti. Haiwezekani ni lazima tuwe na malengo, tuseme hasa ikifika mwaka fulani, basi tuliondoe tatizo hili. Mimi nili-*suggest* humu kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, nikawaambia tupunguze gharama kubwa tunazotumia kwenye sherehe, tuandae mkakati wa kuwa watoto wote wakae juu ya viti na meza. Ilipofika mwaka 2014 sherehe za Mapinduzi zije ikiwa watoto wetu kila mmoja akiwa kakaa juu ya kiti na meza, mambo ya kusema kila siku hapa patashughulikiwa, kuna skuli nyengine ni asilimia 100 na kuna skuli nyengine ni asilimia 50. Sasa huo ni usawa gani kwa watoto?

Kwa hivyo, mimi nafikiria kuwa hii wizara ina kazi kubwa zaidi kuliko vile ambavyo ilijiwekea malengo yake, ni kumtizama kila mahala mtoto alipo. Tunaiangalia Wizara ya Afya, mtoto chini ya miaka 2 anapewa usaidizi gani. Kama mtoto anachanganywa na wagonjwa wengine, hakuna kama hospitali kubwa ambazo zina wagonjwa wengi, hakuna pahali ambapo mtoto kama ana miaka chini ya miaka miwili, anapelekwa kwa daktari maalum wa watoto, mtoto yule ananyang'anywa haki yake, kwa sababu anachanganywa na watu wengine.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nafikiria hii wizara iweze kuchukua jukumu lake ni kumwangalia, mtoto tunamuangalia katika utunzaji wake, mazingira ambayo tunakaa ni safi, ukitembea katika geto kwa mfano, maeneo ambayo yana mchanganyiko wa nyumba, Je, mazingira yake ni safi. Sasa watu wanaoshughulika na usafi wa mji na sehemu nyengine, watakuwa na wao ni *mas-uul* wa kuona kwamba watoto wanacheza katika mazingira yenye usafi. Kwa sababu moja katika jambo kubwa ambalo linatakiwa katika kunyanyua afya ya mtoto ni kuishi katika mazingira yaliyo na usafi. Baada ya kusoma katika sehemu tofauti, ndio wizara hii iweze kuiandikia serikali kuiambia kwamba watoto wetu wanaishi katika mazingira haya, kwa hivyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ifanye kadha na kadha, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ifanye kadha na kadha. Kuna skukuu zinatokea Jumamosi na Jumapili, watoto wanataka kwenda kucheza katika sehemu za miji, viwanja vyao vinachukuliwa na kujengwa nyumba na watu tofauti. Kwa hivyo, ina maana watoto hawana pa kucheza, viwanja vyote vya wazi vinachukuliwa na kujengwa nyumba kubwa kubwa, kila mmoja anachukua ardhi. Sasa tutakuja kusema kuhusu watoto, lakini sisi wenyewe ndio tunawapokonya haki zao.

Mhe. Spika, kama wizara hii haikukaa ikasoma tafiti tofauti zinazofanywa, haikukaa ikafanya wenyewe tafiti wanazoziweza halafu ikaishauri serikali, bado tutakaa katika vitendawili vile vya kuweka malengo ambayo ni ya wazi, sio malengo mahususi. Ni lazima tufikie wakati wizara itoe malengo mahsusi. Kama nilivyosema katika utangulizi wangu wa mwanzo pale, kwamba Zanzibar tayari katika utafiti wa *UNICEF* wameona kwamba kuna *population* fulani iko *under nutrition*, yaani lishe ni ndogo. Lakini kwa wanawake wa mjini hasa hapa Unguja ni wazito sana kuliko uwezo wa kiwiliwili chao, sasa wizara hii imefanya kazi vipi ya kuwashauri hawa wanawake wapunguze, ili afya zao ziweze kuongezeka. Utafiti wa *UNICEF* huo uliofanywa inaonesha kwamba wanawake wa mjini Unguja ni wazito kuliko uzito wao wa kawaida, yaani wako *over weight.* Wizara hii imefanya kazi gani ya taalim, hawa ambao wana lishe ndogo waweze kupatiwa lishe, lakini wale ambao lishe yao kubwa zaidi na hawana mazoezi, wizara imefanya utaratibu gani wa kuweza kuwaelimisha hawa wanawake, kwa sababu hizi ndio tafiti ambazo zinafanywa ili tuweze kunufaika.

Mhe. Spika, nikija kwenye sehemu za vijana. Mimi nafikiria kwamba vijana wana mambo matatu. Kwanza wanataka ajira, wizara hii sio kazi yake kutoa ajira, kama itapata fursa ya kuanzisha ajira, sawa. Lakini kazi yake ni kuhamasisha wizara nyengine waweze kutoa ajira kwa vijana bila ya upendeleo. Mimi nitastaajabu sana ikiwa waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, itakuwa hafanyi kazi karibu na wizara hii. Lakini haiwezi kufanya kazi karibu na ikawa wizara hii haina takwimu sahihi ya ajira ya vijana, tukiwa na takwimu sahihi za ajira za vijana katika maeneo tofauti, basi tunaweza tukaichangamsha hii wizara, kwa sababu inawezekana akawatazama hawa wa mjini, inawezekana akawatazama wa mkoa fulani, lakini kama wizara ina takwimu za vijana ambao hawana ajira na wana uwezo fulani, basi inaweza ikaichangamsha hii Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Maeneo ya wavuvi, maeneo ya wakulima, maeneo ya wanawake wanaolima mwani. Yote hayo ni maeneo ambayo wizara hii iweze kuyajua na iweze kuiandikia wizara kama hii ya uwezeshaji.

Mhe. Spika, kwa hivyo, ni lazima wizara ichangamke, kwa sababu imepewa kazi ya kuunganisha, haiwezekani tukae ofisini tu, halafu tufikirie kwamba sisi tunafanya kazi ya wanawake, watoto na vijana. Suala la pili vijana

wanalotaka ni michezo ukiwemo mchezo wa mpira wa miguu. Je, wizara imefanya utafiti wa kiasi gani, kwa sababu naona Zanzibar, mara nyingi huwa nasema tumebakisha na huu mpira wa miguu tu, lakini riadha hakuna siku hizi. Hujasikia kijana wetu kenda mbio kwa mita ngapi. Je, kuna kitu gani kinachozuia kwamba maskulini kusiwe na michezo ya riadha. Kwa sababu riadha ndiyo inayowafanya vijana wetu wakachangamka.

Mhe. Spika, moja katika haki za vijana ni kufanya riadha na michezo mingine. Kwa sababu tatizo la mpira wa miguu linawachukua watu kidogo tu, kwa sababu timu inaweza kuwa na wapenzi 1,000 lakini wachezaji ni 15 tu. Lakini riadha inaweza ikachukua watu wengi sana, kama mbio zile za *marathon* ambazo watu wengi sana wanaweza wakashiriki, ni lazima tuchangamke Zanzibar ni hii hii, sisi tunasema Zanzibar ni nchi, lakini haina mambo ya kinchi ndio maana tukaitwa sio nchi. Kwa sababu mambo yake ni hivi hivi tu. Sasa kama tunataka kuifanya ni nchi ni lazima waweze kujua leo ni siku ya riadha Zanzibar inatangaza, vijana wote wanafanya riadha.

Mhe. Spika, vile vile vijana wanataka elimu yenye manufaa na wao, vijana wetu wanapomaliza skuli zile nyenzo za kusoma baada, yaani elimu mbadala ni maneno tu yapo, lakini hakuna vituo ambavyo vinasomesha vijana kwa kazi mbali mbali. Vijana wanataka kujisomesha uvuvi, leo uvuvi tulionao ni kuingia ndani ya mashua ukaambiwa twende zetu, lakini hapana chuo cha uvuvi hapa, ambacho kitawafundisha vijana angalau uvuvi wa kisasa. Ukija kwa wakulima hali ndio hiyo hiyo na ufugaji hali ndio hiyo hiyo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, pia kwa upande wa serikali vile vile ijue majukumu yake, kwa sababu unapowaambia kwamba wewe ni Waziri wa wanawake, vijana na watoto, iwe iwe inajulikana kwamba *specification* zao ni hizi na hizi, na hii ni wizara mtambuka, yaani inaingia kila pahala. Sasa Waziri atakayeendewa akaambiwa Mheshimiwa vijana wa eneo fulani pamoja na wanawake na watoto wanasumbuka hawana barabara, hivyo ajijuwe kwamba kaambiwa na wizara jukumu lake.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, dakika tatu unazo kumaliza hotuba yako.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, baada ya hayo niliyozungumza, napenda nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa, lakini namuomba sana aweze kuchukua haya ambayo nimeyachangia kwa maslahi ya nchi yetu na kwa maslahi ya wanawake, vijana na watoto. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu *Subhanahu Wataallah*, aliyetujaalia uhai na uzima tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwa kuwa na mimi ni Mjumbe wa kamati ya wizara hii. Kwa hivyo, nina mawili au matatu tu sitotumia sana muda wako.

Mhe. Spika, naanza kusema kwamba wizara hii imepewa jina la ustawi wa jamii. Neno ustawi wa jamii lina maana pana sana. Kwa kweli ustawi wa jamii unakusanya hasa huduma zote mbali mbali zinazomgusa kila mmoja wetu katika taifa letu. Hii wizara ina mambo mengi muhimu yaliyogusa moja kwa moja wananchi wote wa Zanzibar. Bila kuchagua huyu ama yule, imekusanya kulea watoto, imewakusanya vijana, ina wazee na ina wanawake wenyewe ambao ndio wazazi wa taifa hili.

Mhe. Spika, nilikuwa napenda sana wakati nikiwa nataka kutoa hotuba yangu hii awepo Waziri wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kimtazamo wangu ni kwamba hii wizara imepewa jina, lakini ukubwa wa jina hili haukutandazwa katika upana wake wa shughuli zake kiutendaji. Ustawi wa Jamii unagusa afya ya binadamu, malazi, haki zote za kibinadamu, malezi, makuzi pamoja na kazi zao na mazingira yote yaliyowazunguka, huo ndio ustawi wa jamii. Kwa hivyo, wizara hii mwenzangu aliligusia Mhe. Rashid Seif, kwamba katika wizara ambayo inapatiwa pesa finyu sana, na ambapo majukumu yake ni makubwa basi ni wizara hii. Huo Mhe. Spika, ulikuwa ni utangulizi wangu.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye mchango wangu. Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 18 katika kifungu cha 46 kinachosema ustawi wa jamii. Hapa nimeona kuwa Waziri amegusia kwamba ametoa msaada fulani kwa watoto

wanaoishi katika mazingira magumu. Hapa Mhe. Spika, mimi baada ya kuiangalia takwimu hiyo nimesikitishwa mno na nimepatwa na mfadhaiko mkubwa, wa kuona jinsi wenzetu wanaoishi katika mazingira magumu walivyo.

Mhe. Spika, nikupe uthibitisho, tuangalie kiambatisho katika ukurasa wa 46 wa kitabu cha Mhe. Waziri. Hapa ametufafanulia hawa ambao wamepata misaada ya chakula watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu. Amewataja kwa upande wa Shehia za Unguja ni Kijitoupele pamoja na Mtopepo, na idadi ya watoto hao wote ni 274 kwa upande wa Unguja. Mhe. Spika, hizo ni Shehia 2 tu. Akaelekea tena Pemba akawapa msaada watoto katika Shehia 3 na idadi yake ni 384, hizo ni shehia 3.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwenye maneno yangu ya kwanza kwamba huo ustawi wa jamii umekwenda kwenye tatizo nene na pana mno. Kwa hivyo, niseme kwamba serikali sio wakati wake tena sasa wa kuiwachia Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, bali hili limekuwa ni tatizo la taifa, na ni lazima sasa mipango na utaratibu mzima upatikane wa kuona kwamba hali hii imekuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, jumla ya shehia hizo 5 ni watoto 662, hii ni idadi kubwa na ni shehia 5 tu. Kwa hivyo, ningeiomba serikali pamoja na wizara yenyewe, wakati wa zoezi la sensa litakapofanyika kuweza kuona kwamba inafanya hii *research* na kuwatambua rasmi watu hawa. Lakini sio kuwatambua tu, pamoja na kupewa misaada ya chakula ama sare, bali wawezeshwe ili waweze na wao kujikomboa kwa ajili ya kupata uwezo wa kuzalisha na kuweza kujikimu kimaisha. Vyenginevyo taifa hili, ile nia nzuri inayokusudiwa kwa ajili ya jamii ya Wazanzibari, kwa kweli itakuwa ni kikwazo na hatutofikia malengo.

Mhe. Spika, sasa niende katika ukurasa wa 30 kifungu cha 73 Idara ya Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri naelezea kwamba malengo ya wizara ni kuhakikisha kuwa Mabaraza ya Watoto yanafanya kazi katika wilaya zote.

Mhe. Spika, kwa upande wa suala hili niseme kwamba ni lazima Mhe. Waziri alitimize, kwani watoto wamejenga choyo kuona watoto au vijana wenzao wako kwenye mfumo huo wa Mabaraza, lakini wengine ukiwa hujawafikia basi ni kuwanyima haki zao.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba afanye juhudi pamoja na maarifa yake, tena namuelewa mama Zainab analiweza hilo na watendaji wake ni wazuri wanaweza hili. Kwa maana hiyo, ni lazima alikamilishe, ili watoto nao wajione kwamba wanashiriki na yeye anawatendea haki zao. *(Makofi)*

Nikiendelea katika suala hili pia Mhe. Waziri amezungumzia kuhusu kuwainua wanawake kiuchumi pamoja na kuanzisha Benki ya Wanawake. Mhe. Spika, ni kweli kabisa ipo haja ya kuwepo kwa benki hiyo, na muda mrefu wizara inaigusia na kuizungumzia. Lakini kimsingi ni wazi kwamba wizara hii kwa fedha ambazo inapatiwa kasma ya bajeti yake haimudu kuendeleza shughuli zozote zile kuweza kufungua hiyo benki.

Kutokana na hali hiyo, nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ashirikiane na mama Zainab, ili kuona wanawake wanakomboka nao kiuchumi kwa ajili ya kupatiwa mikopo, ambayo itaweza kuwaendeshea shughuli zao bila ya bughudha wala riba kubwa na kuweza kujipatia mitaji, ili kuweza kujikimu kimaisha.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo yale mazingira magumu hususan yanawakumba wanawake zaidi. Hivyo, wanawake hawa kama serikali itachukua juhudi za kuwawezesha, basi naamini kwamba wataweza kumudu na pengine inawezekana tatizo hili likapungua kwa asilimia kubwa, kwamba na sisi Zanzibar tunaishi na watoto ambao wako kwenye mazingira magumu. Kwa kweli ni haki yao wakombolewe, ili waweze kuishi kama wanavyoishi watoto wote duniani katika haki zile za kibinadamu.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 24 kifungu cha 61 kuhusu Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Spika, wenzangu wameyazungumza mengi na wala nisingependa niyarudie, lakini kwa kuwa tunaelewa ya kwamba vijana ndio nguvu kazi ya taifa. Taifa linahitaji kurithiwa, na sisi tuliomo humu tunamaliza muda wa uhai wetu, lakini vijana wanahitaji kutayarishwa na baadae kuweza kuja kushika nafasi hizi na kuliongoza taifa hili.

Kwa hivyo, nimwambie mama Zainab vijana wetu wengi wao kwa sasa wameelemea katika mambo ya dawa za kulevya kwa kukosa kazi. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anieleze kwamba anashirikiana vipi na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ili kuona tatizo hili wanalinasua na kuona vijana wanapatiwa ufumbuzi, na kwa wale wanaoingia kwenye *Sober Houses*, ili waachane na hali hiyo.

Kwa hiyo, watakapotoka kuna mpango gani, ili kuona wakati wanapotoka kule wanapatiwa miradi kwa ajili ya kuendelezwa, kwa lengo la kuachana kabisa na dawa za kulevya na hatimae kuweza kuwa vijana bora na wazuri na kuwa watoto wema katika taifa letu.

Mhe. Spika, kwa kuwa mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru na sasa tumsikilize Mhe. Hassan Hamad Omar na baadae Mhe. Kazija Khamis Kona.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kwa ajili ya kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala*, aliyenijaalia kuwa katika hali ya afya njema na kuweza kusimama katika Baraza lako hili tukufu, kwa ajili ya kujadili mambo ya nchi yetu.

Vile vile nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na watendaji wake kwa hotuba yake nzuri na iliyojaa maudhui ya kuwajenga watoto, vijana, wanawake pamoja na wazee. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu kwenye ukurasa wa 5 kifungu kidogo cha 6, Mhe. Waziri ameeleza kwamba kuhakikisha kuwa haki za watoto, wanawake, vijana na wazee zinafuatiliwa na kutolewa taarifa mara kwa mara. Kwa kweli hili ni jambo zuri na tunalipongeza sana, kwamba haki za watoto, vijana, wanawake pamoja na wazee zinafuatiliwa mara kwa mara na kutolewa taarifa.

Lakini niseme kwenye Haki za Watoto moja wapo ni kupata elimu, sasa kama ni elimu tujiulize maandalizi yetu ya kupata elimu ni mazuri, watoto wetu wanapata haki stahiki za elimu. Tukilijua hilo basi tutajua kwamba taarifa za mara kwa mara zinatolewa na ustawi wa jamii unafanya kazi katika haya.

Vile vile Mhe. Spika, katika haki za mtoto ni nyingi sana, ndani ya skuli zetu kuna haki za mtoto mpaka kwenye michezo, na mwenzangu hapa Mhe. Rashid Seif Suleiman amezungumza, kwamba ni haki mtoto kumjenga katika kumuimarisha kwenye michezo.

Lakini wakati mwengine inapelekea kuwadharau hawa watoto. Kwa mfano, mtu anaweza kufeli kimasomo na kupasi kimichezo, yaani amefeli kimasomo na kupasi kimichezo, lakini tunashindwa kuwaendeleza.

Mhe. Waziri husika, tunaomba kupitia kwako Mhe. Spika, wale vijana ambao ni watoto waliopasi kwenye michezo, basi tuwaorodheshe na tuwaendeleze, kwa sababu wanaziletea heshima skuli zao walizotoka, taifa letu na baadae kuwa wanamichezo wazuri sana.

Mhe. Spika, katika haki za mtoto ni kupata malezi bora. Sisi kama wazazi tunao wajibu wa kulea watoto wetu katika mazingira mazuri. Lakini inafika wakati mtoto tunamuadhibu kama mwizi au jambazi na hali hii si nzuri, kwa sababu mtoto anahitaji maelekezo mazuri kutoka kwa wazazi, na kila mtu analo jukumu kama mzazi na wala si lazima mtoto aliyemzaa mwenyewe, kwani mtoto yeyote wa mwenzako naye ni mwanao.

Kwa hivyo, Mhe. Spika mtu anaweza kupata tetesi tu kwamba mwanawe analo tendo ovu, basi akachukua hatua za makusudi na kumuadhibu vibaya. Kwa mfano, wazazi wengine wanasaga mpaka pilipili na kuweza kumtia mwanawe kwa kumuadhibu vibaya, na wengine wanawapiga kipigo cha mwizi kabisa, jambo ambalo halipendezi, kwa sababu mtoto anaweza kupotea na kuchukua shilingi mia moja tu, basi *Wallahi* anathubutu mzazi kama huyo kuweza kumzonga gazeti kwenye mikono ya mtoto na kuwacha moto.

Kwa kweli hii ni hatari na wala mtoto huyu hatakuwa na mazingira mazuri, mimi naweza kusema kwamba unamfundisha utundu.
Mhe. Spika, pia miongoni mwa haki za mtoto ni kumuendeleza na kumpa mafunzo ambayo ni mazuri. Haki hii itamjengea mustakbali mwema katika maisha yake. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 31 kifungu kidogo cha 4, hapa Mhe. Waziri ameeleza kwamba kuwainua wanawake kiuchumi pamoja na kuanzisha Benki ya Wanawake. Mhe. Spika, ni sawa wizara imekusudia vizuri.

Katika kuanzisha hizi benki, basi benki hizi zisianzishwe mijini tu hata na vijijini kuwe na *branches* zake, kwa sababu wanawake wa shamba ndio wenye kupata tabu sana kuliko mijini, kwani wanawake wa mjini ni wajanja sana, lakini vijijini ndio wenye kazi ngumu na wala mambo haya hawafaidiki nayo.

Kwa mfano, tukiangalia akinamama wamejishughulisha sana na mambo mazito ikiwemo kilimo na hata uvuvi wa mwani. Lakini bahati mbaya masikini ya Mungu hata wale waliotuahidi ndani ya Baraza lako hili tukufu kwamba watatafuta masoko ya mwani, ili kuboresha na mpaka leo bado hatujaona mwani kupanda bei na hili ni tatizo. Kwa kweli tukiwaangalia akinamama ndio wenye kulima mwani kwa wingi, yaani wanasikitisha sana, kwani kazi nzito na ukiwaona utawaonea huruma.

Kwa hivyo, tunaiomba Wizara hii ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, ili waweze kuwaandalia mazingira mazuri.

Mhe. Spika, napata tabu sana katika wizara hii na wanawake jinsi walivyotajwa hapa. Lakini kuna wanawake ambao wameachwa na waume zao na wengine wamefiliwa na waume zao. Kwa kweli watu hawa wanakuwa na matatizo makubwa sana, kwani mtu mwanamke anaweza kuachwa na mume wake na watoto wote akatupiwa, na *Wallahi* hana chochote cha kuweza kujisaidia na wala kitabu hichi hakijamtaja mwanamke wa aina hiyo na hayo ni matatizo.

Kwa hivyo, naomba kushauri hapa kwamba Mhe. Waziri awaone hawa, awe na kitengo au idara ambayo itakuwa ikiwashughulikia, kwa sababu wanawake hawa walioachwa na waume zao au waliofiwa na waume zao wanakuwa na wakati mgumu sana na wala si vibaya kuwatizama kwa jicho la huruma.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu haki za wazee. Mhe. Spika, tunaishukuru serikali yetu kupitia Ustawi wa Jamii kwamba imewajengea mazingira mazuri. Lakini na mimi nasema kama wenzangu waliopita na wala sipendi kurudia, isipokuwa naomba kusisitiza, kwamba wazee wamejengewa sehemu nzuri ikiwemo hapo Sebleni na wanapata mahitaji mazuri, lakini ni sehemu ya mjini tu.

Kwa kweli kama nilivyosema kwamba kama kitengo hiki kimekusudia kuwatizama wazee basi wote wawe na haki kama hizi, hivyo fungu hili la bajeti ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto liongezwe.

Kwa nini niseme hivyo Mhe. Spika. Kwa sababu zamani ilikuwa Serikali hii ya Mapinduzi, wazee wetu walikuwa wakipata *welfare* ijapokuwa ilikuwa ni kiasi kidogo cha fedha, lakini kwa kila kijiji ambacho kina mzee basi ilikuwa inamfikia.

Lakini baada ya kujengewa pale waliopata ni wachache tu, hivi tuseme kwamba vijijini hakuna wazee na wazee ni wa mjini tu, haiwezekani. Kutokana na hali hiyo, ni vyema kuwaangalia kwa fungu la huruma katika utaratibu wa kuwaangalia wazee vijijini kwetu wanakotoka.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu huu kwenye ukurasa wa 25 kuhusu haki za vijana kifungu cha 7, Mhe. Waziri hapa ameeleza kwamba kujenga uwezo kwa vijana kupitia Stadi za Maisha, Vita dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya.

Kwa kweli hapa tumekusudia kuwajengea stadi vijana, lakini ukiangalia nchi yetu ya Zanzibar asilimia 99 ni Waislamu, na nchi hii imepiga marufuku pombe za kienyeji. Lakini inaruhusu pombe za kizungu, ambazo wakifika huko na kuanza kuwapa basi na pombe nyengine zote watapata, na wala hapa hatuwezi kuwajengea uwezo vijana

wetu, kwa sababu mtu akishalewa hana lolote la kimaendeleo analolifanya, isipokuwa jeuri, ni vyema tuangalieni huko.
Mhe. Spika, tukiangalia vijana wetu hawa kuhusu vita dhidi ya UKIMWI pamoja na dawa za kulevya kuna hizi *Sober Houses*. Kwa kweli hizi tusifanye kuwacheka wala kuwakebehi, kwani *Sober Houses* ni sehemu wanazoishi vijana waliokuwa wakijishughulisha na mambo ya ulevi, na hivi sasa kuna majengo maalum ambayo wanakwenda kule kwa ajili ya kupata mafundisho na wanapotoka pale wanakuwa ni walimu wa wenzao.

Kwa hivyo, hawa tusiwajejee na wala tusiwakebehi hata kidogo, kwa sababu ni wengi ambao waliokuwa huko na tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kwamba wengine wametoka wakiwa salama na wanaendelea na shughuli zao za maendeleo.

Mhe. Spika, vijana hawa tukiwapa nyenzo basi watafikia hatua tunayoitaka, na watatoka katika mambo ya majanga machafu na watakwenda katika mambo ya maendeleo.

Vile vile tuzidi kuwapa elimu, kwa sababu dawa kubwa ni kuwapa elimu, ikiwa tunawapa elimu kila siku basi wataweza kuachana na mambo maovu na baadae kufuata mambo ya mafanikio katika nchi yetu hii.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 25 kifungu kidogo cha 3 kuhusu kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa. Mhe. Spika, huyu kijana ameekewa malengo katika mambo ya uratibu wa Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa.

Kwa hivyo, mimi niseme tu kwa uono wangu binafsi nasema kwamba, huu mwenge upo muda mrefu tangu *TANU* na *Afro*-Shirazi, lengo kubwa tunaambiwa kwamba unamurika maadui. Lakini tukiangalia hao maadui wapo kila siku na mafisadi wapo na wala sijaona tija yoyote, kwa sababu tunaambiwa kwamba unamurika maadui, lakini bado wapo.

Mhe. Spika, naomba niseme tu kwamba itafika siku mwenge unapita sehemu watoto skuli pamoja na wafanyakazi wanatoka na kwenda kuupokea mwenge, mimi nadhani jambo hili liende mpaka kwenye chama tu na ikifika siku yao wakaadhimisha, lakini linatupotezea muda sana.

Hivi tunasema kama mwenge unalinda amani, ni juzi tu Wazanzibari wasiopungua 38 waliteremka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume wakitoka Somalia, kwa mambo hayo ya kutoa amani wakae kipindi hiki na tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, nimpongeze Rais Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume na Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad kwa hatua tuliyofikia kwa juhudi zao. Hivi sasa nchi yetu ina amani ya kutosha na kama nchi ina amani ya kutosha, basi tukisema hatuna maendeleo tutakuwa watu wa maajabu sana.

Kwa kweli nchi ina utulivu na wala haina vita, amani ipo kwa nini tukose maendeleo, isipokuwa ni mipango mizuri tu ya kupanga na kuitekeleza, kwa sababu unaweza kupanga mipango, lakini kama hukuitekeleza na kuisimamia vizuri, basi itabakia kwenye mabuku haya.

Mhe. Spika, mimi naona kutowepo kwa mwenge hatuna hasara yoyote. Itafika wakati fedha zinazochangwa kwa ajili ya mwenge zipelekwe kwenye maendeleo mengine ni gharama kubwa.
Mhe. Spika, mengi ya kueleza tunayo, lakini kutokana na muda wako na umetuomba hapa tuchangie basi mimi kwa leo niishie hapo. Kwa hivyo, naunga mkono hoja au hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunakushukuru na sasa nimkaribishe Mhe. Kazija Khamis Kona na baadae Mhe. Farida Amour Mohamed.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Nianze na mchango wangu kwenye ukurasa wa 2 kuhusu pongezi. Mhe. Spika, hapa Mhe. Waziri ametoa pongezi wa Mhe. Rais kwa kuiondoa ile ada ya kulipia kwa akinamama wanaokwenda kujifungua katika hospitali za serikali. Vile vile na mimi nampongeza Mhe. Waziri kwa hili.

Lakini kidogo nimeshtuka hapa Mhe. Spika na nitamuomba Mhe. Waziri, ili sote tulijue, kwa sababu hapa naomba ninukuu kidogo Mhe. Spika. "Hili ni jambo zuri, ambalo ni kubwa tena la faraja, kwani litapunguza vifo kwa akinamama na watoto". Sasa hapa kila nikifikiria na kujishauri nasema kumbe hizi fedha tulizokuwa tukilipia sisi wazazi akinamama kwenda kujifungua zilikuwa zikisababisha vifo vya akinamama na watoto najiuliza hili?

Kwa hivyo, hapa Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, kwa sababu Mhe. Rais alitoa tamko hivi karibuni kweli, lakini hapa namuomba Mhe. Waziri, yaani tokea tulipoingia kwenye mfumo wa Umoja wa kitaifa atuletee takwimu akinamama wangapi wamejifungua Hospitali za Serikali ambao wamefariki pamoja na watoto.

Vile vile atuletee takwimu mwaka 2013 bajeti ijayo, ili tuweze kulinganisha na tujue ni kweli hizi fedha zilikuwa zikichangia nazo au vipi? Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri suala hilo aje anipatie maelezo.

Tukiendelea hapo kwenye ukurasa wa 3 kifungu 7, ambacho kinazungumzia kwamba wizara inaishukuru na kuipongeza Serikali ya Mapinduzi kwa kufanikisha zoezi na kuwafariji na kutoa misaada kwa wahanga wa ajali ya Meli ya *Mv. Spice Islander*.

Mhe. Spika, kwanza niishukuru serikali na mimi kwa kuwajali wale wahanga. Lakini katika ajali ile Mhe. Spika walikuwemo watoto nao pengine wamepoteza familia zao mule na watoto wao wamepona. Sasa je, namuuliza Mhe. Waziri kama yeye ni Waziri wa Wanawake, Watoto na Vijana, aliwasaidia nini watoto hawa waliopona katika ajali ile. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anijibu swali langu kwa kina kabisa. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 11 kifungu cha 24, na hapa naomba kidogo ninukuu Mhe. Spika. "Aidha wizara imo katika hatua ya kufanya utafiti wa omba omba, ili kuangalia kiini cha tatizo hilo". Mhe. Spika, naomba hapa hakuna haja ya kufanya utafiti hii wizara, kwa sababu utafiti upo wazi kwamba watu wetu wanaombaomba kutokana na umasikini Mhe. Spika, tena kiini gani chengine na kiini ndio hicho Mhe. Waziri.

Kwa hivyo, hapa labda afanye utafiti huo, na Mhe. Spika naomba kutoa ushauri kama ataukubali Mhe. Waziri, ni asilimia ngapi wanawake, vijana na walemavu wangapi wanaojishughulisha na kuomba omba, kwa sababu na walemavu wamo mule utawaona wamekaa na wizara inayoshughulikia masuala ya walemavu ipo na sijui inawasaidia nini walemavu wale, ambao ni masikini ya Mungu, jamani *Toba* ya *Yarabi*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuendelea tena kidogo na wala sitochukua muda wako mkubwa, kwani sina mambo mengi na yote yameshazungumzwa, isipokuwa wizara hii inahusika na watoto, vijana na wanawake.

Kwa hivyo, hapa nimuombe Mhe. Waziri au nimuulize swali kule vijijini tofauti na huku mjini, kwa sababu vijijini tuna mazingira magumu hasa Wilaya yangu Mhe. Spika, kwamba kule kuna watoto wanaojishughulisha na ajira ndogo ndogo, ili wapate manufaa.

Sasa sijui wizara yake Mhe. Waziri inawaangalia vipi na watoto wale wanaojihusisha na ajira si kama kwa kutaka, isipokuwa kutokana na hali ya maisha ya wazee wao. Kwa hiyo, sijui Mhe. Waziri hawa nao atawafikiria vipi, watoto hawa pamoja na familia zao, kwa sababu Wilaya ya Kaskazini 'A' na Micheweni kila nikisikia zinaongoza tu. Kwa mfano, ukija kwenye watoto wasio na *vitamin* B, wenye mazingira magumu, wanaojihusisha na ajira Wilaya ya Kaskazini 'A'.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwamba na sisi atufanyie utaratibu, ili tuondokane na masuala haya au serikali kwa jumla, yaani kila kitu tuko nyuma. Kutokana na hali hiyo, tunaiomba serikali ituendeleze na sisi, ili tuonekane kwamba tuko juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jambo la mwisho la kumalizia ni kuisisitiza tu serikali kwamba hii Benki ya Wanawake itaanza lini, ili na sisi wanawake tuondokane na umasikini hasa wanawake wa vijijini kule, kama vile Matemwe, Kijini, Kigunda na sisi tutajisikia tuko katika hali ya faraja.

Kwa kweli hii benki tunaomba tuondokane na kuhadithiwa kwenye vitabu, hivi sasa tuone kwamba utaratibu wa kuendelezwa hii benki na bajeti inayokuja tuambiwe hii benki iko tayari, akinamama mnatushajihisha na sisi

tunashajihisha akinamama wenzetu waende wakajiunge kwenye benki, wachukue mikopo, ili wafaidike nao kiuchumi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, na mimi naunga mkono bajeti hii. Lakini namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anijibu lile swali langu la mwanzo, vizuri tena kwa kina. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa tumsikilize Mhe. Farida Amour Mohammed na baadae Mhe. Marina Joel Thomas.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuzungumza machache katika hotuba hii ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uwezo na afya njema ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuchangia machache.

Pili naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake hii nzuri kwa kina na umakini sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze mchango wangu moja kwa moja, kwa sababu wanawake ndio wengi lakini sasa riba ni kubwa mno katika mikopo hii Mhe. Spika, ukiangalia badala ya kuwaondolea mzigo wanawake hawa tunawaongezea mzigo mkubwa mno. Mpaka wanafika wakati wanakata tamaa na wanashindwa kuendeleza vikundi vyao kwa sababu mapato yao bado ni madogo. Kwa imani yangu ninavyohisi naomba nikwambie Mhe. Waziri, utafute mbinu hasa ya makusudi ya kuwakomboa hawa wanawake.

Kwa ushauri wangu naomba mashirikiano yako pamoja na Waziri wa Fedha, Uchumi na Maendeleo, jamani tuanzishieni hii Benki ya Wanawake, hichi kimeshakuwa kilio kikubwa kama ilivyokuwa Wizara ya Afya na ICU. Inazungumzwa kila siku lakini bado haijafikia mwisho. Zanzibar ni nchi iliyoungana hebu watu mambo mema huiga, mambo mabaya huyaacha, hebu namuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yako na taasisi zote zinazohusika tuwaige wenzetu wa upande wa pili. Tanzania Bara tayari wameshaanzisha hii Benki ya Wanawake, wenzetu wanafaidika. Naomba sana Mhe. Waziri hili ulizingatie. Wanawake itakapoanzishwa benki hii na kupata mikopo basi nina hakikisha yatapungua yote hayo yanayoambiwa ya omba omba na mambo mfano wa hayo. Hapa tayari watakuwa tayari

Mhe. Spika, kwa vile masuala mengi watu wameshayazungumza nataka nije moja kwa moja kwenye suala la ajira kwa watoto. Watoto kuna wa aina tatu, hapa kabla ya yote kwanza naomba nimshukuru na kumpongeza marehemu muasisi wetu Mhe. Abeid Amani Karume, kwa dhati kabisa kwa kuanzisha hivi vituo vya kulelea watoto. Kwa njia moja au nyengine wazazi ndio siye, mtu pengine anazaa mtoto pengine anaona maisha magumu au pengine kwa roho yake tu ilivyoharibika anachukuliwa mtoto anakwenda kutupwa. Watoto wale waliokotwa okotwa zamani na wengine waliokuwa maisha yao ni magumu wakenda wakawekwa katika eneo moja ikawa maisha yao yanakwenda vizuri. Walikuwepo Forodhani baadaye muda mrefu serikali ikaamua kuwahamisha pale na kuwapeleka katika maeneo mengine.

Mhe. Spika, tumpongeze mama Shadiya alifanya kazi nzuri kwa kuweka kituo kile pale Mazizini na kuwalea hawa watoto. Nataka nimuulize Mhe. Waziri na atakapokuja hapa atupe jawabu sahihi. Nimeona katika kiambatanisho chake hapa kwamba kutembelea vituo vya kulelea watoto Unguja na Pemba. Katika mtazamo ninavyohisi hivi vituo vya kulelea watoto hasa vya serikali sivioni. Nakuomba Mhe. Waziri utuambie ni lini utafanya utaratibu wa uhakika wa kutuletea vituo hivi vya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu Unguja na Pemba sio Unguja peke yake na Pemba pia tunataka tuone kuna kituo pahala gani.

Kwa sababu katika pahala pana watoto wanaoishi katika mazingira magumu ni kisiwa cha Pemba. Kuna watoto wanaishi katika mazingira magumu halafu hawana pahala maalum pa kuwaweka hawa watoto ili wakaenziwa. Vituo vingi ulivyovitaja katika kitabu chako ni vituo vya watu binafsi, wale ni watu wanahiyari zao, wale wanaolelewa mle wanalelewa kwa pesa. Wengine wazazi wao ni masikini, wale wana masharti yao, wengine yale masharti yanawashinda. Lakini pakiwa ni kituo cha serikali cha kulelea watoto wetu basi pale tutapata mafanikio na kwa Mwenyezi Mungu pia tutapata fungu kuwalea watoto wale waliokuwa katika mazingira magumu.

Mhe. Spika, naomba niingie katika suala la Ustawi wa Jamii, ingawa wenzangu walizungumza sana kwamba ustawi unakusanya mambo mengi. Hapa nije kwenye wazee. Wazee wetu ni wengi na vituo vya kulelea wazee hasa vilivyotajwa humu ni vituo vitatu mpaka vinne. Pemba kuna limbani na kuna na Gombani na Unguja kuna Sebleni kuna na Welezo. Lakini nataka nikwambie Mhe. Waziri, wazee hawa waliokuwemo ndani ya vituo hivi ni robo tu ya wazee waliokuwemo katika maisha magumu kupindukia. Ambao kuwa wanataka wasaidiwe kwa hali na mali. Gombani kuna wazee wanne kama sikosei na Limbani kuna Wazee 15. Hebu tujiulize Mhe. Spika, wazee hawa kwa Pemba tuseme ndio wote hawa wanaohitaji kusaidiwa. Mhe. Spika, wazee wapo wengi.

Mhe. Spika, katika wazee hao hao kuna wazee wale ambao wanaosaidiwa shilingi 5,000/-pesa ile nafikiri inakwenda katika Afisi ya Tawala za Mikoa naona kama ni Mhe. Mwinyi Haji. Naomba Mhe. Waziri pesa hii wanayopewa kwa nini haingizwi huku moja kwa moja katika Ustawi wa Jamii tukaiona bajeti yake hasa wenyewe wanavyopewa. Kwa sababu zile pesa siye tunaziona tu kule tukenda kwenye Tawala za Mikoa, huona kama kuna pesa fulani wamepewa wazee, shilingi elfu tano tano. Sasa ile bora ingeingizwa hapa kwa sababu hii ni wizara yako, ikawa ni kazi rahisi ya kuwakusanya hao wazee, kwa sababu wewe ndio mwenye hawa wazee.

Mhe. Spika, wazee hawa wanaopewa shilingi elfu tano tano, wanapata tabu kubwa, kwa sababu wazee wengi wanaishi vijijini. Mtu anatoka kijijini anakwenda kuchukua pesa ile Mawilayani. Pengine yeye mwenyewe hafiki pale peke yake lazima apate mtu wa kumuongoza pamoja na nauli. Hiyo elfu tano itafanya nini mpaka aende kule akachukue na mtu ndio akaichukue. Kwa nini hamuandai *program* maalum ya kuwafata wale watu angalau kwenye shehia zao. Naomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri mliangalie hilo, waangalieni wazee hawa mnaowasaidia, ile elfu tano ni kubwa mtu hawezi kuiacha kutokana na hali yake ngumu aliyonayo ya maisha. Lakini kuifuata Wilayani pesa ile ni usumbufu, itakuwa yeye hana chochote kitakachobakia, hebu wasaidieni jamani.

Mhe. Spika, halafu nakuomba sana Mhe. Waziri hebu kaa ufanye utafiti ujue hasa hawa wazee baada ya hawa waliokuwemo ndani ya maeneo maalum ya kulelea, kama Sebleni, Gombani na Limbani, hawa waliokuwepo nje waliokuwa na mazingira magumu kupindukia utufanyie tathmini uwajue hasa ni wangapi, halafu utatafuta njia nyengine ya kuwasaidia.

Mhe. Spika, nikija kwenye suala la walemavu ambalo kuwa limo humu. Nimeona katika kiambatanisho kuna kesi nyingi za watu waliodhalilishwa. Lakusikitisha tunakuta humu kuna wale watu waliodhalilishwa au waliofanyiwa vitendo viovu. Lakini bado Mhe. Spika, hatujawahi kuona kesi zilizohukumiwa katika hili, hawa wenzetu bado wataendelea kuwadhalilisha hawa watoto walemavu. Wenzetu walemavu na wao ni binaadamu kama siye, ulemavu ule hawakuuomba. Leo wao, kesho miongoni mwetu Mwenyezi Mungu atusaidie, lakini anaweza akampa ulemavu mtu mwengine yeyote. Sasa kama tutakuwa wale tunawanyima haki zao, tutakuwa hatujawatendea haki kiukweli. Jamani wanaofanya makosa wahukumiwe hadharani tuwaone, wasifichiwe kwa nini wafichiwe.

Mhe. Spika, inasikitisha Mhe. Waziri, watu wazima, wanaakili zao timamu, wanaojua kutaka na kukataa wamo, kwa nini mtu akamuingie mlemavu kwa shida gani. Inauma Mhe. Waziri, nakuomba sana katika hili, wasaidieni jamani wenzetu walemavu. Halafu Mhe. Waziri kwa kumalizia nataka nikwambie kitu kimoja muhimu. Nimekupongeza sana kwa dhati kwa kazi yako kubwa uliyoifanya. Lakini nataka nikwambie Mhe. Waziri una kazi kubwa sana ya kuwaelimisha wanawake juu ya kujua haki zao. Baadhi ya wanawake hawajui haki zao za msingi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Katiba na Sheria, uandae ratiba maalum ya kupita mitaani au kwenye Mashehia au Wilaya kwa kuwaandalia Semina wanawake au mafunzo maalum ya kuwaeleza na kuwaelimisha juu ya kujua haki zao za msingi. Kwa sababu kuna mwanamke pengine atatokezewa na tatizo lakini hajua zile nyia za kupita. Sasa kama hujaenda wewe ukawaelekeza kujua namna ya haki zao, haki hii utaipatia huku itakuwa si rahisi na haya yote ni majukumu yako Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nasisitiza sana Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha Benki ya Wanawake jamani ndio mkombozi wa mwanamke wa Zanzibar. Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mimi nitachangia katika maeneo kama manne.

1) Kuhusu ada ya uzazi ambayo hili linawagusa moja kwa moja akina mama.

2) Kuhusu kupata milo mitatu kwa wazee wanaokaa katika nyumba za Wazee Sebleni.

3) Uwanzishwaji wa Baraza la Vijana.

4) Kuhusu Benki ya Wanawake. Hili limezungumzwa sana nahisi sitokwenda ndani sana.

Kwanza napenda kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuondosha hii adha ya Wazazi ambayo imewakomboa kwa kiasi kikubwa akina mama. Napenda kutoa msisitizo kwa wale ambao wahudumu katika sehemu hii ya Wazazi. Kuondoshwa kwa ada hiyo kusiwafanye wahudumu hao wakawahudumia vibaya wazazi hao. Inawezekana pengine kupunguzwa kwa ada hiyo wakachukua fursa na wao wawahudumie vibaya wale wazazi. Naomba niwasisitize kwamba ada imetolewa lakini wahudumu wawahudumie vizuri wazazi hao ili waweze kuwafanyia huduma hiyo kwa vizuri.

Jengine kuhusu suala la milo mitatu kwa wazee wanaoishi katika nyumba za Wazee Sebleni wengine Welezo. Hii pia nampongeza Mhe. Rais kwa kuamua kwa makusudi kuwasaidia wazee hao. Wale ni wazee wetu, wanahitaji huduma hiyo na hawana wa kuwasaidia. Hapa pia nasisitiza kwa wale waliopewa kazi hiyo ya kuwahudumia wazee, wawahudumie ipasavyo, wawapikie chakula chenye lishe nzuri, sio wamepata fursa hiyo ya kuwasaidia wazee wale labda wawapikie kila siku maharage, sembe, wale wanataka afya na wanataka matunzo. Kwa hivyo, nasisitiza kwa wale wafanyakazi ambao wanawahudumia wazee wale wawahudumie kwa moyo mkunjufu ili wapate lishe bora, wapate na nguvu zaidi.

Jengine ni kuanzishwa kwa Baraza la Vijana. Vijana wetu wengi wao hawana ajira kwa hivyo wanaweza kujihusisha katika mambo mbali mbali ambayo yanaweza kuwahatarisha maisha yao, pengine uvutaji bangi, wizi, dawa za kulevya n.k. Kuanzishwa kwa chombo hichi cha Baraza la Vijana kitawasaidia vijana wengi kukaa pamoja kujadili changamoto zao, matatizo yao na kupanga mikakati yao mipango ambayo itaweza kuwasaidia kujiajiri wenyewe katika kuendeleza maisha yao. Hivyo namuomba Mhe. Waziri katika suala hili litakapoanzishwa Baraza hili, naomba Baraza Mhe. Waziri uwawezeshe wapate mafunzo ili waweze kujiajiri wenyewe na kuepuka vitendo ambavyo vinaweza vikawahatarishia maisha yao.

Mhe. Spika, jengine ni suala la Benki ya Wanawake ambayo limezungumzwa na wenzangu wengi. Hili pia Mhe. Waziri napenda nimpongeze kwa sababu chombo hiki kitawakomboa wanawake kiuchumi, wanawake wengi hawana ajira. Wakipata Benki hii ina maana watapa fursa ya kukopa na kuanzisha biashara ndogo ndogo ambazo zitawawezesha kuinua maisha yao na hatimae kuondokana na umasikini. Na hata akina baba nao itawasaidia kutokana na kwamba mkiwainua akina mama na akinababa nao pia mnawainua.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba kuzungumzia haya Mabaraza ya Wilaya. Mhe. Waziri haya Mabaraza ya Wilaya kuna baadhi ya changamoto ambazo zinawakabili. Mabaraza haya yanafanya kazi nzuri na wanakuwa wanapanga mipango yao kazi ambayo wanakosa fedha za kuendeleza mipango yao ya kila siku, jambo ambalo linapelekea kutokuwa na ufanisi katika Mabaraza hayo. Namuomba Mhe. Waziri katika hilo ayaangalie vizuri mabaraza na ayawezeshe ili watoto wakae pamoja kujadili changamoto zao, kujadili matatizo yao ili kuweze kupatikana kwa ufanisi wa kazi zao.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana na Wanawake. Pia nianze kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, nimpongeze Afisi Mdhamini Pemba pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi zake na utekelezaji wake wa kazi akiwa ni Afisa Mdhamini Pemba.

Mhe. Spika, kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kumteuwa Mhe. Zainab kuwa Waziri wa Wanawake wa Ustawi wa Jami, Maendeleo ya Vijana. Mimi kwa kumsaidia Mhe. Waziri kwa sababu imeguswa Wizara yangu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo alipochangia Mhe. Rashid Seif. Amezungumzia kuhusu michezo ya riadha kwa vijana. Nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kuwa michezo ya riadha inaendelea maskulini na sehemu nyengine tofauti.

Jengine limezungumziwa kuhusu wanawake kuwa wanauzito mkubwa kuwa hawafanyi mazoezi. Hilo namuomba Mhe. Mwakilishi aangalie kwenye vilabu vingi vya michezo ni wanawake na tukiwemo sisi Mawaziri na Manaibu Waziri, hilo namuhakikishia kama lipo na linaendelea kwa juhudi zote kwa Unguja na Pemba.

Pia nende kwenye SACCOSS kwa kweli zimeasisiwa mwaka 2001, SACCOSS hizi za wanawake kwa kweli zimetoa viongozi ambao ni Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Madiwani na Masheha. Kwa kweli nawahakikishia wanawake wenzangu wa Kizanzibari kama wanawake tunaweza na miongoni mwa SACCOSS hizi zimezaa matunda makubwa sana kwenye visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye bajeti hii niende kwenye uzalilishaji wa kijinsia. Kwa kweli Mhe. Waziri amejitahidi kwenye Mikoa yote mitano, kwenda kipembe hadi kipembe kufatilia masuala haya yanayotendeka kuhusu uzalilishaji wa kijinsia, kuhusu wanawake, walemavu, watoto kwa kweli anafuatilia kwa hali na mali na anajitahidi sana Mhe. Waziri wetu tumpe hongera kwa juhudi zake hizi anazozifanya.

Mhe. Spika, kwa kweli niendelee kwenye benki ya wanawake. Naipongeza sana serikali kuona benki hii ya wanawake itakuwepo kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha na kushirikiana pamoja na serikali pamoja na Mhe. Waziri anayehusika na Wizara hii ya Wanawake na vijana na kadhalika. Kwa kweli hili suala hili serikali imelitupia macho sana kwa upande wa wanawake na nawambia wanawake wenzangu tuwe tayari kuja kuchukua mikopo, lakini mikopo hiyo tunapoichukua tulenge lengo kuu ni nini. Lengo kuu ni maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kwa sababu nimezungumzia mambo ambayo yananihusu kwenye Wizara yangu pia nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi tuwe tayari kufanya mazoezi tukiwa ni wanawake na wanaume ili kupunguza uzito na kupata afya bora.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na Mhe. Waziri nakushukuru sana, mimi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, kwa hotuba yake ambayo ameiwasilisha juzi kwa kweli ina muelekeo mkubwa sana kwa jamii yetu.

Mhe. Spika, kwa upande wa taasisi yangu nataka vile vile niwapongeze Waheshimiwa Wawakilishi wote wanawake na wanaume waliochangia katika suala zima la uanzishwaji wa Benki ya Wanawake. Naomba kidogo na mimi nitoe ufafanuzi katika eneo hili.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Waziri katika hotuba yake, tayari muelekezi yupo anafanya tathmini ili kutusaidia sisi serikali Benki hiyo inaanzishwa kwa utaratibu upi. Kwanza nataka niwambie Waheshimiwa Wawakilishi kwamba katika kuanzisha Benki kima cha chini cha kuanzisha Benki ni bilioni 15. Lazima hapa tuweze kupata mshauri ili aweze kutusaidia na kutushauri kwamba benki hiyo tunaianzisha kwa utaratibu gani. Hivi bilioni 15 tunazipata kwa kuuza *shares* au tunazipata kwa kutolewa na serikali au tunazipata kwa kuuza *shares* kupitia mashirika halkadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme tu kwamba waheshimiwa Wawakilishi waiyamini serikali yao na tupo katika hatua za kuangalia uwezekano wa kuanzisha Benki hii. Sisi tunaelewa sana kwamba Benki hii itawanufaisha na itawasaidia wanawake na sio wanawake tu hata wanaume wanaruhusiwa kuweka katika Benki hii na kukopa katika benki hii, lakini zaidi itakuwa ni ya wanawake katika maendeleo yao.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba Waheshimiwa Wawakilishi bado waendelee kutuamini na kuanzisha Benki sio suala la kukaa usiku mmoja, siku ya pili yake ukasema tayari. Kuna wengine hapa walimuuliza Mhe. Waziri kwamba mwaka jana ulituambia hivyo hivyo na mwaka huu unatwambia hivyo hivyo inaweza ikachukua hata miaka miwili, mitatu na hata minne katika suala la uanzishwaji wa Benki.

Mhe. Spika, katika kuanzisha benki ni lazima uangalie wenzako nyenzo zao ni zipi na wewe nguvu zako utakazoziingiza ni zipi. Sasa hivi tuna mabenki karibu 11 hapa Zanzibar, ukianzisha benki hivyo ujue kwamba una

ushindani wa Mabenki 11. Ni dhahiri kwamba lazima tuelewe hayo yote na ndio maana tukamuweka huyo mshauri muelekezi ili kutufanyia tathmini tuone tunafanyaje.

Mhe. Spika, mimi nikuwa nataka kuchangia hilo tu, lakini vile vile nimalizie kwa kusema kwamba naiunga mkono hotuba hii na bajeti hii ya Mhe. Waziri mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kutoa shukurani na kumpongeza Mhe. Waziri wa Ustawi wa jamii ambaye ni Wizara kaka ya Wizara ya Afya. Kwa kweli mara nyingi matatizo yake huishia Afisini mwangu nikayapeleka kwake. Kumezungumzwa mambo mawili matatu hapa ambayo yanakwenda huku na huku. Ningeanza na lile la kutunza watoto.

Kuna wengine wamezungumza watoto katika hali ya uchanga wao na kuna wengine wamezungumza watoto katika hali ya kulelewa. Ni vizuri niwaeleze Wajumbe kwamba tangu kitoto kinapokuwa kwenye mimba ikishatunga tu mpaka miaka mitano ni dhamana ya Wizara ya Afya, akizidi miaka mitano ndio ulezi huo unaanza kuingia kwa Mhe. Waziri wa Wanawake. Lakini mtoto anapopata matatizo katika daraja yoyote ile bila ya shaka Wizara ya Ustawi ndio inayohusika. Tunapozungumza lishe inawezekana lishe ikawa ipo Wizara ya Ustawi na inawezekana lishe ikawa ipo Wizara ya Afya.

Sisi katika wizara yetu tunajaribu na nitakaposoma hotuba yangu pengine kesho au leo mchana, itategemea na hali itakavyokuwa kipo kifungu cha lishe tutakieleza yale tunayofanya na tunayotakiwa kufanya. Moja katika hoja inayostahiki ni kwamba kumekuwa na tabia ya kumtizama mtoto mdogo na afya yake ya lishe baada ya kuzaliwa. Ilikuwa tumtizame mtoto mdogo katika afya yake tangu mama mjamzito ana mimba apate lishe nzuri yule mama, alishwe vizuri, alee mimba yake na ndipo atazaa mtoto mwenye afya.

Mhe. Spika, uzoefu niliokaa mwaka mmoja Wizara ya Afya mara nyengine unakwenda unamkuta mama mjamzito kwenye wodi yule mama mwenyewe unaona kama ile mimba imemuelemea kama sio lile tumbo lililojaa kile kitoto ule mwili haupo. Kwa hivyo hili linakuwa ni tatizo hata kabla ya yule mtoto hajazaliwa. Sisi kwa hivyo tunaitizama lishe sasa tangu mtoto atakapokuwa tumboni. Ili akizaliwa akiwa na afya nzuri ndivyo inawezekana akaweza akatimiza miaka mitano salama.

Naomba niwambie kwamba juzi kulitokea kitu *very interesting pale Washington,* hoja ilikuwa ni ya mama na mtoto, lakini yule aliyeanzisha mpaka ule mkutano kukamilika ni yule msimamizi wa USAID akahakikisha kwamba viongozi wakubwa wote wale pamoja na mama *Hilary Clinton* kwamba wakija pale waje na picha zao walipokuwa umri wa miaka mitano. Hapo ilikuwa *very interesting* maana vyengine ukivitizama ile picha na alivyosasa anaitwa mama mkubwa hata hailingani. Kilichokuwa kikisisitizwa kama sisi tumewahi kuvuka Mhe. Spika, mimi na wewe tumevuka hapo, leo ndio maana tunaitwa Mawaziri. Basi tujitahidi angalau na vitoto vivuke miaka mitano. Nategemea kufanya Semina na mimi nikwambieni mlete picha zenu za miaka mitano tuzione zilivyo.

Nilitaka hilo nilieleze kwamba dhamana hizi zimegawika katika Wizara mbili, Wizara ya Afya inastahiki kumtunza mtoto anapokuwa mchanga mpaka miaka mitano. Baada ya pale tena inaanza kuwa ustawi. Lakini huwa wanakuja Wizarani kwangu mtu ana vitoto vitatu, vinne, ananambia Mhe. Waziri naomba msaada wako. Namwambia fuata hii barabara ukipita hiyo Mahakamani kwa chini huko, kabla hujaifika ile *cross* unayokwenda pwani utakuta Wizara imeandika, hili ulokuja nalo ndio dhamana yake yule Mheshimiwa, kwa hivyo hilo nilitaka nilieleze hivyo.

Na ada za uzazi, nalo ni suala ambalo liko kwenye dhamana yetu nitalizungumza pale nitapozungumzia Wizara ya Afya.

Lakini Mhe. Spika, suala kubwa ambalo nilitaka nilichangie ni hili la udhalilishaji. Sisi na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto tumepewa dhamana ya kuweka kituo pale Hospitali ya Mnazi Mmoja kinaitwa *One Stop Centre*, kimeanzishwa nadhani mwaka jana kwa mashirikiano, sisi tuna madaktari wetu pale zinapokuja zile kesi kuzishughulikia tunashughulikia pamoja na watu wa polisi na mtu kutoka Idara ya Ustawi, tumeimarisha mafunzo katika daraja ya kituo na Pemba kule nako tunataka kuanzisha, tumesomesha watu tunataka kwenda kwenye hospitali za mashamba na mwisho tutakwenda katika daraja mpaka Hospitali za Wilaya jinsi ya kufanya uchunguzi kesi zile zinapokuja pale.

Limezungumzwa hapa suala la umuhimu wa *DNA* kwa ajili ya uchunguzi huo. Nakumbuka karibuni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alifanya ziara Marekani pamoja na naibu wangu, moja katika mafanikio waliyopata ni kwamba tutasaidiwa kile chombo cha *DNA*. Kama nakumbuka wiki tatu nyuma kulikuwa na ujumbe uliotoka huko ukaja kumuona Mhe. Makamu wa Pili kueleza hatua iliyofikia. Nilivyoelezwa na Naibu Waziri wangu na wale watu wengine ni kwamba huenda ikawa hilo kontenda likawa kwenye *high seas* ambalo tunaweza kupata hicho kifaa cha *DNA* kikatusaidia.

Lakini kwa kweli si kifaa rahisi ni kifaa ghali pamoja na kwamba serikali inahimizwa kununua lakini ni ghali, si ghali kukinunua tu, ghali kukitunza na si ghali kukitunza tu Mhe. Spika, kinahitaji utaalamu wa hali ya juu sana. Kwa sababu Mhe. Waziri hapa alikuwa ananiuliza hivyo *forensic evidence* ndio inakuwa vipi? Namwambia hii ni moja katika utaalamu unaotakiwa kutumika kwenye *DNA*, kama kuna mhalifu amefanya kitu akasahau chochote pale ukapatikana unywele mmoja tu Mhe. Spika, basi ukenda kuwekwa huko kwenye *system* ikitolewa na yeye damu yake anaambiwa bwana mkubwa huna vya kukataa, huu ni unywele tuliyoukuta kulikotokea tendo, huu unywele ni wako tizama matokeo hayo hapo. Kwa hivyo, ni kifaa muhimu sana lakini kinahitaji utaalamu wa hali ya juu, Mwenyezi Mungu atujaalie atuwezeshe na wale watakaotuletea wamesema watatupa mafunzo ya kukiendesha.

Sasa Mhe. Spika, suala nililotaka kulieleza hapa pana barua ambayo naomba uniruhusu niisome iliyotoka kwa Dr. Jamala A. Taib, huyu ni Mkurugenzi wangu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Barua hii kaiandika tarehe 2 Julai, 2012 anamuandikia Katibu Mkuu wa Ustawi wa Jamii hali tulivyo pale Hospitali ya Mnazi Mmoja na masuala ya udhalilishaji anasema hivi,

"Kujitokeza kwa matukio ya ubakwaji wa watu kwa hadaa katika majumba ya Michenzani, tafadhali husika na mada ya hapo juu, kumejitokeza na tabia ya watu wasiofahamika ambao hujiita Polisi Jamii kila jema tunalolijenga watu wanalitafsiri vibaya, wanalitumia vibaya. Hujiita Polisi Jamii kuwahadaa watu na kuwapeleka varanda katika majumba ya Michenzani na kuwalazimisha kufanya ngono kwa nguvu, kuwabaka kwa lugha ya sasa. Hadi hivi sasa zimesharipotiwa kesi tano katika Kitengo cha Mkono kwa Mkono (*One Stop Centre*) wakiwemo wanafunzi watatu wanawake na wengine ni wake za watu katika mwezi wa Mei na Juni.

Kwa barua hii tunaleta taarifa kwako kwa hatua za haraka kudhibiti tabia hii mbaya ya ubakaji na pengine kuwapa maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa makusudi. Nategemea mashirikiano ya haraka kulitatua tatizo hili".

Huyu Mkurugenzi wangu anamwambia huyu, sasa huu ni mtindo mpya, kama watu wakibakwa mitaani sasa wanabakwa kwa hadaa ya Polisi Jamii na huwa wanakwenda pale kwenye bustani, si kuna tabia ya wanafunzi wengi wanakaa masikini pale kwenye bustani karibu na *Haile Selassie* pale. Siku hizi pale ni kama *library* wanafunzi huwa wanakusanyika kujisomea na kusaidia kupata mjadala wa masomo. Sasa Polisi Jamii iliyokuwa na tabia mbaya ya ajabu wameanza kugeuka kwamba pale ndio lindo lao.

Kwa hivyo, kwa kupitia nafasi hii Mhe. Spika, nnahakika kuna watu wanatutizama kwenye *screen*, tunaomba kutoa taarifa hiyo kuchunga watoto wao. Anapokujia mtu kukwambia yeye ni polisi jamii mwambie polisi jamii haniulizi barabarani ananiuliza huko mtaani na yeye ikiwezekana aripoti. Ni vizuri hawa wakakamatwa tukaweza kuepukana na balaa hii.

Si hivyo tu, lakini kuna ofisa wetu wa hiki kituo anasema ni hatari jinsi ya yale mambo yalivyoongezeka, yaani kesi zinazokwenda za ubakaji na udhalilishaji pale kwenye kituo ni nyingi mno. Anasema, ama hii kidogo ilinishitua, si chini ya mia kwa mwezi, sisi tuko kimya kila mmoja na safari yake yule kaingia, yule kaja Baraza la Wawakilishi yule kenda shamba kulima, kuna wengine wao wanafanya uharibifu, sasa hao wanatoka wapi Mungu anajua lakini tujitahidini na watoto wetu. Yule *staff* wetu amechanganyikiwa kwamba hali hii sikawaida isiwe kuna watu wamekuja kutufanyia fujo kusudi kutuharibia jamii yetu.

Mhe. Spika, nilitaka kuchangia hayo ili kuihadharisha jamii na kumsaidia Mhe. Waziri kwamba suala la ubakaji si suala la Wizara ya Ustawi wa Jamii peke yake, ni suala la sisi sote na tunahitaji kila mmoja kumtahadharisha mtoto wake na watoto wetu. Mimi kwangu nishawashika masikio nina wari wawili nimewaambia bimkubwa kinga ni bora kuliko tiba, kimbiza nafsi yako najitahidi kuwaambia ikifika saa moja ya usiku wamechelewa 12 na nusu basi wawe wameshafika kibandani, lakini mji umeharibika na sote tuwe askari.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja na naomba nimsaidie Mheshimiwa tuikubali hotuba yake na apewe fedha hizi ili aendelee na kazi hii. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana. Mhe. Spika, naomba nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuzungumza machache kuhusiana na hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2012/2013.

Awali ya yote naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi ambavyo wamekamilisha matayarisho ya hotuba hii na kuweza kuiwasilisha hapa ndani ya Baraza lako tukufu kwa ustadi mkubwa na kuweza kufahamika.

Mhe. Spika, nimelazimika kusimama katika eneo ambalo limeguswa na wachangiaji mbali mbali walipokuwa wanachangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri suala zima linalohusiana na jinsi gani tutaweza kudhibiti vijana wetu na matumizi ya dawa za kulevya.

Mhe. Spika, naomba tuelewe sote kwamba vita dhidi ya dawa za kulevya havitaweza kufanikiwa kwa kutekelezwa na taasisi fulani fulani, vita hivi ni vya jamii nzima ni lazima jamii nzima ishirikiane kwa pamoja na taasisi za serikali na zile ambazo si za serikali ili kuhakikisha kwamba tunafanikiwa jinsi ya kuweza kuwadhibiti vijana wetu wasiweze kuingia katika janga la kutumia dawa za kulevya.

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu kama wazee ndani ya jamii tuna wajibu wetu ambao tunapaswa kuutekeleza na ni wajibu mzima wa kuwalea vijana wetu katika maadili mema. Sitakosea Mhe. Spika, nikisema kwamba wazazi wengi kwa kisingizio pengine cha majukumu kuwa mengi na shughuli za kila siku za maisha wanasahau kulea watoto katika maadili ambayo sisi kama Wazazibari tumekulia nayo. Hali hii huwapa fursa vijana wetu muda mwingi kuwepo nje bila ya kuwa na shughuli maalum za kufanya katika umri mdogo kabisa na ndipo wanapoweza kujiunga katika vikundi ambavyo huweza kuwasababisha kuingia katika maadili ambayo sio mazuri kama kuvuta sigara, bangi, dawa za kulevya na aina ya mambo hayo.

Sasa katika hili Mhe. Spika, naomba niwaombe sana wazazi watimize wajibu wao wa malezi. Mimi nakumbuka Mhe. Spika, wakati nilipokuwa mdogo na wengi wa wajumbe hapa wanaweza kukubaliana na mimi hasa vijana wa kiume wakati wanapokwenda msikitini Magharibi huwa wanazuiliwa ndani ya misikiti au katika darasa vyuo fulani wa ajili ya kupata elimu ya dunia na akhera humo humo ndani mpaka wakati wa kumaliza Sala ya Isha ndipo wanaporudi majumbani. Kipindi hiki ndicho mara nyingi kinachoonekana kwamba baina ya Magharibi na Isha vijana wetu utakuta makundi ya kupotea potea. Kwa hivyo, niwaombe sana wazazi turudishe utamaduni, wale ambao tuna maadili ya Kiisilamu ambapo ndio wengi turudishe utamaduni huo, lakini wale ambao hawana utamaduni huo wa baina ya Magharibi na Isha basi ni vizuri kuhakikisha kwamba watoto wanarudi nyumbani mapema sana.

Kwa sababu wakati ambao vijana wetu wanaweza kuingia kwenye makundi haya kwa kificho ni wakati huu wa baina ya Magharibi. Kwa hivyo, niombe sana ushirikiano wa walezi katika hili ambapo ndio sisi tuliopo hapa na wengine ambao bila shaka wanatusikiliza.

Mhe. Spika, naomba pia tuwe wawazi, sisi kama Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais tunatimiza wajibu wetu mkubwa wa kutoa taaluma kwa jamii lakini pia kwa vijana kwa kupitia skuli. Ni lazima tuwaeleze vijana wetu wazi wazi athari ya dawa za kulevya, vijana wetu hawa kwa kufahamu athari hizo tutaweza kuwazuia wasiingie katika janga hili. Kwa hivyo, ni muhimu tukae na watoto wetu tuwaeleze juu ya suala zima la athari ya dawa za kulevya kwanza kwake yeye kijana mmoja mmoja, lakini pili ndani ya familia ambayo naamini wengi wetu au sote na wanaotusikiliza wanafahamu athari ya dawa za kulevya. Lakini pia kwa jamii kwa jumla lakini kubwa zaidi kwa serikali ambayo inawahitaji vijana hawa kama nguvu kazi katika kuendeleza maendeleo ndani ya nchi yetu. Kwa hivyo ni lazima tuvunje ukimya, tuzungumze na vijana wetu tuwape taaluma ili wao wenyewe waweze kusema hatutajihusisha hiki nikitu kibaya hatutakwenda kuingia katika dawa za kulevya. Hilo ni muhimu sana.

Sisi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais tunalifanya kwa nguvu zote hata kupitia katika skuli, ni lazima athari zifahamike kwa vijana wetu ili wasiweze kwenda kutumia dawa hizo.

Jenginie Mhe. Spika, ni suala zima la kuwa na uadilifu katika vyombo vyetu ambavyo vitaweza kudhibiti hizi dawa za kulevya zisiwemo katika *circulation* hapa ndani ya visiwa vyetu. Niombe sana vyombo vya ulinzi na usalama lakini pia Mahakama zitende kazi zao kwa uadilifu mkubwa.

Pia niwaombe Waheshimiwa wananchi nao kuacha muhali, kama tunawafahamu watu ambao wanajihusisha na suala zima la uuzaji, uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya Zanzibar ni ndogo sana tunajuana basi ni vizuri tutoe taarifa hizi kwa vyombo husika ili waweze kushughulikiwa ili tuweze kudhibiti dawa zisiingie ndani ya visiwa vyetu. Kwa hivyo, mambo makubwa tunayoweza kuyafanya ili kuzuia vijana wetu wasiingie katika dawa za kulevya kwanza tuhakikishe kwamba hazitakuwepo, lakini kubwa sana kuhakikisha kwamba vijana wetu wenyewe wanazikataa kwa sababu ni sawa sawa na bidhaa ndani ya soko, ikiwa kuna bidhaa ndani ya soko ambayo wateja hawaihitaji bidhaa hiyo moja kwa moja itatoweka na biashara hiyo itakufa.
Kwa hivyo, mimi naomba sana tuweke mkazo katika kutoa elimu kwa vijana wetu na kwa jamii kwa ujumla juu ya athari ya dawa za kulevya ili tufike pahala vijana wetu waseme no to drugs na inawezekana kabisa. Kwamba hawataingia katika janga la kutumia dawa, tukifanikiwa hapo hata hii biashara ya dawa za kulevya ndani ya visiwa vyetu itapotea Mhe. Spika. Hivyo, naomba sana katika hili niseme ni suala gumu na linahitaji ushirikiano wa kila mmoja wetu, sote kwa pamoja tutaweza kuwaepusha vijana wetu katika kutumia dawa za kulevya.

Mhe. Spika, nilitaka nilizungumze hilo tu lieleweke vizuri sana na baada ya hapo niseme kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii kwa asilimia mia moja nakushukuru.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, hapana shaka muda uliobaki haumtoshi Mhe. Waziri kufanya majumuisho, kwa maana hiyo basi apate muda akatafakari michango yetu Waheshimiwa Wajumbe ili jioni aje kufanya majumuisho na kumpitishia vifungu vyake kwa kadiri mtakavyoona inafaa. Tusitishe shughuli zetu basi hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 6:45 Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, ninapenda kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliochangia hotuba ya bajeti ya Wizara moja kwa moja au kwa maandishi.

Michango yao kwa njia moja au nyengine itaweza kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara. Miongoni mwa Wajumbe waliochangia ni pamoja na:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Hamza Hassa Juma
7. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
8. Mhe. Mgeni Hassan Juma
9. Mhe. Fatma Mbarouk Said
10. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
11. Mhe. Mussa Ali Hassan
12. Mhe. Asha Abdu Haji
13. Mhe. Salim Abdulla Hamad
14. Mhe. Abdi Mossi Kombo
15. Mhe. Salma Mussa Bilali
16. Mhe. Salma Humoud Ali
17. Mhe. Rashid Seif Suleiman

18.Mhe. Ashura Sharif Ali
19.Mhe. Hassan Hamad Omar
20.Mhe. Kazija Khamis Kona
21.Mhe. Farida Amour Mohamed
22.Mhe. Mariana Joel Thomas
23.Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
24.Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo
25.Mhe. Waziri wa Afya
26.Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais

Wajumbe 26 Mhe. Spika, wameichangia hotuba hii ya wizara yangu. Ninawashukuru sana kwa kweli, ninawapongeza na ninaamini kwamba wanaipenda wizara hii.

Mhe. Spika, wajumbe waliochangia kwa maandishi ni mmoja tu: Naye ni:-

1. Mhe. Mohamed Said Mohamed

Mhe. Spika, kabla sijaanza kutoa majibu naomba nizungumze machache. Mhe. Spika, mimi mwenyewe hapa nilibebewa mimba akanizaa, nikawa kitoto kichanga baadae nikawa mtoto wa kusoma skuli, baadae nikaingia katika rika la vijana na sasa hivi nipo katika utu uzima karibu ninaingia kwenye uzee lakini bado sijawa mzee sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nimepewa kazi ya kuwalea wazee, vijana, wanawake na watoto, na kwa bahati wote hao ninawapenda sana. Kwa sababu ninawapenda wanakuwa hawana taabu kwa waziri wao, wakati wowote wana nafasi ya kuzungumza na mimi kunishauri, kunielekeza ukiacha hao watoto wadogo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kuna mheshimiwa mmoja hapa alisema kwamba Raia hakukosea kuniteuwa mimi kuwa Waziri wa Ustawi wa Jamii. Ninashukuru ulezi umefika pahala pake. Ukiona pahala pamezorota pesa ni ndogo. Jamani tutafanyaje na ndio hali yetu ya umaskini. Lakini hata hivyo tunajitahidi kweli kweli kuona kwamba kile kile kidogo tunachokipata tunagawana kidogo kidogo.

Kama msemo wa marehemu Mzee Karume unavyosema, “Ni afadhali tuwe na kitu kidogo lakini tugawane kidogo kidogo kuliko kuwa na kitu kingi tukaanza tugombana”. Sasa hiki tulichokipata ndio hiki.

Sasa nikianza Mhe. Spika, wizara inawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote waliochangia na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali za Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Aidha, ninapenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi – Mhe. Amina Iddi Mabrouk kwa ushauri wake na maelekezo yake na tunaahidi kuyafanyia kazi tukishirikiana pamoja na yeye. (*Makofi*).

Kuhusu suala la sheria ya kumlinda na kumhifadhi mtoto, sheria hiyo tayari ipo na imeshapitishwa na Baraza lako Tukufu na kutiwa saini na Mhe. Rais mwaka 2011. Sheria hii inasimamia ulinzi wa watoto wote nchini, wakiwemo watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wenye mahitaji maalum.

Mhe. Spika, kuhusu kuharakisha mpango wa kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira magumu, wizara inaendelea na zoezi la kuwatambua na kwa mwaka huu tutafanya Shehia 10 Unguja na Shehia 10 Pemba, tukipita tukiwatambua hawa watoto wenye mazingira magumu.

Aidha, kuhusu ushauri wa kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira magumu wataingizwa katika sensa ya mwaka 2012 na tunachukua ushauri wako Mhe. Mwenyekiti, tutawasiliana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ili kulishughulikia jambo hili.

Mhe. Spika, kuhusu kuwepo programu endelevu za kuelimisha na kushajihisha vikundi vya vijana na kutafuta masoko ya bidhaa zao ndani na nje ya nchi, ambapo suala hili pia liliulizwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Wizara inafanya tathmini ya vikundi ya vijana kwa Shehia zote za Unguja na Pemba ili kujua mahitaji halisi ya vikundi hivyo kwa lengo la kuwaunganisha na fursa mbali mbali zilizoopo na zitakazojitokeza ikiwemo mafunzo, mikopo na fursa za masoko ya bidhaa zao.

Mhe. Spika, kuhusiana na suala la kuendelea kuwatambua watoto wenye ulemavu nchini, wizara inashirikiana na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu suala la usajili ya watoto wenye ulemavu. Wizara inayo mashirikiano makubwa na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais chini ya Idara yake ya Watu wenye Ulemavu, na tunaahidi kushirikiana kwa karibu zaidi kupitia maofisa wa wanaofisa wa wanawake na watoto wa Wilaya pamoja na Waratibu pamoja na kuhakikisha kuwa watoto wenye ulemavu wanafanikiwa pamoja na kutambuliwa. Mhe. Spika, tutashirikiana sana na Mhe. Madam Fatma Ferej ili jambo hili liwe zuri zaidi.

Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu suala lake la kwamba hakuna umuhimu wa kufanya utafiti wa ombaomba. Naomba kumjibu kwamba suala la ombaomba limekithiri kwa visiwa vyetu, tunaona vibaya na haya. Hivyo kuna umuhimu wa kuelewa ukubwa wa tatizo hili na sababu zinazowapelekea watu kuwa ombaomba. Matokeo ya utafiti huo yatasaidia kutoa picha halisi ya kutuwezesha kupanga mipagno endelevu kwa kushirikiana na sekta nyengine ya kuwasaidia na kuweza kulitatua tatizo hili.

Mhe. Spika, ninapenda kujibu suala la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Makame Mshimba, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Bikame Yussuf Hamad waliotaka kujua ni lini Baraza la Vijana litakuwa tayari. Naomba niseme Mhe. Spika, mwaka jana tulilifanyia kazi Baraza la Vijana.

Rasimu ya Katiba iliyoandaliwa awali ilionekana ina mapungufu makubwa ambayo yangeliweza kukwamisha na kurudisha nyuma utekelezaji wa Baraza hilo. Hivyo wizara ikatafuta mshauri mwelekezi ambaye alikusanya maoni ya vijana yaliyopelekea kuandaliwa upya rasimu ya Katiba hiyo.

Mwaka huu rasimu ya Katiba ya Baraza la Vijana imeshajadiliwa vya kutosha katika vikao vyote vinavyohusika mpaka vya Makatibu Wakuu, na sasa wizara inashirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupata maelekezo ya kitaalamu na kutayarisha mswada wa sheria. Mhe. Spika, Baraza la Vijana litaundwa rasmi wakati wowote tukiwa tayari.

Mhe. Spika, naomba kujibu suala la vikundi la vijana lililoulizwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba wizara inaendelea kufanya tathmini ya vikundi vya vijana kwa Shehia zote za Unguja na Pemba ili kujua mahitaji halisi ya vikundi hivyo kwa lengo la kuwaunganisha na fursa mbali mbali zilizoopo na zitakazojitokeza ikiwemo mafunzo, mikopo na fursa za masoko ya bidhaa zao.

Mhe. Spika, wizara haina lengo la kuwadhalilisha skaunti maana ni miongoni mwa mwa vijana ambao tunawapenda. Wizara inashirikiana na skaunti kwa kufuata utaratibu uliowekwa wa kuwasiliana na kamati ya kufufua uskaunti Zanzibar.

Vijana waliolalamika hawakufuata utaratibu wa kuwasiliana na kamati. Ninapenda kulithibitishia Baraza lako Tukufu kwamba wizara itaendelea kushirikiana na skaunti na vijana wote nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha katika mambo mbali mbali yanayohusu vijana. Naomba nimwambie Mhe. Mshimba kama Mkurugenzi wetu alikosea, tunaomba radhi Wizara ya Ustawi wa Jamii kwa hilo.

Kuhusu suala la takwimu za vijana waliopata ajira, takwimu zilizotolewa ni sahihi. Siwezi mimi kusema uwongo lakini naomba muelewe kwamba kuna ajira za muda, sio sisi tu vijana tunaopata ajira za muda lakini hata Wizara ya Kilimo kuna ajira za muda, Wizara ya Mawasiliano kuna ajira za muda, zikimalizika muda wake kila mmoja kwaheri karibu, mbali ya wale wataalamu na watu wengine waliokuwa wameajiriwa.

Kwa hivyo hizi ajira za muda na za kudumu, ushauri wako wa kufuatilia maslahi ya vijana hao, tumeupokea na tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, na kuhusu kuwatafutia eneo la biashara. Ushauri wako tunauchukua na tutashirikiana na Wizara ya Biashara au niseme tunashirikiana hivi sasa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kulifanyia kazi suala hilo.

Naomba kujibu suala la maslahi ya watumishi kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, wafanyakazi wote wa wizara yangu wanalipwa maslahi yao yanavyostahiki kwa mujibu wa sheria na matoleo ya serikali. Kama kuna mfanyakazi yeyote au dereva yeyete anayesema yeye halipwi maslahi yake, hamtumsaidii lolote ajitokeze atwambie ili tumshughulikie na yeye apate haki yake. (*Makofi*).

Mhe. Spika, Mhe Jaku alitaja kujua kuhusu posho la wafanyakazi 118 wa vituo vya nyumba ya wazee na watoto Mazizini, Sebleni na Welezo. Ninapenda kumjibu kuwa wafanyakazi hao 118 wote pamoja na mishahara yao wanalipwa posho la mazingira magumu ambayo ni shilingi 50,000/= kila mwezi tunawalipa.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba alitaka kujua kuhusu kuwepo kwa hati ya nyumba ya kulelea watoto Mazizini. Ninapenda kumjuulisha kwamba hati ya nyumba ya kulelea watoto Mazizini ipo tayari nimekuja nayo ile pale pamoja na mkataba wake tayari tunao, umeshaandikwa vizuri, tumeshatiliana saini na vyombo vya habari vikapata habari. Nilisema tukiwa tayari hatuna kificho, samahani Mhe. Spika. (*Makofi*).

Lakini ninamuomba tu Mhe. Mshimba akubali na tunamkaribisha katika afisi yetu aje ili tumuoneshe mkataba, hati na mambo mengine yoyote atakayoyahitaji, lakini kama si hivyo haitoshi tuna mpango wa kuwafanyia semina wajumbe wa Baraza wote wa Baraza la Wawakilishi. Siku hiyo tutauleta mkataba, hati na kila mjumbe atapata nafasi ya kuuwona, kuusoma na kutoa mawazo yake, kama jee umeandikika au haujaandikika hapo ndio tutapata maoni. Lakini kwa utaratibu wa kiserikali hatuwezi tena tukasimama hapa tukasoma mikataba na hati, ninaomba radhi kwa hilo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba kuhusu utekelezaji wa sheria ya mtoto kwamba haijafanya kazi kwani bado watoto wanatumikishwa. Mhe. Spika, naomba niseme sheria inafanya kazi, tuliileta hapa Baraza lako tukufu likaikubali, Rais akatia saini na mimi mwenyewe Waziri nikaitangaza rasmi kwenye magazeti ya serikali, lakini bado kuna wazee ambao hawashughuliki wanawatumikisha watoto wao, wanasema kwamba wanatafuta riski, jambo ambalo si zuri hata kidogo kuwatumikisha watoto wadogo.

Mhe. Spika, sheria Na. 6 ya mwaka 2011 imeshaanza kazi. Kinachoendelea sasa ni kuandaa kanuni na hifadhi ya mtoto wakati huo huo wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto inaendelea kuelimisha juu ya athari za kumnyima mtoto haki zake za msingi ikiwemo kutumikishwa kwa ujira mdogo au pasipo na ujira na kumkosesha kwenda skuli.

Wizara pia imeandaa mpango wa kuelimisha sheria hii kwa jamaii. Tutapita kipembe kwa kipembe, kichoro kwa kichoro kuelimisha juu ya sheria hii. Hivi sasa tumeshaanza kazi. Penye tatizo la ubakaji wazee wanasema kweli watoto hapa wanabakwa na palipokuwa hapana tatizo, wanatwambia kama hapa ubakaji haupo.

Mhe. Spika, naomba kumjibu tena Mhe. Mshimba suala lake linalohusiana na vikwazo vingi vya kufanya biashara kwa wanawake na riba kubwa kwa akinamama wanaopata mikopo. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa imani yake kubwa aliyoonesha kwa kuwajali wajasiriamali wanawake. Suala la kuwaendeleza wajasiriamali kwa kuwapa mikopo ni suala ambalo linalohitaji mashirikiano makubwa baina ya taasisi zinazoshughulikia masuala ya utoaji wa mikopo na wajasiriamali wenyewe.

Aidha wajasiriamali wanatakiwa wawe na moyo wa kizalendo wa kurejesha mikopo, kuna wengine wanawanyima wenziwao mikopo kwa sababu hawataki kurejesha mikopo. Ni ukweli usiopingika kuwa taasisi zinazotoa mikopo zinaweka masharti na riba ambapo wanawake hukumbwa na ugumu wa kupata mikopo hiyo. Kilio hiki cha kuwapunguzia masharti magumu wanawake wajasiriamali kimekuwa ni cha muda mrefu. Hivyo wizara yangu ina mpango wa kuanzisha benki ya wanawake itakayopelekea kufungua kusaidia tatizo hilo.

Kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wa Fedha ameeleza asubuhi ya leo kwamba kuanzisha benki ni kazi kubwa. Kima hiki cha chini ili tunaanza benki hii lazima tuwe na shilingi bilioni 15. Kwa hivyo si kazi rahisi Mwenyezi Mungu atatujuaalia tutaifungua hivyo benki, tena kwa vigelegele na shangwe, watatusikia watu sasa wanawake wana benki yao. (*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mtumwa Kheir, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Bikame Yussus Hamad, Mhe. Kazija Khamis Kona, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Salma Mussa Bilali na Mhe. Farida Amour Mohamed kuhusu suala la mtaalamu wa benki ya wanawake anatoka nchi gani na lini benki itakuwa tayari.

Benki itakuwa tayari pesa tukizipata alhamdulillah lakini mtaalamu anatoka humu humu ndani ya nchi yetu. Naomba kulifahamisha Baraza lako Tukufu kwamba mwanzoni suala la uanzishaji wa benki ya wanawake lilikuwa

ni kuanzisha tawi la benki ya wanawake kupitia Tanzania Bara, yaani tuungane pamoja. Tulikwenda kuwasiliana nao wenzetu wakatufahamisha lakini baadae tukapata maelekezo kwamba tuanzishe benki ya wanawake ya Zanzibar bila ya kupitia Tanzania Bara, hapana habari ya tawi hapa, tuwe na chombo chetu peke yetu. (*Makofi*).

Kwa hivyo kuanzia sasa mtaalamu mwelekezi ambaye ni Mzanzibari na anatoka katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha Chwaka ameshaanza kuandaa utaratibu na mpango maalum utakaozingatia namna ya upatikanaji wa fedha, vigezo vya uanzishaji wa benki na hati ya kisheria ya uanzishaji wa benki hiyo.

Mhe. Spika, kuhusu kesi ngapi za udhalilishaji wa watoto zinaendelea mahakamani. Ninapenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim, Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Salma Mussa Bilali, Mhe. Farida Amour Mohamed, Mhe. Salma Mohamed Ali, Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Hamza Hassan Juma kuwa kituo cha mkono kwa mkono kuanzia Januari, 2012 hadi Mei 2012 kinafanya kazi kama kawaida, lakini kwa bahati mbaya sana kesi mpaka hivi sasa zilizopo mahakamani ni 10 tu. Kesi zipo nyingi lakini ziliopo ni 10.
Mhe. Spika, suala la udhalilishaji na unyanyasaji kijinsia limekuwa likilalamikiwa na wengi na hasa hatua zinazochukuliwa. Hata sisi wizara tunasikitika sana pamoja na kazi kubwa tunayoifanya ya kutoa elimu kwa jamii, kuandaa sheria na mambo mbali mbali, maelekezo, uhamasishaji wa kuwaambia watu wanaume jamani musiwabake watoto, lakini hawakubali.

Leo kwenye redio nimesikia nilisikia mtoto wa miaka miwili na nusu kabakwa jamani si hatari hiyo. Kwa bahati mbaya sana Mhe. Spika, kesi mahakamani hazihukumiwi, watu hawatiwi adabu. Kama tutawatia adabu watu kweli watapunguza kasi ya kubaka watoto.

Wizara inaandaa kampeni ya kitaifa kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, kama tunavyoandaa kampeni ya karafuu kwamba tuhakikishe karafuu zinachuma. Sasa tunaandaa kampeni ya udhalilishaji. Kwa hivyo sote hapa Wajumbe wa Baraza lako la Wawakilishi itabidi tushiriki kikamilifu katika kulizungumzia jambo hili. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuhusu suala la matokeo ya utafiti wa udhalilishaji wa watoto. Utafiti huu ulizinduliwa na makala zilisambazwa kwa wadau wote na wizara ipo tayari kuwapatia makala wote wale wanaohitaji kuhusu suala la kufanya utafiti wa kuangalia ukubwa wa tatizo la udhalilishaji kwa watoto.

Wizara imo katika hatua ya kufanya tathmini ya kuangalia ukubwa wa tatizo hili kuhusu suala kwamba hatua gani zinachukuliwa kuhakikisha kwamba ushahidi hauvurugwi. Wizara inachukua hatua ya kuimarisha vituo vya mkono kwa mkono, mafunzo, miongozo, vifaa pamoja na kuhamasisha jamii kufuatilia kesi hizi na kutoa ushahidi dhidi ya kesi za udhalilishaji.

Naomba sana wananchi tusijaribu kumficha mtu anayembaka mtoto. Tukasema tunafanya hisani tumuozeshe, tufanyeje, kwani yeye hakujua tangu zamani kama kuna utaratibu wa kuowa.

Kwa kushirikiana na Shirika la Save Children, wizara imejipangia kuwapatia nyenzo madaktari wa one stop centre kwa ajili ya kukusanya ushahidi wa kitaalamu. Hapa ninataka niseme pamoja kuwa tunasubiri hiyo DNA lakini chombo hiki kikiletwa na vifaa vyake, basi hata ule unywele tu ukianguka basi ushahidi utapatikana kwamba wewe ndio uliaohusika na jambo hili.

Hivyo kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, tayari tumeshafanya mafunzo ya siku tano ya namna ya kukusanya ushahidi wa kitaalamu kwa madaktari 17 kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, Kivunge na Makunduchi.

Kuhusu suala la nani anayepaswa kununua DNA machine. Ni serikali kupitia Wizara ya Afya na kwa bahati nzuri amelielezea uzuri Mhe. Waziri wa Afya asubuhi ya leo. Kwa hivyo tunategemea wakati wowote tunaweza tukapata hii DNA. Lakini pamoja na chombo hiki ninashauri kwamba isiwe sababu ya kusema kuwa kesi zisihukumiwe kwa sababu tunasubiri chombo hiki.

Mhe. Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Ismail Jussa ladhu kuhusu ushauri wake kwamba wizara itekeleze wajibu wa watoto. Ushauri wake inaupokea, samahani, wizara itekeleze wajibu wake kuhusu watoto. Ushauri huu tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Hata hivyo katika kuhakikisha watoto wanazijua haki zao na wajibu wao inaendelea kuhamasisha uundaji wa Mabaraza ya Watoto takriban katika Shehia zote za Unguja na Pemba, ambapo jumla ya Mabaraza 114 yameshaundwa katika Wilaya zote Unguja na Pemba. Lakini bado Waheshimiwa wanasema twende vijijini zaidi nako tukaanzishe Mabaraza ya Watoto. Tunakubali wala hatuna ubishi wala hatuna ushindani kwa hili.

Pia wizara inakubaliana na wazo na ushauri wa mwenyekiti wa kuwezesha Mabaraza ya Watoto kukutana na Waheshimiwa Wawakilishi katika majimbo yao kwa kuandaa utaratibu. Waheshimiwa mikutane nayo hayo Mabaraza huko majimboni.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mshimba suala lake kuhusu utekelezaji wa sheria ya mtoto kwamba haijafanya kazi. Kwani watoto bado wanatumikishwa. Sheria inafanya kazi lakini bado wazazi hawajakubali suala hilo.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba na Mhe. Farida Amour Mohamed suala lao linalohusiana na vikwazo na riba kubwa kwa akinamama wanaopata mikopo. Ni kweli riba ni kubwa lakini tuombe Mungu ikianzisha benki ya wanawake yote haya yatatupungukia.

Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa imani yake kubwa aliyoonesha na inaonekana hasa kwamba anawajali wanawake. Suala la kuwaendeleza wajasiriamali kwa kuwapa mikopo ni suala ambalo linahitaji mashirikiano baina ya taasisi zinazoshughulikia masuala ya utoaji wa mikopo na wajasiriamali wenyewe. Suala hili nimeshalizungumza tayari, lakini wale wajasiriamali wanatakiwa wawe wazalendo kwa kurejesha mikopo kwa wakati.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kuwa taasisi zinazotoa mikopo zinaweka masharti na riba kubwa, ambapo wanawake hukumbwa na ugumu wa kupata mikopo hiyo. Kilio hiki cha kuwapunguzia masharti magumu wanawake wajasiriamali kimekuwa ni cha muda mkubwa. Kwa hivyo Wizara ina mpango mzuri wa kupita tukiwafahamisha hao wanawake kuhusu mambo ya mikopo kwa jumla na kwenda kwenye taasisi zilizokuwa hazina riba kubwa ya mikopo.

Mhe. Spika, napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi, pamoja na Baraza lako tukufu kuwa mchakato huu wa kuanzisha benki ya wanawake. Naomba na nyinyi mushiriki katika kutoa mchango Waheshimiwa Wajumbe, katika kufungua chombo hiki kila Mjumbe angalau basi mtugaie japo milioni moja moja, hapo mambo yetu yatakuwa mazuri.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma suali lake lenye kifungu (a),(b) na (c), kuhusu wanawake wajasiriamali walioshiriki maonesho ya sabasaba mwaka huu, kwamba hawajafanya biashara vizuri, wanahitaji kusaidiwa na watakaporudi Mhe. Waziri aitishe kikao kutathmini shughuli zao kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala hili nimelifuatilia kwa kina tangu alipolitoa Mhe. Hamza Hassan. Ni kweli kwamba kuanzia tarehe 01 mpaka tarehe 03 biashara hazikufanyika. Lakini baada ya ufunguzi kuanzia tarehe 04 hadi tarehe 07, wanawake hao waliuza biashara zao vizuri sana na kuweza kuagiza mizigo mingine kutoka Zanzibar na biashara ilikuwa nzuri sana.

Mhe. Spika, kuhusu ubora wa bidhaa na soko. Ni kweli wajasiriamali wanahitaji mafunzo, kusimamiwa na kufuatiliwa, haya yote hufanywa kwa mashirikiano ya karibu baina ya Wizara zinazoshughulikia masuala haya, nikimaanisha Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa taarifa yenu bidhaa za Zanzibar za mwaka huu zimepata sifa kubwa, baada ya kutembelewa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Makamo wa Pili wa Rais na wamesifu uzuri wa bidhaa zetu kutoka Zanzibar. Kwa hivyo, tuwapongeze wanawake wajasiriamali sasa hivi wameendelea kweli kweli katika kuweka vifaa vyao kwenye hali nzuri, yaani vijiuze. (*Makofi).*

Mhe. Spika, aidha, Wizara imejipangia vizuri kwa kuitisha kikao cha tathmini ya shughuli zao baada ya kurudi mwezi wa nane. Watakaporudi tunamuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba tutawaita na tutazungumza nao ili watueleze mambo yaliyowakuta, kama kuna tatizo ili mara nyengine lisitokee.

Mhe. Spika, naomba sasa kumjibu Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak na Mhe. Salum Abdalla Hamad ambaye alitaka kujua ni misingi ipi ya Kiislamu ambayo imetumiwa katika marekebisho ya sheria ya Mahakama ya Kadhi. Mhe.

Spika, misingi iliyotumiwa ni kwa kufuata Qurani tukufu na Sunna za Mtume Muhammad (SAW) na hadithi zilizothibitishwa. Aidha, Mhe. Salum Hamad alitaka kujua tutahakikisha vipi sheria hii mpya, haitapingana na misingi ya dini ya Kiislamu.

Mhe. Spika, tunaoandaa hii sheria ni Waislamu, kwa hivyo kwa vyovyote tutakwenda kwa misingi ya Kiislamu na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia kwamba hatutopingana na misingi ya Kiislamu. Napenda kumjibu kuwa Wizara katika kufanikisha marakebisho ya sheria hii, katika hatua zote tulizofanya mikutano iliyowashirikisha viongozi wa dini Unguja na Pemba kwa ajili ya kupata maoni yao, pia rasimu ya waraka ya marekebisho ya sheria hiyo, itawasilishwa na kujadiliwa na Baraza lako tukufu. Kwa hivyo, nategemea Waheshimiwa Wajumbe mtatoa michango mikubwa katika kuhakikisha sheria hii haipingani na misingi ya dini ya Kiislamu.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak wa nafasi maalum za wanawake na Mhe. Kazija Khamis Kona, swali lake kuhusu hatua iliyochukuliwa na Wizara katika kuwasaidia wanawake na watoto walioathirika na MV Spice Islander, kwamba tulifanya kazi kubwa. Mimi mwenyewe kama mwanamke kwanza nilikwenda kuwakagua maiti zote za wanawake na watoto, na nilishuhudia mimi mwenyewe watoto wamelazwa katika matumbo ya mama zao ambao tayari wameshafariki dunia. Tuliosha maiti sisi, lakini kama haitoshi tulikwenda kuwafariji, mimi mwenyewe nikifuatana na Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais tulikwenda mpaka Pemba kwenda kutoa ubani na kuwafariji wenzetu. Kwa kushirikiana na Idara ya maafa tuliwapa ushauri nasaha.

Mhe. Spika, mambo si hayo tu, tulitoa na michango ya kifedha hasa kuwapa wazee waliohusika na misiba ile. Naomba kumuhakikishia kuwa tayari wizara imewasiliana na Wizara ya Afya, na kutokana na upungufu wa madaktari tumepata daktari ambaye huja kukagua na kutoa huduma za kiafya kwa wazee mara tatu kwa wiki, na pale panapohitajika. Daktari wa kumweka ndani hasa kule Sebleni hatujampata. Lakini tangu siku aliyokwenda Rais pale na akatoa agizo, basi daktari anakwenda wiki mara tatu. Kwa hivyo, hilo naona sio jambo baya kwa sababu hata sisi tukiwa majumbani tukiumwa sana, baada ya huduma ya kwanza huwa tunakimbizwa hospitali, lakini daktari Mhe. Mtumwa wa kumuweka mule ndani, ndugu yangu, mwanangu, mpenzi wangu, shoga yangu bado hatujampata.

Mhe. Spika, naomba kuwajibu Mhe. Salum Abdalla Hamad, Mhe. Farida Amour Mohamed, Mhe. Salma Mussa Bilal na Mhe. Mussa Ali Hassan kuhusu malipo ya shilingi 5,000 zinazotolewa kwa wazee wa majumbani kwamba msaada huo unasimamiwa na kutolewa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kupitia Idara ya Tawala za Mikoa. Lalini pamoja na hayo, jambo kubwa tunatakiwa tulee wazee wetu jamani, wazee wametuzaa wametuhangaikia mpaka tumekuwa wakubwa vijijini huko, kwa hivyo tusiwatupe wazee wetu, tuwalee ndio dini hasa ya Kiislamu inavyotuambia tuwalee wazee wetu, ukiachiwa radhi na mama na baba adabu yake hapa hapa duniani kabla hatujafika mbele ya haki. Kwa hivyo, tuwaleeni wazee wetu na sisi viongozi hapa tuwe mfano wa kutosha wa kuwalea wazee wetu. Kuhusiana na idadi ya wazee wanaotunzwa na serikali kimkoa na vigezo vinavyotumika kuwaingiza.

Mhe. Spika, naomba kuendelea kumjibu Mhe. Mussa kwamba wizara haichukui wazee kulingana na mikoa, bali huchukua kulingana na mahitaji na vigezo maalum, navyo ni hivi nitakavyovitaja, awe ni mzee mwenye umri usiopungua miaka 60, awe hana sehemu ya kuishi wala mtoto au jamaa anayeweza kumtunza, awe hana uwezo wa kujihudumia kwa mahitajio yake ya lazima. Huyo ndiye tunayemchukua kwenye nyumba za wazee. Sio tukawachukue tu wazee wote vijijini. Uwezo huo bado serikali hauna tunanong'ona.

Mhe. Spika, kuhusiana na kujenga nyumba za wazee katika majimbo, ni kwamba wizara haijaona haja ya kujenga nyumba za wazee katika kila mkoa, kwani vituo viliopo sasa vina nafasi ya kutosha na vinachukua wazee kutoka katika mikoa yote ya Unguja na Pemba. Aidha, kwa mujibu wa miongozo ya kiustawi na utamaduni wetu, wazee kama ilivyo watoto wanatakiwa kutunzwa katika mazingira ya kifamilia, na hivyo kuwapeleka katika nyumba za kutunzia wazee hiyo ni hatua ya mwisho kabisa inapokuwa hapana budi. Kwa hivyo, tutakapokuwa kule kwenye mikoa wale wazee waliokuwa taaban hawana watoto, hawajiwezi tena ndio mnatuletea sisi katika nyumba ya wazee, bado nyumba ya wazee ina nafasi ya kutosha kuweka wazee. Kwa hivyo, tuambiane tuwashughulikie wazee, ili tukiwaleta pale tuwe na uhakika mzee kijana akiletwa pale hatumpokei, tunasema aah! Mwenzetu bado nguvu yako ni nzuri tunaweza tukamsaidia kitu kidogo akarudi nyumbani. Mhe. Spika, hata hivyo ushauri wa Mhe. Mjumbe tunauchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kupotea watoto naomba kumjibu Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak na Mhe. Mussa kwamba ni kweli mara nyingi watoto wanapopotea wazazi au walezi hutoa matangazo katika vyombo vya hahari, lakini wanapoonekana huwa hawatoi taarifa hii, inatokana na mfadhaiko wanaoupata kutokana na tatizo husika. Hata hivyo, tutawafahamisha wazee kwamba mtu yeyote au mwananchi atakayepotelewa na mtoto wake na akishamuona basi kama yeye anaona tabu kutangaza, sisi akituarifu tutatangaza habari hiyo kwamba watu wajue kuwa sasa mtoto keshaonekana.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Mgeni Hassan Juma pamoja na Mhe. Fatma Mbarouk Said wa Jimbo la Amani ambao walitaka kujua je wizara ina mkakati gani wa kuwasaidia vijana katika kuondokana na dawa za kulevya, na kuporomoka kwa maadili kwa vijana na je, wizara inawasaidiaje vijana wasio na ajira ili kuweza kupata ajira.

Mhe. Spika, kwanza nataka nijibu suala hili la watoto wanaokula dawa za kulevya, kwa bahati nzuri Mhe. Fatma pale kaeleza vizuri suala hili leo asubuhi. Mhe. Spika, suala la ajira ni kubwa sana, yupo mwenzangu Waziri anayehusika na mambo haya ya ajira. Lakini tusitegemee ajira za serikalini tu jamani, huko vijijini tukubali kujituma. Mimi ninalo kundi la vijana wa *ZASOSE*, sasa hivi wako kule Tunguu wanafanya kazi ni vijana, lakini wamejitolea kulima kwa hiyari zao wala sikuwalazimisha mimi, nililofanya ni kuwahamasisha. Kwa hivyo, suala la ajira bado litakuwa lina matatizo, mwenzetu labda akipata uwezo tutaona vipi atakavyoweza kuwasaidia vijana wetu, na tutakuwa tayari kushirikiana naye katika shughuli hii.

Mhe. Spika, jukumu la wizara yangu ni kuwapatia mafunzo na kuwahamasisha vijana kushirikiana na mipango ya serikali kupambana na dawa za kulevya. Wizara inaendesha kampeni hiyo kwa kupitia ujumbe wa mwenge kwa siku yoyote unapokuja mwenge, na sasa hivi mwenge ni wa kiserikali sio wa chama tena, kama tunavyosema kwamba mwenge ni wa chama. Mwenge ulikuwa kwenye chama, lakini ukatolewa kwenye chama kwa sababu ulionekana labda kuna matatizo kidogo, kila mmoja na chama chake na kadhalika. Lakini sasa hivi mwenge ni chombo cha serikali.

Kwa hivyo, kama ni chombo cha serikali, basi tunapokwenda popote kwenye ujumbe we mwenge wa uhuru ambapo vitabu vya kampeni hiyo huandaliwa kila mwaka. Aidha, makongamano yote ya vijana, suala hilo linakuwa ni ajenda ya kudumu na mafunzo ya *study* za maisha ambayo humpatia kijana fursa ya kujitambua na kujua namna bora ya kuishi na kuimarika.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Mgeni Hassan Juma, waliotaka kujua je umiliki wa shamba la *Rozela* ni wa ZASOSE au ni wa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mgeni kwamba shamba la maua na mboga mboga la Tunguu ni la *ZASOSE*. Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto tunawasaidia vijana wetu, kwa sababu ni kitu kipya, bado hawajajiweza, tumewatafutia shamba na limefanyiwa *grading*, mbegu na kadhalika. Tumejenga kibanda cha mlinzi na tumeweka tangi la maji ili kuweza kuwasaidia vijana, tunawapa chakula na tumenunua mbolea kuwapa vijana, lakini shamba ni lao sio letu sisi. *(Makofi).*

Mhe. Spika, habari ya mtoto wa umri wa ziro mpaka miaka minane. Nadhani Mhe. Waziri wa Afya amelieleza vizuri asubuhi ya leo.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Bikame Yussuf Hamad kuhusu malengo ya wizara kama ifuatavyo. Malengo makuu ya wizara yanatokana na mpango mkakati wa wizara mwaka 2011/2015 ambao ndio dira ya wizara ya utekelezaji. Hivyo ni lazima yatajirejea kwa miaka hiyo ili tuweze kujipima, yaani yale malengo sisi tukishapanga hatuyatumikii kwa mwaka mmoja tu, tunaweza tukenda nayo mpaka kufikia miaka mitatu au minne, tuna malengo hayo tunakwenda kwa utaratibu. Musione kwamba kwa nini tunarudia rudia malengo hayo hayo, hapana, hatuyarudii ndio utaratibu wa kiserikali.

Mhe. Spika, suala la mashirikiano na mahusiano kwa taasisi za vijana ndani na nje ya nchi, ni suala muhimu linalopelekea vijana kutoka nchi mbali mbali kujifunza na kubadilishana uzoefu kwa maendeleo yao. Kwani vijana hao hupata fursa ya kushiriki katika shughuli mbali mbali za kimaendeleo kwa kujitolea katika miradi ya kijamii kama vituo vya afya, ujenzi wa maskuli, usafi wa mazingira na kujengeana moyo wa uzalendo miongoni mwao.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilal kuhusu mradi wa kuwawezesha kinamama ili kuondoa ajira za watoto. Ni kweli kwamba mradi huu ulikuwepo na hivi sasa mradi kama huo unaendelea kwa kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na unasaidiwa na *Save the Children*.

Mhe. Spika, kuhusu suala la *SACCOS* ya Waridi. Nataka niseme mimi mwenyewe nilikwenda Mkokotoni kwenye *SACCOS* ya Waridi na nilikwenda kama mara tatu hivi kuzungumza na Waridi, lakini inavyoonekana na mimi nilishagombana na wale wahusika waliokuwa wakichukua pesa za *SACCOS* ya Waridi wakijifanya wao wanawatunzia, kumbe wanawaibia pesa zao. Sasa sisi tumewalazimisha wazilipe pesa, lakini bado hawajazirejesha. Nakuhakikishia Mhe. Spika, pesa za Chwaka, za Waridi na nyenginezo zote nitazifuatilia mimi mwenyewe, labda nishindwe tena wale wezi wakishanihangaisha tena nitakuwa sina la kufanya nitakujibu, lakini hilo tutalifuatilia.

Mhe. Spika, kuhusu suali la Mhe. Salim Abdaala Hamad wa Jimbo la Mtambwe kutaka kujua ni kwa nini katika kipindi hiki imeripotiwa kesi moja tu ya kubakwa kwa mwanamke Pemba. Mhe. Spika, kwanza nataka niseme kwamba watu wanabakwa kama nini, kila leo wanabakwa. Lakini kuna wengine hawaripoti, wakishabakwa wanasema ni mambo ya aibu haya jamani, tunyamazeni tusiseme. Sasa huyo aliyetoa taarifa ni huyo mmoja na ndio maana ikaripotiwa hii, lakini wengine hawasemi, ukiacha wale wengine wanaosema mpaka kwenye vyombo vya habari. Ni kweli hii inatokana na uelewa mdogo na kuoneana muhali na kuona haya wazee katika vyombo vya sheria, yaani wakipelekwa kwenye vyombo vya sheria wanaona haya.

Kwa hivyo, wizara inaendelea kuchukua juhudi za makusudi ili kuhakikisha matukio yote yanayojitokeza katika shehia zetu yanaripotiwa na wala yasifumbiwe macho. Lakini na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mkiwa huko na nyinyi tusaidieni kuwaambia hawa watu jamani wapunguze kuwabaka watoto.

Mhe. Spika, kwanza naomba kumshukuru Mhe. Rashid Seif Suleiman kwa mchango wake mzuri na wenye umuhimu kwa lishe ya kinamama, wajawazito pamoja na masuala aliyoyaeleza kuhusu vijana wanawake, watoto na wazee na masuala ya michezo. Ushauri wako tutauzingatia na sio kuuzingatia tu, tutaufanyia kazi. Wizara imejipangia vizuri kwa suala la makuzi ya mtoto na kuwa na lengo maalum ambalo tumeliweka katika malengo yetu ya Idara ya Ustawi wa Jamii na jamii kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, mkakati wa wizara ni kuzishirikisha sekta zote zinazohusiana na makuzi ya mtoto, kuanzia anavyokua tumboni mpaka anapozaliwa. Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilal suali la kuhusu utekelezaji wa sheria ya mtoto ilianza kutumika rasmi mwezi wa Mei mwaka 2012, baada ya kutangazwa rasmi katika gazeti rasmi la serikali na mimi ndiye niliyetangaza Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Lakini nakupa habari ndugu yangu kwamba ubakaji na udhalilishaji ndio kwanza unaendelea na sheria ipo. Sasa tusaidiane kwa sababu hili sio la Wizara tu peke yake, hili ni la familia kwa ujumla au ni la jamii kwa ujumla tulizungumze huko, tusilionee haya.

Mhe. Spika, kwa mfano mzee mmoja kule Ole Kianga alisema, jamani watoto wetu wanaume hapa wanabakwa na watoto wanaume, usiku ukiingia tu watoto hawana nafasi. Sasa mimi nahisi wangekaa wazee pale wakalizungumza jambo hili, na wakaamua hata kuwatia watoto adabu wale wanaowabaka wenzao, sidhani kama lingekuja juu. Lakini kwa sababu watu wanalisemea ndani ndani kila mmoja anaogopa inakuwa sasa linapata nguvu mpaka wale watoto wameshazowea. Mhe. Spika, ni aibu kubwa, akimuona bwana wake huyo anakuja, basi mpaka sauti inabadilika.

Mhe. Spika, suala la Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Jimbo la Mtambwe, anataka kujua katika kambi zilizofanyika Pemba, ni vijana wangapi wa Pemba walishiriki na wanafaidika vipi kiutamaduni. Katika kambi za kimataifa zilizofanyika Pemba, kambi ya Mkoani vijana 10 walishiriki na kambi ya Kiwani vijana 10 walishiriki tena kwa hiyari yao. Kijana anayetaka kwa utaratibu wetu hujaza fomu ya kujiunga na kambi hizo, katika kambi hizi vijana wetu hushiriki kuonesha utamaduni wetu katika mavazi, mapishi, lugha ya Kiswahili inayofundishwa, yaani sio kama wakifika wanakaa tu, lakini wanajifundisha mambo mbali mbali pale walipo. Wakitoka kule waliokuwa hawajui kutengeneza mkate wa gole sasa wanakuwa mafundi.

Mhe. Spika, vijana wetu hunufaika kwa kujifunza lugha za kigeni, hupata fursa za kualikwa kambi hizi nje katika nchi mbali mbali, kati ya vijana watano waliopata fursa ya kwenda Kenya, Afrika ya Kusini na Msumbuji wawili wametoka Pemba, hongereni jamani. UVIKIUTA ni Umoja wa Kikristo Tanzania, huu ni ushirika wa vijana waliopiga hatua kwa kujiajiri wenyewe na kutoa mafunzo mbali mbali ya uzalishaji mali.

Mhe. Spika, kuhusu taratibu zilizotumika kwa kupata vikundi sita tu. Vikundi vyote vilivyoomba fedha za *UN Habitat* vilikuwa 60, lakini vilivyopatiwa fedha ni vikundi sita tu. Vigezo na taratibu za uteuzi zilizotumika zilifanywa na wenyewe *UN Habitat*.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mafunzo kutolewa kwa vikundi tisa, huu ni uamuzi wa *UN Habitat*, wao ndio walioamua tuvifundishe hivi vikundi, na wao ndio walioleta vigezo vyao, na wao ndio waliotoa fedha, sisi hapa hatuna letu. Lakini letu sisi kubwa lilikuwa ni kuwahamasisha vijana tu.

Mhe. Spika, serikali inawahamasisha wananchi kujiunga na vikundi hivi ili kuweza kuwahudumia kwa urahisi. Vikundi vilivyoundwa sio mali ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika wala Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kila taasisi ina wajibu wa kusaidia juhudi za wananchi. Wizara inahusika na uratibu wa shughuli zote za maendeleo ya vijana, jukumu letu ni kuwakusanya na kuwaunganisha na fursa mbali mbali zilizopo. Baada ya Baraza la Vijana likishaundwa itakuwa ndio *center* yao ya kukutana.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Rashid Seif Suleiman. Nadhani nimeshamjibu. Lakini kulikuwa kuna suala la ushauri wake alilotoa ambalo alisema vijana tuwapatie ajira, michezo ni muhimu kwa vijana na elimu kwa kuwa karibu sana na wizara husika, ili kuimarisha mambo hayo. Kwa hivyo, sisi tutajitahidi kuwaelimisha hawa vijana na tutakuwa pamoja na wizara husika, ili tuhakikishe kwamba maagizo haya yanayotolewa yanaendelezwa na yanafuatiliwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Mhe. Hamad Omar wa Jimbo la Kojani, alizungumzia kupeleka michango ya mwenge katika miradi ya maendeleo. Masuala ya mwenge hayako tena katika chama, nilishasema mapema. Badala yake yako katika serikali, na michango yote hutumika katika miradi ya maendeleo na miradi ya maendeleo ni ya wananchi. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe naomba ukubali mambo haya yasivunjwe.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Marina Joel Thomas na pia nampongeza, maana yake yeye kateuliwa juzi hapa, lakini mchango wake ni mzuri kweli kweli, nashukuru sana amezungumzia juu ya Baraza la Vijana ambalo tayari nimeshalizungumzia, umuhimu wa kuwaweka pamoja vijana kujadili changamoto zao na kupanga mipango ya kupambana na changamoto hizo. Wizara ina dhamira ya dhati ya kulianzisha na kulisaidia baraza hilo.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe, Salma Mussa Bilal swali lake linalohusu vigezo vya kuongezwa fedha za wazee, baina ya wazee wa Sebleni na Welezo, kwamba mafao ya wazee wa Welezo ambao wameongezwa posho lao kutoka shilingi 7,000 mpaka shilingi 15,000 kutokana na wazee hao kupatiwa huduma zao makaoni hapo, ikiwemo milo mitatu kwa siku. Huduma za afya na mavazi, ukilinganisha na wazee wa Sebleni ambao wameongezewa posho lao kutoka shilingi 25,000 mpaka shilingi 40,000.

Mhe. Spika, ninalotaka kulisema hapa ni kwamba wazee wa Welezo hali zao sio nzuri, inabidi washughulikiwe kwa kila jambo, wafuliwe, wakati mwengine waogeshwe, wapikiwe, watandikiwe vitanda, wapatiwe dawa na kila jambo. Ni tofauti na wazee wa Sebleni, wazee wa Sebleni wanapewa shilingi 40,000 wanatayarisha wenyewe chakula, isipokuwa mara hii tunampongeza Mhe. Rais kwa kusema kwamba lazima tuwapikie wazee milo mitatu na hali ya maisha ilivyo, shilingi 40,000 watanunua angalau kitu cha kutamani tu kidogo sio mambo makubwa ya hivyo.

Mhe. Spika, sasa naingia katika ufafanuzi unaohusu vifungu katika kitabu cha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2012/2013. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa ufafanuzi wa vifungu mbali mbali ambavyo vimetajwa na Mhe. Jussa, Mhe. Hamza, Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Bikame Yussuf Hamad. *(Makofi)*

Naanza na Ofisi Kuu Pemba kifungu 220201 ukurasa Nam. 1 kuhusu chakula na vinywaji. Mhe. Spika, kifungu hichi ni kwa ajili ya semina na mikutano yote itakayofanyika kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kama ilivyopangwa kwenye *MTEF* wa wizara.

Aidha kifungu hichi kimebeba pia gharama za chakula, vinywaji, usafiri kwa washiriki wa semina na gharama nyengine za mahitaji ya mikutano, pamoja na kuendesha shughuli zote za uhamasishaji wa vikundi vya vijana, wanawake, watoto, mabaraza yao pamoja na wazee, si kwa ajili ya ofisi tu, lakini kuna kazi nyingi kuhusu kifungu hichi.

Vile vile kifungu hichi kimeongezeka kutokana na upanuzi wa shughuli kazi Pemba, uliotokana na kuongezeka kwa bajeti ya shilingi milioni 80/= kwa mwaka wa fedha 2012/2013. *(Makofi)*

Kuhusu kifungu 220203 hichi kinatumika kwa ajili ya kugharamia viburudishaji katika vikao vya kamati mbali mbali za Idara zote na wageni. Sisi kwa utamaduni wetu jamani tukubalini tukipata mgeni lazima tumpe kidogo viburudisho. *(Kicheko/Makofi)*

Kifungu 220301 safari za ndani ukurasa Nam. 1 ambapo alitaka kujua kwamba fedha hizi shilingi milioni 29,400,000/= ni nyingi ukilinganisha na mwaka, ambazo zilikuwa ni shilingi milioni 17/= tu.

Mhe. Spika, suala hili la ongezeko la fedha katika kipindi hiki 2012/2013 unatokana na safari za kikazi za Maafisa Waandamizi kutoka Pemba kuja Unguja na kwenda Dar-es-Salaam, Vikao vya Kamati Tendaji, Kamati ya Uongozi, Uwasilishaji wa Bango Kitita, Uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara, Utengenezaji wa Mishahara, Vikao vya Bodi ya Zabuni na vyote vinavyohusu kazi.

Kwa kipindi cha mwaka jana 2011/2012 ilibidi wizara kuhaulisha vifungu vya fedha kutokana na safari nyingi na fedha zilikuwa kidogo, ikabidi tuhaulishe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu swali lake Nam. (c) linahusiana na kifungu cha 20509 ukurasa wa Nam. 2 kuhusu Ada ya Ushauri (*Consultant Fee*), alitaka kujua ni kwa nini wizara Makao makuu imeweka kifungu hichi, lakini Ofisi Kuu Pemba imeweka tena suala hili. Hii ni ada ya wawezeshaji wa mikutano, semina na mafunzo mbali mbali yanayofanyika huko Pemba na wala sio Unguja. *(Makofi)*

Kuhusu kifungu 211114 Posho la Nguo za Heshima. Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Bikame Yussuf Hamad, posho hili lilitumika kwa ajili ya sare za walinzi na madereva. Aidha linatumika kwa nguo za baridi kwa wafanyakazi wanaosafiri kwenda nje ya nchi kwa ununuzi wa nguo za kuwahifadhi dhidi ya baridi, kifungu hichi jamani.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Mhe. Spika, napenda kutoa ufafanuzi wa vifungu mbali mbali vya matumizi ya wizara kama nilivyotakiwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Bikame Yussuf Hamad. Nianze na kifungu cha 220200 kifungu kidogo 220201 na 220203 ukurasa wa 4 kuhusu vyakula na vinywaji na viburudishaji.

Vifungu hivyo hutumika kwa matumizi ya kununulia chakula na vinywaji katika mafunzo, vikao na mikutano yote inayoendeshwa na Idara. Kwa mfano, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina shughuli za kupitia Sera ya Uhai, Hifadhi za Maendeleo ya Mtoto, Kuandaa Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar, kufanya mapitio na kuandaa mswada pamoja na Kanuni za Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 1985.

Pamoja na hayo, pia kufanya tafiti mbali mbali, kufanya vikao vya robo mwaka vya masuala mtambuka, kuandaa mikutano mbali mbali ya mashirikiano na wadau wa maendeleo, na kusimamia vikao vya mashirikiano baina ya wizara yetu na wizara ya Tanzania Bara. Kwa kweli sisi hatuna chetu hapa, isipokuwa ni kazi tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kutoa ufafanuzi kuhusu fungu 11108 ukurasa wa 6 juu ya malipo ya kujikimu na malazi. Kifungu hichi kimejumuisha malipo ya kujikimu kwa viongozi wa wizara, ambao ni Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti, tunaposafiri nje ya Zanzibar kwa mwaka mzima.

Aidha kinajumuisha malipo ya kujikimu kwa wataalamu elekezi iwapo watapatikana nje ya Zanzibar, kukamilisha shughuli mbali mbali na hata ndani ya Zanzibar ikiwemo kufanya utafiti, kuandaa sera, mafunzo na kadhalika.

Mhe. Spika, kuhusu kifungu 220300 kifungu kidogo 220301 na 220302 katika ukurasa wa 5. Kifungu hicho hutumika kwa safari za nje na ndani kwa Waheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Maofisa wa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, safari za nje hizo ni muhimu kila mwaka wizara kuhudhuria kutokana na majukumu ya wizara.

Mikutano yenyewe ni pamoja na Mkutano wa *CSWC* Marekani, *CDAU*, *CRC Geneva*, *Social Welfare* Marekani, *ECD* France, Hifadhi ya Jamii, Vikao vya Afrika ya Mashariki na mbali mikutano ambayo haijapangwa, lakini kwa umuhimu wake wizara inabidi ihudhurie. *(Makofi)*

Fungu hili pia linatumika kugharamia safari za kikazi za Pemba na Dar-es-Salaam kwa watendaji kwenda na kurudi. Vile vile fungu hilo pia linatumika kuandaa na kuhudhuria vikao vya mashirikiano baina ya wizara.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, mnaelewa Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri amejitahidi kufafanua, lakini yuko karibu kumaliza. Kwa hivyo, tumpe nafasi pamoja na utulivu, ili tufahamu na iwe wepesi wakati wa kuja kupitisha vifungu, na ikiwa hatukumsikiliza itakuwa ni shida kidogo, baadhi ya maelezo itakuwa hamuyasikii vizuri.

Mhe. Waziri tumalizie, ili tupate muda wa kupitisha vifungu kwa utulivu. Kwa kweli inaonekana Waheshimiwa Wajumbe, wanakaribia kuridhika kwa hiyo unamalizia nadhani.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ufupi nataka niseme kwamba Wizara ya Ustawi wa Jamii haina hadaa wala unyang'anyi, tunachopewa tunaogopa na kutetemeka, lazima kitumike kama kilivyopangwa. Kwa hivyo, kwa upande wa vifungu naomba nimalizie na hilo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna suala la kifungu cha posho maalum katika Idara ya Uendeshaji na utumishi, kimekusudia kulipa maposho ya dhamana kwa viongozi wakuu wa wizara na uendeshaji na utumishi.

Maposho wanayolipwa Madereva na Makatibu Wakuu, Katibu Muhutasi wa Viongozi, matarishi, wakuu wa Masjala ya Siri pamoja na posho la mazingira magumu kwa wafanyakazi wa vituo vya kutunza wale wazee na watoto pia linatoka katika fungu hili la 21110 Posho Maalum, yaani posho hilo linafanya kazi kweli. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kwa sababu inaonekana Waheshimiwa Wajumbe wamechoka kidogo, lakini mimi niko tayari. Mhe. Spika, ufafanuzi wa vifungu vyote hivyo vya posho maalum, ada ya ushauri na kadhalika mujue kwamba si kwa ajili ya matumizi tu, lakini kuna kazi mbali mbali ambazo tunatakiwa sisi tuzifanye.
Vile vile nataka niseme kwamba kuna kifungu cha 221102 cha Mafunzo ya ndani. Mhe. Spika, kifungu hichi kimekusudiwa kulipia gharama za mafunzo kwa wafanyakazi watakaohudhuria mafunzo ya muda mfupi hapa nchini Zanzibar na Tanzania Bara kwa mujibu wa mpango wa mafunzo.

Mafunzo hayo ni mafunzo ya msingi ya kujitayarisha na elimu ya cheti na stashahada, mafunzo maalum ya *computer* pamoja na sheria za kazi, fedha na manunuzi, gharama hizo ni pamoja na nauli, ada ya mafunzo, malazi na chakula.

Kifungu 221104 kuhusu malipo ya ada (*tuition fee*). Kifungu hichi kimewekwa kwa ajili ya kusaidia malipo ya ada ya vyuo kwa wafanyakazi watakaojiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini kwa mafunzo ya stahahada na shahada kwa muda mrefu. Mhe. Spika, ni kweli kuwa fedha hizo ni kidogo, lakini wizara inao mpango endelevu wa kuwaendeleza wafanyakazi wote hatua kwa hatua.

Mhe. Spika, sijui kama watu wako tayari kwamba nitoe hoja. Lakini nataka nimalizie Mhe. Spika, kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia hotuba yangu na wengine wamenipongeza na kusema Mhe. Rais amefanya kazi nzuri ya kunichagua mimi, basi na nyinyi muniamini Waheshimiwa Wajumbe, kwamba jambo hili nitalisimamia kwa uadilifu na *Inshaallah* tutafanya kazi zetu kwa usalama bila ya matatizo yoyote, na tuko pamoja kwa ajili ya kushirikiana na nyinyi kwa hali na mali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, namshukuru Mhe. Waziri kwa kufanya majumuisho kwa muda wa saa 1 na dakika 10, na kwa kiasi fulani dalili imeonesha kwamba tayari mulikwisha tosheka na yale mengi ambayo ameyaeleza Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nichukue nafasi hii tena Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya wizara. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 28 – WIZARA YA USTAWI WA JAMII, MAENDELEO YA VIJANA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunasoma karatasi ambayo tumegaiwa hii na imeandikwa Fungu 28 Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Nafikiri tunayo sote na tunaitumia hiyo.

Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana mama yangu, mlezi wangu ndani ya Baraza hili Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, najaribu kuangalia kifungu 220200 na kifungu hichi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa sitaki nipige tena buti katika vifungu, lakini nataka niunganishe na ukurasa wa 4 kifungu cha 2202. Kwa kuwa sitaki nizuie vifungu vyengine kwa suala hili hili, pia kwenye ukurasa wa 6 inagawa itakuwa si vizuri kifungu 211110 Posho Maalum.

Kwa kifupi hasa, niliwahi kutoa ushauri wakati nilipokuwa nikichangia, kwamba Mhe. Mwenyekiti vifungu hivi vinajirejea na Mhe. Waziri amesema kwamba yeye hafichi chochote. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaamini Mhe. Waziri hafichi yeye. Sasa hizi fedha inawezekana hata yeye pengine matumizi yake hana muda wa kuja kuyaangalia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumsaidia yeye pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wengine mimi niliwashauri Mwenyeviti wenzangu katika kila wizara, kwa sababu haya inaonekana kama *copy and paste*, yaani inabadilika *figure* tu, lakini kwa kifupi gharama zinavyozidi Mhe. Mwenyekiti zinashtua.

Kwa mfano, gharama inapotoka kwenye shilingi 800,000/= mwaka uliopita mpaka shilingi milioni 13/=, kweli tunajua kuna semina pamoja na mambo mengine, lakini kwa nini iongezeke kwa kiasi kikubwa kama hichi na wala sio kifungu hichi, isipokuwa ni vifungu vingi.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu kwamba tunaomba sana kila kamati ijaribu kuangalia mafungu ya wizara zake na siku ya Bajeti ya Wizara ya Fedha, basi tuje tumshauri Mhe. Waziri wa Fedha, ili kamati zikae na wizara husika kwa ajili ya kuyasimamia matumizi haya. Kwanza kupata ile michanganuo na kupata ule uhalisia hasa, kwa nini ikaongezeka na sio mara dufu, isipokuwa ni mara trufu, kwa sababu kama ingekuwa mara dufu ingekuwa haijambo, ingekuwa angalau mara mbili, lakini mara trufu na hali hii imetushtua sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi hatutaki tumpatishe tabu Mhe. Waziri. Lakini tunaomba tu kwamba vifungu hivi vyote tunavipitisha *under probation*, yaani tunaiweka kwenye *incubator*, mtoto bado siku zake za kuzaliwa na fungu tunapitisha. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tutashirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha kwa kila wizara kuja kuvihakiki vifungu hivi, ili matumizi haya kama tutahisi ni makubwa, basi bado tunazo fedha ambazo tulizoziokoa, yaani tuliyopangua kidogo Bajeti ya Mhe. Waziri wa Fedha katika zile fedha za kununulia madeski na tutazichanganya hizi na zitakazo bakia, chakula kitakuwepo, vinywaji na viburudishaji na zitakazobakia tutazipeleka kwenye madawati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tusimuhangaishe Mhe. Waziri, kwa sababu maswali yatakuwa ndio hayo hayo na hata wananchi watakuwa hawatuelewi.
Nafikiri kwa kuokoa fedha za umma, muda, pamoja na kutomshughulisha sana Mhe. Waziri, basi nafikiri fungu hili tunaliacha na kulipitisha, pia nawaomba wenzangu waliozuia mafungu ya aina kama hii ya vyakula na vinywaji, kwenye posho maalum pia yawe chini ya angalizo katika kamati husika Mhe. Mwenyekiti kwa heshima yako na ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikubaliane na Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti, kwamba vifungu hivi basi tuendelee kuvipitisha.

Lakini katika utekelezaji wake kila kamati isimamie wizara yake na tuone kwamba yale matumizi ambayo tunayoripoti hapa sisi Mawaziri ni kweli yanatumika, vyenginevyo basi ikifika miezi mitatu au sita waweze kunishauri mimi, ili fedha itakayozidi katika vifungu hivyo tuweze kuihamisha na kuipeleka katika mwahala ambamo kunahitajika zaidi. Mhe. Mwenyekiti nakubaliana na Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, una nyongeza.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wa Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo yote nakubaliana nayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri kwa makubaliano hayo tuendelee, kwamba mambo haya tunayaweka kwenye *incubation period* au sivyo. *(Kicheko)*

Kifungu 0301	–	Ofisi Kuu Pemba	366,268,000/=
Kifungu 0401	–	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwa kweli mimi ni mmoja kati ya ambao tuliibua maswali mengi kuhusiana na vifungu mbali mbali, na kama nilivyosema kwamba takriban bajeti za wizara zote.

Nimemsikiliza kwa makini mama yangu Mhe. Zainab Omar Mohammed, akitupa uchambuzi pamoja na ufafanuzi wa matumizi hayo. Mhe. Mwenyekiti, katika Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti nilihoji vifungu kadhaa, ili nieleweke vizuri, Mhe. Mwenyekiti naomba nitoe mifano na baadae nioanishe na majibu aliyonipa Mhe. Waziri.

Kwa mfano, katika kifungu cha 211100 Mishahara ya Fedha Taslim chini ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Fungu la malipo ya kujikimu na malazi limewekwa ni shilingi 22,880,000/=. Fungu la viburudishaji katika vote 220200 nasema pamoja na kifungu hichi kwa sababu hoja yangu ni moja tu kwa pamoja.

Kwa hivyo, hapa limewekwa kuna chakula na vinywaji kwa ajili ya semina na mambo mengine shilingi 24,475,000/= halafu kuna fungu la viburudishaji kwa maana ya ofisini shilingi milioni 14,465,000/= na jumla hapo kwenye viburudishaji ni shilingi 38,940,000/=.

Fungu la mwisho nilitolee mfano Mhe. Mwenyekiti kwa ajili ya kuhitimisha hoja yangu liko kwenye *vote* ambayo iko ukurasa wa 5 gharama za safari *vote* 220300, iko juu pale katika karatasi uliyotupa, ambapo safari za ndani ni shilingi 43,580,000/= na safari za nje ni shilingi milioni 49,700,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, nimetoa mifano hii na ninaijumuisha kwa pamoja katika fungu la Idara hii, kwa sababu katika Idara ya Utawala na Uendeshaji, Mhe. Waziri ametuambia kwamba yale mafungu yamenona, kwa sababu yanamhudumia Waziri, Katibu Mkuu na Mkurugenzi. Lakini unapoyakuta mafungu haya katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, ambayo haifanyi kazi inayofanya Idara ya Utumishi na Uendeshaji kwa wizara nzima, yanatia mashaka Mhe. Mwenyekiti.

Sasa masuala haya yanatia mashaka zaidi, kwa sababu ukichukua haya yaliyoandikwa katika hizi, maana yake tumekuwa na utaratibu mpya hivi sasa kila bajeti ikisomwa tunaletewa hii mpya. Lakini ukioanisha na yaliyomo humu Mhe. Mwenyekiti, kuna tofauti kubwa sana katika baadhi ya mafungu. Mimi sitaki kuamini kwamba marekebisho haya yalikosewa na Wizara ya Fedha, na huo ndio umekuwa utetezi wa mawaziri wengi hapa.

Kwa nini Mhe Mwenyekiti nasema hivyo. Kwanza utaratibu hili buku tunaletewa katika kamati kupitisha, kwa hivyo kila kamati inatakiwa ipitishe kifungu kile. Sasa unapotuletea hapa Mhe. Mwenyekiti hii iliyokuwa *lose* na wala hii haikupitiwa na kamati. Kwa hivyo, kusema kweli hii kuja kwake hapa inakosa uhalali, utaratibu na Kanuni za Baraza katika kuzipitia kwenye Kanuni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nisimame hapo, kwa sababu nataka kufupisha na huko mbele nisiendelee kutoa maelezo zaidi. Lakini ukichukua mifano ya mafungu haya niliyokupa Mhe. Mwenyekiti, katika buku hili ambalo ni *original*, utaona watu wamehofia kiasi gani kutokana na tulivyohoji mwanzo na kwenda kubadilishwa na kuletewa hizi ambazo ziko *loose*.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena kwamba siwalaumu Mawaziri, isipokuwa ni watendaji, kwa sababu wao ndio *responsible* kwa haya, kwa sababu mawaziri wetu wengi hawayajui hapa Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa mifano, kulikuwa na fungu katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwenye malipo baada ya saa za kazi shilingi 94,000,000/= kwenye hili buku *original* na huku huioni, ilionekana kwamba watu watashtuka hapa, kwa sababu malipo baada ya saa za kazi yalikuwa ni makubwa zaidi kuliko Fungu la mishahara ambalo lilikuwa ni shilingi 59 milioni kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Vile vile ukienda kwenye vinywaji, sasa imepunguzwa huku juu na itaongezwa wapi na kila idara ipate fedha zake. Kwa hivyo, itakuja kuongezwa katika vinywaji na viburidishaji, na huku kwenye buku *original* ilikuwa ni shilingi milioni 13, na huku kwenye vinywaji na viburudishaji imekuwa ni shilingi milioni 38, sasa mifano kama hiyo Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, ninachosema Mhe. Mwenyekiti, kwamba tunayo *serious reservation*, na mafungu haya yanayoletwa Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie hoja yangu kwa kusema kwamba kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri, kwamba utakuta kila pahala maelezo ni semina, sasa mimi sitaki kuamini kwamba tumeunda serikali kwa ajili ya kufanya semina kila wizara, na ikawa hakuna kazi nyengine za kuwahudumia wananchi, kwa sababu mafungu yaliyonona ndiyo yanayohudumia semina. Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti amemaliza hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi siku ya mwanzo ya bajeti nili-*draw attention* wakati wa Bajeti Kuu nilikuwa mtu wa mwanzo ku-*draw attention* ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwamba mimi Mhe. Mwenyekiti siamini kwamba bajeti yetu ya *recurrent* ya shughuli za kawaida kwamba inapaswa kufika bilioni 307,995,670,000/=.

Kwa kweli mimi naamini kwa kiwango kile alichokitolea mfano Mhe. Omar Ali Shehe kwa bajeti ya Muungano, kwamba angalau asilimia 30 fedha hizi zinaishia katika matumizi yasiyofaa.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba nakubali, kwa sababu hapa hata tukimuhangaisha bure mama yangu Mhe. Waziri, najua hawezi kuyatetea, mimi naamini Waheshimiwa Mawaziri wetu hawajui chochote kuhusu haya, isipokuwa hii ni mipango ya watendaji katika kuficha vichaka ambavyo ndivyo vinavyotumika kufuja fedha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakubali ushauri wa Mhe. Hamza Hassan Juma, lakini nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba hizi ni fedha za wananchi masikini wa nchi hii wanaokamuliwa katika kila manunuzi, mauzaji kuna kodi inayoingia serikalini ndio inayohudumia serikali. Kwa hivyo, tuwe makini kuanzia sasa, na iwe fundisho wakati tunapokwenda kufanya kazi za kamati, tunakwenda kuangalia *value for money* na fedha zilizopo hapo.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, tuendelee, lakini nawasisitiza sana kila kamati na sekta na *PAC* kwa ujumla wake kama ndiye msimamizi wa fedha za serikali, tutayasimamia hayo na tutamsaidia Mhe. Waziri wa Fedha, aokoe fedha hizi na azipeleke kule zinakohitajika katika huduma za wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na yote aliyoyaeleza wala sina matatizo.

Sasa hili kweli ni fundisho kwa sababu hiki kitabu chenyewe Mheshimiwa kilikosewa lakini mimi ninavyoamini kwamba Kamati ya Ustawi wa Jamii waliipitia hii na walivyokwishaipitia ndio sisi tukaleta haya marekebisho. Sasa kama bado hayajaaminika haya inaonekana kama yana wasi wasi basi utaratibu baadae ufuatwe.

Mhe. Mwenyekiti: Nyongeza **Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo**: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hoja ambayo ameeleza Mhe. Jussa ni kwamba fedha hizi zitumike kulingana na mahitaji.

Mimi nataka nimuhakikishie tu kwamba Ofisi yangu itakuwa macho pamoja na Kamati tutashirikiana ili tuhakikishe kwamba kila fedha imetumika kwa mujibu wa mahitaji na wala sio vyenginevyo, kama fedha itajitokeza kuwa ni ya ziada katika eneo lile basi tutaihamisha ili tuipeleke katika maeneo ambayo yanayohitajia fedha, mfano umeelezwa hapa madeski, hilo tutalisimamia Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba mimi ninaamini kwa hapa ndio maana ninasema ninakubali busara ya Mhe. Hamza tuliyoitumia hata juzi, ninasema kwa dhati Mhe. Mwenyekiti, mimi siamini kwamba haya ni matatizo ya Waziri pengine wao hawawi sana katika mafungu haya kwa sababu wanaokuja kuyatetea mafungu haya ni wao, kwa hivyo ninasema nimekubali na hoja iliyotolewa na Mhe. Waziri, ninaikubali hoja iliyotolewa na kaka yangu Mhe. Waziri wa Nchi Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba tuyapitishe, na kwa hivyo ninadhani huko mbele mengine tutayaachia yale ambayo kama haya, mengine tutayahoji, lakini haya mengine tutaachia kwa sharti kwa hilo la kwamba Kamati zitakwenda kufanya kazi sana kujiridhisha kwa pamoja na baadae PAC ije ifanye kazi yake kwa zile *quiries* ambazo zitakuja kufanywa kazi zake kwa sekta tutazipasisha kwa Kamati ya PAC ili na wataalamu zaidi ifanye kazi zake. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, ninasema tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mama yangu wala asiwe na wasi wasi kwa kusimama kwangu, hii ni sawa sawa na chura kumpigia teke unakua unamsaidia mwendo, wala asishtuke kwa kusimama kwangu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hii nitaomba sana Mhe. Waziri wa Fedha kama Mhe. Waziri maelezo yake yatakuwa hayajanitosheleza Mhe. Waziri wa Fedha aje anisaidie zaidi.

Hoja yangu hapa ni kuhusu kuundwa kwa Benki ya Wanawake. Nilimsikia sana Mhe. Waziri wa Fedha akitoa ufafanuzi kuhusu suala la study ambayo imefanywa na Wizara na wakapata ushauri wa BOT kuhusu mtaji wa kuanzisha benki ambayo itakuwa inaitwa Benki ya Wanawake au Benki ya Maendeleo ya Wanawake pengine na Vijana.

Alieleza kwamba capital ambayo ili iweze kuanzisha benki ya aina kama hii, zitapatikana bilioni kumi na tano.

Mhe. Mwenyekiti, *regulator* wetu wa mambo ya uchumi ni BOT, lakini BOT yenyewe wametuthibitishia kuwa huwa wanapata wakati mgumu katika ku-*regulate* shughuli mbili tofuati; uchumi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na uchumi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, halafu kuweza kuweka vile vigezo.

Sasa nilikuwa nataka hapa nipate ufafanuzi kwa sababu mimi ninavyojua *capital* ya benki inategemea vile vile na mazingira halisi ya wale ambao wanaotaka kuanzishiwa ile benki na ule mtaji utakavyoweza kuwatosheleza kwa kiasi gani.

Sasa nilikuwa ninataka nijue jee hii *capital* ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Wanawake ni kwa Tanzania nzima, hii *capital* ya bilioni kumi na tano. Maana yake kule Bara tunajua tayari imeshaanzishwa lakini jee *capital* ya bilioni kumi na tano ilikuwa vile vile ni kigezo kwa hapa Zanzibar, kwa sababu kwa upande wa Tanzania Bara wenzetu ile benki mtaji wake inatakiwa uweze ku-*cover* watu milioni arobaini na sita ambao kwa kuweka *ratio* ya wanawake itajulikana ni asilimia ngapi, lakini hata *population* ya watu ya milioni moja na laki tatu pia mtaji wa kuanzisha benki hii, sasa hebu tungelipata ufafanuzi kwa sababu pengine kutokana na jiografia na *population* ya Zanzibar lakini vile vile na biashara za wanawake wa Zanzibar ambao si wengi wanazo biashara zinazoanzia milioni kumi, wafanyabiashara wanawake wa Zanzibar sana ni milioni tatu mpaka tano, basi pia hii benki ianzishwe kwa *capital* ya bilioni kumi na tano, hatuoni kwamba maendeleo ya Zanzibar hasa wanawake tunaweza tukayakwamisha kwa kulinganisha *capital* ya Zanzibar na *capital* ya Tanzania Bara, nilikuwa kidogo ninataka ufafanuzi kwa Mhe. Waziri kama atahisi kidogo asaidie Mhe. Waziri nipo tayari, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo nitoe ufafanuzi juu ya suala ambalo Mhe. Hamza anataka tumsaidie.

Kuanzisha benki kwa maana ya *commercial bank* pahala popote Tanzania mtaji wake ni bilioni kumi na tano. Benki itakapoanzishwa haimzuii mtu wa upande mwengine wowote kuja kukopa na kuja kuweka *deposit.*

Kwa hivyo unapokuja kuianzisha Zanzibar ni sawa sawa unapoianzisha Mwanga au Kagera, wewe unaweza ukenda ukakopa na unaweza ukenda ukafungua akaunti yako pale. Kwa hivyo unapoianzisha benki maana yake *population* yako si *population* ya watu milioni moja nukta tatu ni *population* ya bilioni arobaini ya watu wote.

Lakini unapotaka kuanzisha benki ambayo iwasaidie jumuia tu ya watu fulani, kuna kitu tunakiita *community bank*. Wanawake wa Zanzibar wanaweza wakaanzisha kitu tunakiita Zanzibar Community Bank, mtaji wake ni mdogo kidogo. Unaweza ukaanza na mtaji wa milioni mia tano yaani nusu bilioni.

Kwa hivyo mtaji huo unaweza ukaanzisha Zanzibar Women Community Bank na benki hiyo ikakua na hatimaye ikafikia mtaji wa bilioni kumi na tano na ikaweza ikajigeuza wenyewe ikawa ni benki kamili.

Nitatoa mfano kamili. Mfano mzuri ni Dar es Salaam Community Bank imeanzishwa kama ni community bank, lakini leo ifanye vizuri Dar es Salaam Community Bank kwa mtaji walionao wakai-*turn into bank* na unaweza ukatoa mikopo hiyo lakini kuna masharti tofauti ya uanzishwaji. Community Bank inasema kwamba share holder mmoja hawezi aka-*own share* zaidi ya asilimia 20.

Kwa hivyo hili suala tunaliangalia kwa undani kabisa na nimejaribu kuzungumza na wenzangu Wizara ya Wanawake, leo mchana nimezungumza na PBZ, kuna study wao waliifanya miaka ya nyuma sana na ushauri wakautoa serikalini nimewaomba waniletee kesho na baadae tuwe na kikao cha pamoja baina ya sisi na Wizara ya Wanawake, Wizara ya Uwezeshaji Kiuchumi pamoja na BOT na PBZ yetu ili tuone tunalichukuaje hili suala na hatimaye tulipatie ufumbuzi.

Lakini nataka nimtoe wasi wasi ndugu yangu Mhe. Hamza kwamba nia yetu hasa ya kuanzisha benki yetu ambayo itakayosaidia wanawake ipo, kinachotutanza hapa ni kwamba tuanze na community iweze kukua au tuanze na benki moja kwa moja ambapo taratibu za kuweza kupata mtaji tunaziangalia vile vile.

Ninamuomba Mhe. Hamza avute subra na akitaka elimu zaidi mimi nipo tayari kumuelimisha zaidi ili tuweze kulifahamu hasa suala hili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri wa Fedha kwamba kwa kuwa nia yake na nia yangu ipo sahihi, kwamba tuweze kuwa na benki ambayo itakayoweza kuwasaidia hasa akina-mama wetu ambao wao hasa ndio zaidi ndio wenzi waliotuleta hapa.

Sasa nilikuwa na ushauri. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri akae karibu sana BOT, unajua **BOT** Wazanzibari wengi bado wanasikitika mpaka wafanyabiashara bado katika ile mikopo wanayoitoa mfano ule *small medium enterprises*, wenzetu Bara kule wanapata bilioni nne kwa mtu mmoja, hapa Zanzibar mpaka leo bado hakuna mtu yeyote au mfanyabiashara yoyote ambaye amepata.

Sasa wangelikaa wakajaribu kuangalia zile fursa ambazo BOT wanatoa kwa upande wa wenzetu wa Tanzania Bara, lakini vile vile kwenye bajeti ya mwaka huu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wametoa fedha katika bajeti kuu ya serikali kuingiza katika BOT yaani Tanzania Investement Bank, yaani fedha zimetoka ndani ya mfuko mkuu wa serikali kwa kuingiza mtaji pale ili iweze kukopesha watu wengi.

Sasa nadhani Wazanzibari wana hamu kubwa sana kusikia kwamba serikali yao inatoa fedha katika mfuko wake ambayo ndio kodi ya wananchi inaanzisha mtaji, BOT na wao waangalie mazingira kwa Zanzibar ilivyo waanzishe hiyo benki.

Lakini vile vile na akina mama kuweza kuji-*organize* kuanza hiyo community bank. Mimi ninafikiri ili mwakani tuwe na kauli ya kusema kama tumeshindwa mwakani basi alau mwaka wa mwakani wanaanzisha.

Kwa sababu mimi nilipoambiwa bilioni kumi na tano, sisi tuliwahi kupata semina kutoka BOT na wakatwambia Waheshimiwa kama munaweza mukajikusanya mukiwa na milioni kumi na tano munaweza mukaanzisha benki.

Sasa mimi ndio nikawa ninajiuliza sisi tunashindwa kitu gani. Lakini bado na mimi nilikuwa na ushauri wangu na nilikuwa naomba sana sasa hivi Mhe. Waziri ana wataalamu wazuri tu pale wizarani, Mhe. Waziri wa Fedha yeye ndiye mwenye taasisi zote za fedha Zanzibar, ninaamini tunaweza tukapata pahala pa kuanzia.

Huo tu ulikuwa ndio ushauri wangu. Ninakushukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mhe. Waziri hana pingamizi juu ya hilo kufanya mashirikiano na wizara hapa ya Nchi, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na hizo *study* ambazo zimefanywa na PBZ kwa kushirikiana pamoja na Benki Kuu ninadhani hana matatizo Mhe. Waziri au kuna maelezo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina uzoefu wa kuanzisha mipango hiyo.

Lakini ninachotaka kukisema ninadhani kishamaliza pale ndugu yangu Wizara ya Fedha kwamba sisi kwa vyovyote tunataka kuanzisha benki ni lazima tupate pesa, yaani serikali itoe mchango mkubwa wananchi watoe michango yao midogo midogo kupitia SACCOS zao, iwe kama ni kiongezeo.

Sasa kama serikali bado hatujakuwa na mchango benki bado hatujaifungua.

Mhe. Mwenyekiti: Kimsingi Waziri anakubaliana na ushauri wote uliozungumzwa hapa. Tunaendelea.

Jumla ya Kifungu **Shs.318,000,113**

Kifungu 0501 Idara ya Wanawake na Watoto Shs.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru tena Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu kama alivyoukariri kabisa na kwa usahihi Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, nilizungumzia suala la utekelezaji wa sheria ya mtoto au haki za mtoto kwamba inaonekana pamoja na sheria ile kujumuisha vifungu vinavyohusu wajibu wa mtoto kwa kulingana na mahitaji ya jamii ya nchi kama zetu badala ya jamii za Kimagharibi ambazo zinasisitiza zaidi haki kuliko wajibu.

Nikasema katika utekelezaji hotuba ya Mhe. Waziri imejikita zaidi kuzungumzia haki, nikasema hii inaonekana ule wajibu uliingizwa mule ili kulainisha tu waliokuwa na hoja zao lakini katika utekelezaji hauonekani uhalisia wake.

Sasa Mhe. Waziri katika majibu yake Mhe. Mwenyekiti, kaniambia kwamba ushauri wangu anaupokea ninafurahi, lakini angeishia pale nisingesimama. Lakini katika majibu yake akasema kwamba katika utekelezaji wa hilo wameunda Mabaraza ya Watoto ambayo ni miongoni mwa kazi zake ni hilo.

Sasa hili kidogo mimi ninapata wasi wasi, hivyo nilikuwa ninataka anihakikishie tu kwa nini nikasema hili Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika hotuba yake kwenye *paragraph* nambari 77 kayazungumzia Mabaraza ya Watoto, tumeshayasikia lakini hata yeye mwenyewe ukiona nisome mstari mmoja tu au sentensi moja tu inasema kwamba “Lengo la kuanzishwa kwa Mabaraza hayo ni kuwawezesha watoto kuwa na chombo chao cha kusimamia masuala yao, kujiamini na kutambua haki zao”.

Kwa hivyo inaonekana haya majibu mengine tunayoletea sasa yanaongezewa lakini kwa *policy* hasa ya wizara bado *emphasize* ni haki. Sasa mimi sitaki tuhangaishane na Mhe. Waziri, inaonekana bado mkono mkubwa kwenye kusukuma mambo haya ni washirika wa maendeleo na mashirika ya kimataifa.

Nimuombe Mhe. Waziri na watendaji wake katika hili na wao hata tukipewa ushauri wenyewe nchi ni sisi Wazanzibari. Kwa hivyo sisi ni kuangalia kulingana na mwenendo wetu wa jamii ulivyo na jinsi gani tuna-*balance* sawa sawa baina ya haki na wajibu wa mtoto katika jamii yetu.

Nimuombe tu Mhe. Waziri kwamba alichukue akalifanyie kazi *serious* isiwe tu ni kauli ya kunijibu Mwakilishi hapa ili vifungu vipite. Lakini ninasema ukisema kwamba Mabaraza ya Watoto unashughulikia hotuba yako hii haijielezi hivyo.

Kwa hivyo nilikuwa naomba sasa alichukue kwamba katika utekelezaji wa hili tuone kuna *right balance*, kuna uwiano unaokubalika kabisa wa kufundisha watoto wa Kizanzibari, Mabaraza ya Watoto wasiwafundishe kujiamini tu wakawashupalia wazee, lakini wawafundishe vile vile na wajibu wao kwamba watoto unapowarudi kama sheria inavyosema wajue kutii na kufuata vile vile, naliomba sana suala hili kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri kuna maelezo yoyote.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Jussa alitueleza habari na mimi ninakubaliana na yeye kwamba huwezi kupata haki kama hujafanya wajibu.

Kwa sisi tutalifuatilia jambo hili ili tuone katika shughuli zetu kuna haki na wajibu, sio kuwa haki peke yake tu lakini lazima kwanza watu wafanye wajibu wao halafu wapate haki yao. Hivyo hilo tutalifanyia kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Waziri kwa kulikubali hilo na ninaamini katika kuanzia kupokea ripoti za Kamati za Baraza utekelezaji wa bajeti hizi mwezi wa tatu mwakani na katika bajeti ijayo tutapata ripoti ambayo inatuonesha haki na wajibu wa mtoto unatekelezwa kiasi gani.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, ninasema tuendelee. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nilipokuwa nikichangia, nilipokuwa nikizungumzia fungu 272100 ukurasa wa 8 nilisema kwamba fungu hili la maendeleo ya wanawake na watoto katika suala zima la misaada, yaani hapa ninasema maendeleo ya wanawake na watoto, yaani ni misaada ya kijamii kwa wanawake na watoto.

Mwaka uliopita yaani 2011/2012 walitenga milioni kumi lakini bajeti ya mwaka huu 2012/2013 wametia milioni nne. Sasa Mheshimiwa tunamsifu sana kwa kuweza kutunza watoto, wanawake lakini mbona safari hii mwaka huu, mwaka uliopita ulitenga shilingi milioni kumi lakini mwaka huu umetenga milioni nne.

Na tunaona kwamba wimbi hivi sasa la wanawake wenye matatizo, wanaoomba, watoto wa mitaaani wanaongezeka, kwa nini hizi fedha umezipunguza.

Sasa hapa kidogo nilikuwa nataka maelezo na vile vile nilikuwa nina ushauri, kama hizi fedha tulizipunguza labda kutokana na uhaba wa bajeti basi tungeliangalia yale mafungu ambayo tumeyapigia kelele yamezidi sana yakaongezewa hapa, kwa sababau sasa hivi wakati huu uliokuwepo hivi sasa hasa hawa wanawake na watoto kila tunayemkuta na dhiki basi ziwepo fedha alau za kuweza kuwasaidia.

Sasa Mhe. Waziri fungu hili sijui kama amenisikia nikizungumza lakini nilisikitika kidogo kwamba fedha zimepungua kwa bajeti ya mwaka huu.

Sasa Mhe. Waziri kama alikuwa na maelezo kidogo ninaomba msaada wake. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli fungu ni dogo sikatai mimi lakini ndio tulichokuwa nacho.

Sasa kama kutakuwa na utaratibu mwengine tutakaofanya kwa kuongezewa hili fungu, mimi nitashukuru Mwenyezi Mungu. Lakini hili fungu ndilo tulilonalo.

Mhe. Mwenyekiti; Ninafikiri Kanuni hazitupi nafasi ya kuongeza fungu isipokuwa kwa ushauri alioutoa Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwa ile kazi ya pamoja itakayofanywa na Kamati, watakapoona kwamba kuna sehemu fulani fedha imezidi kabla haijaamuliwa kupelekwa Hazina tunaweza tukatizama mapungufu kama haya ninadhani.

Lakini kimsingi kuongezea fungu nje ya pesa hizi, hiyo hata Kanuni yetu inatukataza. Lakini ushauri uliotoka pale ninafikiri si ushauri mbaya, kazi ya pamoja ya Kamati inayohusika kusimamia na kufuatilia matumizi na tukiona kuna kitu ambacho kingeweza kurejeshwa Wizara ya Fedha pengine kabla ya kwenda huko basi tuangalie mapungufu kama haya.

Kuna maelezo yoyote mengine.

Mhe. Mwenyekiti: Nyongeza **Mhe. Waziri wa Nchi, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo**: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ambayo umeyatoa lakini sheria za fedha vile vile zinampa uwezo Waziri wa Fedha kuhaulisha kutoka kifungu kimoja kupeleka kifungu chengine baada ya Baraza lako Tukufu kupitisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ninadhani kuna lolote tunaendelea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba ifanywe hivyo ili hili fungu aidha kama litakuwa liwe la mwaka jana au kama kutakuwa hakuna budi kama mahitaji yapo, kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha ana uwezo huo basi aje aruhusu ili watoto wetu na wanawake wanapopata matatizo waweze kusaidiwa. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Tufanye hivyo kwa mashirikiano ya Kamati kama ilivyoshauriwa mapema. Tunaendelea.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kunijibu lakini nilikuwa ninataka ufafanuzi nilipokuwa nikichangia kuhusu mtoto ambaye aliyeibiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja hata Mhe. Wanu alipokuwa akichangia alisema kwamba yule mwanamke anadunda.

Nilikuwa ninataka ufafanuzi kwamba mwanamke huyu amechukuliwa adhabu gani kama wewe ni mama.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, kwamba mwanamke alikamatwa na kwa bahati mtoto na yeye alipatikana. Lakini baadae huyu mwanamke alikimbia.

Lakini sasa sisi kama Wizara tutafanya kazi ya kufuatilia zaidi ili tumpate na tumpeleke kwenye vyombo vya sheria.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi ninadhani kwamba walichukua hatua hiyo walimfuatilia lakini kwa maelezo mafupi tunaambiwa yupo mtaani anadunda. Sasa kutokana na hali kama hiyo ikiwa yupo mitaani anadunda, kwa hivyo nadhani atakubaliana na mimi kushirikiana na wanawake ambao wanaomjua anakodunda na kuchukuliwa hatua ili kukomesha vitendo hivi vya kuibiwa watoto ovyo ovyo. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Jumla ya Kifungu **227,777,000/=**

Kifungu 0701 Idara ya Maendeleo ya Vijana

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia asubuhi suala hili la Baraza la Vijana la muda mrefu na vijana wanazidi kuteseka Mhe. Waziri alinijibu wakati wowote litaanza, hata hivi sasa ni wakati wowote, ninataka anipe *specific time* lini litaanza.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kazi yote ya kuunda rasimu ya Katiba tayari tumeshakamilisha.

Sasa hivi tumeipeleka hii rasimu ya Katiba kwa Mwanasheria Mkuu. Sasa huko tunasubiri maelezo ya kitaalamu kwamba tufanye nini ili tulianzishe hili Baraza, hatuwezi tu tukasema tuanzishe tu hivi hivi ni lazima kuwe na ufuatiliaji kwa sababu tulianza zamani kufuatilia tukaona kwamba kwa hatua ya kwanza ile tulifeli ikabidi

tukafuatilia kwa hatua ya pili. Sasa hivi tupo katika hatua nzuri, tupo kwa Mwanasheria Mkuu tunasubiri utaalamu wa Mwanasheria Mkuu.

Kwa hivyo namuomba awe mstahamilivu huyu ndugu yangu Jaku lakini kusema nimwambie kesho kuwa Baraza la Vijana litakuwa tayari itakuwa ninasema uongo.

Mhe. Jaku Hashim Ayou: Mhe. Mwenyekiti, kama yupo Mwanasheria Mkuu atufafanulie zaidi hili ili nipate kufahamu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niungane na Mhe. Waziri kwamba nikiri kuwa kweli tumepokea rasimu ya Katiba ya Baraza la Vijana na Mhe. Waziri anafahamu na mimi mwenyewe ninafahamu kwamba tumewapa watu wetu kuweza kulifanyia kazi.

La msingi ni kuangalia iundwe katika utaratibu gani *statutory* au ni kama jumuia yaani kama ni *foundation*, ndio jambo ambalo tunalolifanyia kazi.

Nimuahidi Mhe. Jaku na Waheshimiwa wengine kwamba ni jambo ambalo tutalipa umuhimu unaostahiki ili hili jambo liweze kufanyika katika muda mfupi ujao kadri itakavyowezekana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile kaingia Mwanasheria Mkuu mimi sina tatizo naye tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu vile vile nilitaka maelezo kuhusiana na *vote* mbali mbali katika Idara hii ya Maendeleo ya Vijana hasa katika fungu la 211100 Mishara na fedha taslimu.

Sasa bahati Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika kutoa ufafanuzi hakufika mpaka mwisho tukapata uhalisia wa vile vifungu. Lakini niliunganisha hili ambapo ninataka Mhe. Waziri anisaidie kwamba huku kwenye malipo baada ya saa za kazi, vikao na kamati kumenona lakini ukienda katika *vote* kwenye ukurasa wa 11 ambayo ni misaada ya kijamiii 27200 Maendeleo ya Vijana kuna zero kabisa mwaka huu wa fedha, mwaka jana kulionewa huruma kuliwekwa milioni kumi, mwaka huu ni zero kabisa, sasa nataka maelezo. Naomba katika hili Mhe. Waziri anisaidie maelezo kwa sababu hiyo shughuli hasa ya idara ingepaswa kwenda kusaidia vikundi vya vijana, huko kuna zero Mhe. Mwenyekiti, huku kwenye uendeshaji na utawala ndio kulikonona, naomba Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, tunajiandaa kisawa sawa kwa Baraza la Vijana.

Hivi sasa ninataka kumwambia Mhe. Jussa tumeweka fungu kwa ajili ya kukodi kwa sababu hatuna nyumba hivi sasa ya kuwaweka vijana, lakini tumeweka fungu kwa ajili ya kuwakodia nyumba.

Sasa hivi tumeshanunua vespa kwa ajili ya ufuatiliaji viongozi watakaochaguliwa angalau wawe na kitu cha kutembelea. Lakini pesa hasa za kusema kwamba Baraza la Vijana likiingia tu pale madarakani likishaundwa tuna fungu fulani kwa ajili ya kujiendeshea hiyo bado Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema mimi sina tatizo na Baraza la Vijana, kwa sababu nadhani hili limeshatolewa ufafanuzi vizuri kutokana na hoja aliyoiuliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, na bahati nzuri na Mhe. Mwanasheria ameichangia, hiyo sina tatizo nayo.

Nilikuwa nasema kwamba ukiyatizama mafungu haya kwenye mishahara ya fedha taslim yamenona, yamechukua 99 milioni, kati ya milioni 171 za Idara hii, milioni 99 yaani takriban milioni 100. Milioni tisini na tisa, laki nane hamsini elfu (99,850,000) zipo katika fungu la mishahara ya fedha taslim, mbali nyengine zimeingia katika michango ya hifadhi ya jamii, kwenye gharama za simu, viburudishaji, gharama za safari. Hii ndiyo *priority* ya Wizara. Lakini kule kwenye uhalisia kunakofanya kazi ndio iundiwe Idara hii ambayo ni misaada ya kijamii, ruzuku katika mifuko ya kujitegemea vijana kuna ziro ziro, ndio hoja yangu Mhe. Mwenyekiti.

Mimi sihoji kwamba wametenga fedha kwa ajili ya kulipia nyumba kwa ajili ya Baraza la Vijana, nasema huku kwenye shughuli hasa iliyopaswa ya vijana, huku kuna ziro ziro, Mhe. Mwenyekiti. huku kwenye shughuli za utawala na uendeshaji Ofisi ndio asilimia nafikiri takriban tukifanya hesabu hapa 90 inafanya Idara hii zimejikita hapo. Nataka maelezo kwamba kwa nini tuiidhinishie fedha, Idara hii ambayo haiendi kufanya kazi yoyote kusaidia vijana zaidi ya kufanya shughuli zake za utawala kwa asilimia takriban 90 ya fedha ambazo zimeombwa. Kwa nini tuziidhinishe hizo Mhe. Mwenyekiti, naomba anisaidie.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Ismail Jussa naomba ushauri wake tufanyeje?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nimeona *concern* ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, lakini nataka niseme tu kwamba utaratibu ambao tumeupendekeza mwaka huu, na tunadhani utatusaidia sana kuweza ku- *monitor* pesa ambazo tutakazotuwezesha vijana, tumepeleka bilioni 1.1 kwenye Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kule ndio mtakapoziona na kule ndipo ambapo kutatolewa maelezo ya kina hasa jinsi gani hawa vijana wataweza kusaidiwa kupitia mpango huu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ufafanuzi ambao umethibitisha hoja yangu kuu katika Bajeti hii, kwamba kumbe hakuna haja ya kuwa na Wizara hizi mbili tofauti, tunaongeza bure gharama za utawala na Uendeshaji kwa Idara ya Vijana ambayo shughuli zake hasa halisia inayosaidia vijana zipo katika Wizara nyengine kabisa. Kwa hivyo hapa tunataka tuidhinishe milioni 171 ambazo zingeweza kwenda hospitali zikatumika kwa dawa nyengine zingeweza kwenda skuli zikasaidia kupata madeski. Lakini kaziweka kwa utawala ambao shughuli zake za utendaji zinafanyiwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zikawekwa bilioni moja.

Mhe. Mwenyekiti, nakubali sitaki kumuhangaisha sana Mhe. Waziri, nakubali tuendelee. Lakini nasema hili ni suala ambalo kwa majibu haya imethibitishwa kwamba serikali inapaswa kujiangalia katika muundo wa wizara zake. Isiwe tunachukua fedha nyingi tunaziidhinishia katika shughuli za utawala na uendeshaji wa mambo ambayo kumbe kazi zake zinafanywa na mwengine, na yeye pia ana fungu lake katika utawala na uendeshaji. Kwa hivyo ndio nikasema tunaishia kuwa na bajeti kubwa ya shughuli za kawaida *recurrent*, ambayo haihitajiki inaweza kuokolewa ikenda ikahudumia wananchi wanyonge katika mahitajio yao mengi ya msingi. Pengine hizi zingeweza kuongezea huko kwenye mfuko wa vijana zikapeleka zaidi huduma kwa vijana kuliko kubakia hapo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema tuendelee lakini nadhani *concern* ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi, Mipango na Maendeleo tumeielewa. Ahsante sana Mheshimiwa.

Kifungu 0401 171,068,000

Kifungu 1101 Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kuna yale mafungu mengine siyahoji tena kwa sababu yale tumeshakubaliana tutayashughulikia kupitia Kamati. Lakini kuna *concern* moja hapa ya msingi kabisa, hii namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo. Mhe. Mwenyekiti katika mambo mengi niliyoyahoji katika Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja, nilihoji katika ukurasa wa 15 kwenye *vote* 220400 gharama za mafuta na vilainisho. Mwisho kwenye *sub vote* kuna gharama za umeme. Hapa imewekwa milioni kumi na saba, laki tisa sitini na nane alfu (17,968,000). Nilihoja hili kwamba kunatumika umeme wa aina gani katika Idara hii kwa mwaka, kwamba ni milioni 17 ambayo ni wastani wa takriban milioni moja na nusu kwa mezi.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema wakati ule ili hoja yangu ifahamike vizuri kwamba nimepata mashaka zaidi kama nilivyosema inaonekana kuna michezo michezo ya watendaji. Ukitizama katika buku hili awali ilikuwa milioni 33.9. Nafikiri baada ya kuwa tunahoji imepunguzwa mpaka imefika milioni 17. Lakini hata hizo milioni 17 bado ukitizama wastani wake kwa mwezi ni takriban milioni moja na nusu. Idara moja tu sio Wizara tunatumia fedha hizi namuomba Mhe. Waziri katika hili anipe maelezo kwa nini tupitishe fungu hili kubwa sana kwa gharama za umeme. Utendaji huo wa Idara ya Ustawi wa Jamii shughuli zake za kiofisi hazina shughuli ambazo zinahitaji umeme, kama kuendesha jenereta au kuna viwanda kiasi cha kuendesha umeme mwingi kiasi hichi. Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Ismail Jussa, nataka nimwambie Mhe. Ismail Jussa sisi tulivyofika hapa katika Wizara hii tulikuta deni kubwa la umeme hasa kwa wazee. Kwa hivyo tunalilipa kidogo kidogo, lakini bado deni ni kubwa. Kwa hivyo pesa hizi ni kwa ajili ya lile deni la zamani na hivi sasa tunaendelea pia kulipa kidogo kidogo. Deni la umeme la majumbani, mambo ya kulipia maji na kadhalika. Kwa hivyo hapa palikuwa na deni kubwa ndio maana ukaona kuwa figa hii ni kubwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mhe. Waziri kwa maelezo yake mazuri nadhani kamati itafanya kazi vizuri kuthibitisha deni hilo na kujiridhisha, kujua kama kweli fedha hizo zinakwenda huko baada ya maelezo hayo naomba tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka Waziri anifahamishe tu hichi kitengo cha DNA kipo katika Wizara ya Afya, kipo kwake au kipo katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimjibu Mhe. Jaku Hashim kwamba hichi chombo cha DNA hasa dhamana ni Wizara ya Afya, lakini zaidi nataka nimwambie kwamba sasa hivi kimo ndani ya *container* kinakuja karibu kufika hapa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kauli ya Mhe. Waziri Mhe. Waziri, maana yake hichi chombo ni ghali na kina gharama kiuendeshaji.

Kifungu 1101	Idara ya Ustawi wa Jamii Unguja	616,379,000
Kifungu 1102	Idara ya Ustawi wa Jamii Pemba	84,000,000
Kifungu 1201	Idara ya Utumishi na Utawala	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti katika Idara ya Utumishi na Utawala nilihoji vifungu vingi mimi na Mwenzangu Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa jimbo la Kwamtipura.

Kama nilivyosema vile vyengine sitaki maelezo kwa sababu tumeshakubaliana kimsingi, kwamba kamati zitafatilia naamini watafanya kazi ya kusimamia fedha za walipa kodi wa Zanzibar vizuri.

Hoja yangu ninayoitaka anijibu Mhe. Waziri ni moja tu ipo katika hii karatasi aliyotupa ukurasa wa 19 juu kabisa pale ambapo kuna *vote* chini ya gharama za mafuta na vilainisho, vile vile kuna *vote* 220408 gharama za umeme. Hii sasa ni kwa Makao Makuu ya Wizara kwa sababu ipo chini na Idara ya Utawala na Utumishi pale, vile vile pana jumla ya shilingi kumi na tano milioni na laki sita (15,600,000).

Nilikuwa naomba Mhe. Waziri anisaidie, je na hapa palikuwa na deni la miaka mingi?

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, madeni tumeyakuta na tunayafanyia kazi. Lakini hata hivyo sasa hivi tunalazimika kutumia umeme mwingi zaidi kuliko tulivyokuwa tukitumia zamani, kwa hivyo na pesa ni lazima ziongezeke.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa sababu Kamati tumesema zitakwenda kukagua na hili nalo tutalipeleka huko huko, kamati itajiridhisha. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nahitaji maelezo kidogo katika huu ukurasa wa 18 mwisho kabisa, kifungu cha 220402 gharama za dizel. Mwaka uliopita 2011/2012 walitenga shilingi laki moja na ishirini (120,000), mwaka huu 2012/2013 shilingi milioni ishirini na mbili laki tano (22,500,000), nilikuwa nahitaji tu maelezo kwa sababu hizi ni gharama za dizel. Gharama za petrol kifungu cha 220401 mwaka uliopita ilikuwa milioni nne na laki nane (4,800,000) na mwaka huu milioni saba na laki tano (7,500,000) hii sina matatizo nayo. Kwa sababu tunajua bei ya mafuta imeongezeka pengine na shughuli kidogo zimeongezeka. Tatizo langu kwenye dizel kutoka shilingi laki moja na ishirini (120,000) mwaka uliopita mpaka shilingi milioni ishirini na mbili na laki tano (22,500,000). Kidogo hapa nilikuwa nahitaji ufafanuzi. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli gharama zimezidi kwa sababu sasa hivi kazi ni nyingi, umeme ukikatika ni lazima tuwashe majenereta. Ni lazima

tupate mafuta ya kutosha. Ufatiliaji wa mambo chungu nzima yaliyokuwepo vijijini, kwa hivyo ni lazima tuwe na mafuta ya uhakika. Tunalipia mapema hata ikiwa hakuna dizel sisi tunakuwa tuna hakiba ya mafuta yetu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Kamati hayupo na ndio tunapitisha bajeti yake. Lakini nadhani Makamo Mwenyekiti yupo nilikuwa naomba tu ajaribu katika ile miwani ya kufatilia, kwa sababu laki moja na ishirini mpaka milioni 22 hii siyo mara dufu mara trufu, trufu, trufu. Hii kidogo nilikuwa naomba kidogo Makamo Mwenyekiti wa Kamati kidogo na hili. Kwa sababu Waziri wa Fedha alituomba sana Waheshimiwa tujitahidi kila mnapohisi kuna fedha za wananchi tunaweza tukaziokoa niambieni. Kwa hiyo ile jitihada aliyotuomba na mafunzo uliyotupa nadhani safari hii bango kitita litabakia na kapu ya pesa za kutosha. Mheshimiwa naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri kamati itakapofikiria hili waangalie hii ya nyuma nayo ilikuwa ni kweli, maana shilingi laki moja ishirini (120,000) sijui kama si matumizi ya wiki moja. Inawezekana ikawa kuna makoseo sina hakika. Lakini kamati izingatie na hili la shilingi laki moja na ishirini (120,000) ni pesa ndogo mno. Nadhani matumizi kwa wakati huo labda ya wiki moja na sijui kama inatosha hiyo wiki moja.

Kifungu 1201	Idara ya Utumishi na Utawala	625,395,000
Jumla ya Fungu		**2,409,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 28 - WIZARA YA USTAWI WA JAMII, MAENDELEO YA VIJANA WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	616,000,000
Kifungu 0501	Idara ya Wanawake na Watoto	320,000,000
Kifungu 1101	Idara ya Ustawi wa Jamii	570,600,000
Jumla ya Fungu		**1,506,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Mhe. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe inavyoonekana kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mheshimiwa kuhusu utaratibu kifungu cha 96.1 cha kanuni yetu ambacho Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba ninukuu.

> "Kabla ya Kamati ya Matumizi haijashughulikia fungu lolote la Makadirio ya Matumizi, fungu hilo kwanza litapelekwa kwenye Kamati inayohusika likafikiriwe na halitoletwa kwenye Kamati ya Matumizi ya Baraza Zima mpaka Mwenyekiti wa Kamati iliyopewa kazi ya kulifikiria fungu hilo atakapomuarifu Spika, kwamba Kamati yake imemaliza kufikiria fungu hilo."

Mhe. Spika, kwa kuwa Kamati zetu hizi zimepitisha mafungu katika kitabu hichi ambacho tunakizungumza.

Na kwa kuwa inaonekana kwamba sasa ni utaratibu kwa Wizara zote zikaleta mabadiliko makubwa katika mafungu ambayo yamepitishwa na Kamati zetu.

Mhe. Spika, kwa kufuata kanuni zetu ipasavyo napendekeza kwako na kwa Baraza, kwamba tufikirie kupata siku moja ikiwezekana kesho ili wizara zote zinazohusika ziende kwenye Kamati zao zikabariki mabadiliko ya mafungu hayo. Hiyo ni kufika pahala tukaona tunachokifanya hapa kinakwenda sambamba na Kanuni zetu tulizojiwekea wenyewe. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Wazo ni zuri na Kanuni inavyoelekeza ni sawa. Sasa ni kwa sababu haya mabadiliko na *amendment* ambazo zimefanyika na kusambazwa karatasi baadae. Lakini kimsingi kanuni hiyo aliyoisoma Mhe. Mwenyekiti wa PAC, Mhe. Omar Ali Shehe inahusiana na pale Kamati zinapokuwa zinapitisha Kasma hizi, na hatimae zote zikaliarifu kwamba shughuli zimemalizika na kazi iko tayari kwa kuletwa Barazani. Hiyo kimsingi Kamati zote zimeniambia hivyo.

Mimi nafikiri tusitoe maamuzi kwa yote isipokuwa kama kuna Wizara ambayo imefanya mabadiliko makubwa kiasi cha kusambaza karatasi nyengine kama hizi, basi Waziri atuarifu ili Kamati ipate kwenda kupitia hayo. Lakini kama kuna Wizara ambayo haina mabadiliko yoyote, basi itakuwa haina haja ya kurudia tena, na ile taarifa ambayo Spika alipewa mapema iwe inatosha. Sasa wizara zilizobaki wale Waheshimiwa Mawaziri ambao wamegundua baada ya kukaa pengine na Wizara ya Fedha, kwamba kumekuwa na mabadiliko ya hapa na pale.

Nadhani Makatibu Wakuu wawaeleze Mawaziri ili tuziombe Kamati zinazohusika zile wakakae ili kupitia upya, na iwe wepesi baadae kuja kutoa maelezo hapa na wakati huo Kamati itakuwa inaelewa kwamba kitu hichi kilipita kwao na hasa kuhusiana na ile hoja ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliisema. Kwamba kama kuna mabadiliko makubwa itakuwa mabadiliko hayo hayakupata uhalali wa Kamati, kwa sababu haikufanya kazi hapo kabla. Lakini kwa zile wizara ambazo hazina mabadiliko haitakuwa na haja kwamba zote tuziite wakapitie upya.

Hiyo itakuwa ni kazi ya Mawaziri na vile vile ni kesho kwa muda uliobaki itakuwa hatuwezi kuendelea kuwasilisha hoja ya Wizara ya Afya. Sina hakika kama Wizara ya Afya wana mabadiliko hayo, naona kuna mkono pale labda tumsikilize Mhe. Waziri, ili tuweze kuangalia nini cha kuweza kufanya juu ya utaratibu huu ambao Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya PAC ameueleza kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru sana, lakini ni vizuri tukaweka mambo haya sawa. Alipokuwa mwenzangu anawasilisha nilikuwa sina haja mie kuingilia kati nikaona kama vile najua sana.

Lakini haya mabadiliko tuliyoyaleta hapa ni baada ya Kamati. Tumekwenda kwenye Kamati, tumehojiwa, tumefanyiwa masahihisho na ndipo yakabidi masahihisho hayo yafikishwe kwa wenzetu Wizara ya Fedha ili kurekebisha kumbukumbu ziwe sawa. Sasa kwa nini tunaleta hizi, nimewaona wenzangu wawili, watatu akina Mhe. Haji Omar Kheri.

Mhe. Spika, tunaleta hizi kwa sababu hivi sasa inakuwa rahisi sana ukazipitia hizo zote kwa pamoja kuliko ukurasa mmoja ukafungua buku kubwa, ningekwambia Mheshimiwa hapo *wrong*, tukaanza kwenda huku. Lakini vyenginevyo tunaweza tukalifata hili na sisi tuka *draw attention hoo* hapo pamefanyiwa marekebisho, vyenginevyo hizi baada ya Kamati.

Mimi nina mifano hai kwenye *revenue* kwangu kulikuwa kuna mahali pamoja *revenue* hazikuoneshwa ikabidi turudi zikaonyeshwe. Mkurugenzi wangu wa hospitali aandike Barua kwa Kamati ili masahihisho hayo yafanyike. Kamati ikawapelekea Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha ikabadilisha *revenue* ya Wizara yangu ni baada ya matokeo ya Kamati. Sidhani kwamba tutakuwa tunaleta madudu haya tu kwa sababu tu tunataka urahisi. Nilitaka hilo niliweke sawa, tutakachoweza tulifanye kesho kwa Wizara yangu ni kwamba haya ni baada ya matokeo. Tunaweza kufata hili lakini nikasema Mheshimiwa hapo pamefanyiwa masahihisho. Nakushukuru Mheshimiwa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, natumia kanuni ya 96, nakusudia kusema kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi ambayo Mhe. Waziri amejaribu kuzungumza. Hoja ya Wajumbe ambayo mimi naiunga mkono kwamba kitu ambacho kinakuja hapa ni kile ambacho Kamati walikipitia. Ni kweli Katibu wetu walimuarifu Spika, kwamba Kamati imemaliza. Lakini hadi naondoka mimi mabadiliko ambayo Kamati waliyarekebisha ni mapato ya *first track*

Wizara ya Afya hawakuyaleta, tukahoji ndio wakaleta shilingi milioni 190. Lakini mabadiliko mengine ya ndani ambayo hata Mhe. Waziri akiyaangalia ni mapya. Kwa hivyo busara zao nadhani hata bila ya utata sisi Kamati tupo tayari kufika saa 7:00 tupitie tusaidie, ili Wajumbe wapate kitu halali ambacho Kamati imeridhia. Vyenginevyo itakuwa ni vigumu kuwapitisha.

Mhe. Spika, kuna mabadiliko ambayo Kamati hatujayaona ni mapya, hata Waziri mwenyewe pengine kayaona leo na jana. Kwa hivyo inakuwa vigumu sana kwa mujibu wa sheria kuyapitisha. Mimi kwa niaba ya Kamti yangu nipo tayari kukaa saa 7 kesho na Wizara kuyahalalisha kwa mujibu wa utaratibu ili tuwape wenzetu jambo sahihi kabisa.

Mhe. Spika: Mimi nafikiri maelekezo yangu yalikuwa yapo wazi kwamba hii ni kazi ambayo ni juu ya Mawaziri wenyewe. Kama Mawaziri kama alivyosema Mhe. Waziri wa Afya kama alivyosema Waziri wa Ustawi wa Jamii, kwamba haya mabadiliko mengine yamekuja baada ya maelekezo ya Kamati. Sasa ikibibi hivyo hakuna haja ya kusema kwamba tutoe *general statement* kwamba Kamati zote zirudi upya, hapana kuna kitu ambacho kwenye Kamati ilikuwa hatukupitia.

Basi waiarifu Kamati inayohusika, sisi tukipewa taarifa hapa kimsingi iwe mapema kabla ya ratiba ya Wizara ile haijafika. Ili wakakae wasawazishe bila ya shaka na watu wa Wizara ya Fedha watakuwepo ili kuweka masuala hayo sawa. Kwa zile wizara ambazo hazina mabadiliko au mabadiliko yamekuja baada ya Kamati kufanya kazi haina haja. Tutakwenda na ratiba yetu hii na hiyo itakuwa ndiyo itayotusaidia kwenda na ratiba hii. Vyenginevyo tutafika kila pahala iwe tunakwama na ratiba hii hatimae itakuja kushindikana.

Hatari yake tukimaliza muda uliowekwa kwa mujibu wa kanuni ya kupitia makadirio haya baadae hata yale majadiliano hapo ndio utaratibu. Majadiliano yakiwa hayapo tunakwenda kwenye Kasma moja kwa moja. Sasa hiyo nayo itakuwa ni jambo jengine, litatukwamisha kama tutapitiza ule muda uliowekwa kwa mujibu wa kanuni wa kupitia makadirio haya kwa siku 35 za kazi + siku 5 zikisha hizi + siku 5, kama kuna Wizara ambazo hazijaisha basi maana yake tuite Kamati ya Matumizi moja kwa moja bila ya maelezo yoyote. Hiyo nayo itakuwa hatuzitendei haki Wizara hizo, wala Wajumbe pia hatuwafanyii haki kwa kutochangia baadhi ya Wizara.

Nadhani tuwe makini kwenda na ratiba hii, ili isije ikafikia pahala baadhi ya Wizara zikawa hazikuchangiwa kabisa. Kwa hiyo nadhani maelezo nimeshayatoa na tukubali sasa kwamba Wizara ya Afya kwa muda uliopo hawezi kuwasilisha hotuba hii.
Kwa maana hiyo basi tusitishe shughuli zetu kutoka hapa na tuje kesho ambapo mara baada ya kipindi cha Maswali tutasikiliza Hotuba ya Wizara ya Afya.

Naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 10/7/2012 Saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:30 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 10/07/2012 saa 3:00 asubuhi)